Hii ni nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

**Kikao cha Tatu - Tarehe 6 Novemba, 2003**

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Viwango Tanzania kwa Mwaka 2000/2001. *(The Annual Report and Accounts of Tanzania Bureau of Standards for the Year 2000/2001)*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwanda Tanzania *(TIRDO)* kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2002 *(The Annual Report and Audited Accounts of the Tanzania Industrial Research and Development Organization for the Year Ended 30th June, 2002)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na.31

**Shamba la Katani la Mnazi**

**MHE. CHARLES H. KAGONJI** aliuliza:-

Kwa kuwa tangu Shamba la Katani la Mnazi libinafishwe hakuna dalili zozote za wazi za kuonesha nia ya kufufua zao la Mkonge na kwa kuwa mmiliki wa shamba hilo ameuza vifaa mbalimbali yakiwemo malori na matrekta na sasa kama sio vurugu na maandamano ya wananchi wa Kijiji cha Kwemkwazu ya tarehe 15 Juni, 2002 kuzuia tabia hiyo, Korona ya shamba hilo pia ingekuwa imeuzwa kwa matajiri wa Taveta, Kenya:-

(a) Je, hiyo ndiyo ilivyokuwa shabaha ya Serikali ya kubinafsisha shamba hilo na mashamba mengine ya katani au nia yake ilikuwa kuimarisha kilimo cha mkonge?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani kwa wamiliki wanaokwenda kinyume na masharti ya ubinafsishaji?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Mlalo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa nia ya Serikali ya kulibinafsisha shamba la Katani la Mnazi ilikuwa ni kufufua na kuimarisha kilimo cha mkonge. Hata hivyo, tangu shamba hilo libinafsishwe mwaka 1997 halijaonyesha bayana uwezo wa kufufua zao la mkonge pamoja na kuwa lilibinafsishwa kwa njia ya ufilisi. Hii imebainika zaidi baada ya Kamati ya Serikali kutembelea mashamba ya mkonge nchini mnamo Novemba, 2002. Mambo yaliyojitokeza ni pamoja na:-

- Kutokuwa na Meneja wa shamba mwenye sifa za kuendesha shamba hilo.

- Katika kipindi hicho zilipandwa hekta 20 tu kati ya lengo la hekta 400.

- Mwekezaji ameweza kuvuna tani 450 kati ya lengo la tani 1,710.

- Hakuna ukarabati uliofanyika kwenye kiwanda, wala zana zilizonunuliwa kwa ajili ya kufufua shamba na;

- Kushindwa kulipa mishahara ya wafanyakazi tangu Oktoba, 2001.

Kwa vigezo hivyo mwekezaji hajafanya juhudi za msingi za kufufua zao la mkonge.

(b) Mheshimiwa Spika, Shamba la Katani la Mnazi limebinafsishwa na Mamlaka ya Mkonge na ufuatiliaji wake uko chini ya Bodi ya Mkonge. Kutokana na hali inayojionyesha ni dhahiri mwekezaji aliyepatikana kupitia njia ya ufilisi mwaka 1997

hakuwa makini katika kufufua zao la mkonge katika Shamba la Katani la Mnazi katika kipindi cha miaka saba.

Ili kunusuru hali iliyojitokeza, Bodi ya Mkonge inashirikiana na *PSRC* katika kuchambua na kuhakiki ufanisi mdogo uliobainika katika kipindi hicho. Kutokana na uchambuzi wa awali upo uwezekano wa kunyang'anywa shamba la katani na kulirejesha Serikalini ili shamba hilo lijumuishwe na mashamba ya katani yanayobinafsishwa na Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma kwa ajili ya kupata mwekezaji makini wa kuendeleza zao la mkonge nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kagonji ameridhika, namwona Mheshimiwa Abdillahi Namkulala. Swali la nyongeza.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kuna utaratibu gani kwa hawa wamiliki wa Shamba la Mkonge likiwepo na Shamba lile la Kisiwa kama unataka kubadilisha matumizi ya mkonge kwenda matumizi mengine kama kufuga simba hivi; wanatakiwa wafanye utaratibu gani hao? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, utaratibu uliopo ni kubadilisha mpango wa uwekezaji mitaji au mpango wa ufanyaji kazi kwa maana ya *investment plan* au *business plan.*

**SPIKA:** Swali linalofuata Mheshimiwa Abdulla Lutavi.

Na. 32

**Kasi ya Ukuaji wa Uchumi wa Taifa**

**MHE. ABDULLA S. LUTAVI** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni nchi yenye utajiri mkubwa wa ardhi nzuri kwa ajili ya kilimo na ufugaji, mito mingi, maziwa makubwa, aina mbalimbali za madini, maeneo makubwa yanayofaa kwa utalii na kadhalika, lakini pamoja na raslimali zote hizo bado kasi ya ukuaji wa uchumi wetu ipo chini sana ikilinganishwa na ya wenzetu wengi katika nchi za dunia ya tatu:-

Je, kama tunayo ardhi bora na ya kutosha, siasa na sera zetu safi kabisa, raslimali-watu tunayo kwa wingi na uongozi safi upo, je, huku kuchechemea kwa uchumi wetu kunatokana na nini hasa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukubaliana na Mheshimiwa Abdulla Lutavi, Mbunge wa Tandahimba, kuwa ni kweli Tanzania ni nchi yenye ardhi bora na ya

kutosha, siasa na sera safi kabisa, raslimali watu ya kutosha na uongozi safi chini ya CCM.

Mheshimiwa Spika, vigezo hivi ni muhimu sana lakini pekee havitoshi kusukuma maendeleo ya uchumi wetu mbele. Kwa raslimali chini ya ardhi, kama madini bila ya mtaji na uwezo wa kutosha wa kuzichimba na kuzisafisha kibiashara na kuzifikisha kwenye masoko husika hakuwezeshi nchi kufaidika ipasavyo. Vivyo hivyo, pamoja a kutumia vizuri raslimali yetu kuu ya ardhi katika kuzalisha mazao ya chakula na biashara ambayo yanachangia sana katika kuongeza pato la Taifa, hali ya Soko la Dunia, kwa mazao yetu yote ya kilimo imeendelea kudorora mwaka hadi mwaka. Hali hiyo inachangiwa kwa kiasi kikubwa na utegemezi wa kuuza mazao ghafi ya kilimo ambayo ndiyo yenye bei ndogo katika Soko la Dunia. Mitaji midogo isiyoridhisha na teknolojia duni nayo inapunguza uwezo wetu wa kutumia raslimali zetu kwa kiwango stahiki katika kukuza Pato la Taifa. Bado tuna haja ya kuendelea na zoezi letu la kurekebisha uchumi na sera zetu za jamii ili kuhimili vishindo vya ushindani katika Soko la ndani, nje, kikanda na Kimataifa pamoja na suala zima la utandawazi. Sasa katika hali hii tutafanyaje?

Mheshimiwa Spika, nchi yetu pekee, kwa kiwango cha uchumi wake, haiwezi kubadilisha mwenendo wa masoko ya dunia. Hivyo basi, inatubidi kujifunza jinsi ya kutumia hali hiyo ili kupunguza athari zake kwa uchumi wetu na papo hapo kutambua umuhimu wa kuelekeza juhudi zetu katika maeneo mapya ya uchumi ambayo yanaonyesha matumaini ya kuongeza mapato kwa nchi kama uzalishaji wa bidhaa zisizo asilia, ambazo masoko yake ni mazuri. Mbinu nyingine ya kujikwamua katika hali hii ni kuongeza juhudi zetu za usindikaji na uzalishaji wa bidhaa za viwandani.

Ili kufanikisha hayo, hapana budi kuongeza juhudi katika kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje na hasa mitaji ya moja kwa moja na matumizi ya teknolojia ya kisasa. Pia, katika kukabliana na makali ya Soko la Dunia, nchi za aina ya kwetu, yaani zinazoendelea au za Dunia ya Tatu, hazina budi kuimarisha jumuiya zake mbalimbali za kiuchumi ili ziwe na nguvu ya pamoja katika Soko la Dunia, pamoja na kufanya biashara na mipango mbalimbali ya maendeleo baina yao wenyewe kwa manufaa ya watu wao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Abdulla Lutavi, atakubaliana na mimi kuwa hivi sasa tunashuduia dalili nzuri za mafanikio katika mwenendo wetu wa uchumi lakini ipo changamoto kubwa ya kuwa na ukuaji endelevu na kwa viwango vikubwa ili kutengamaza uchumi, kuboresha na kuendeleza huduma za kijamii na kiuchumi, hatimaye kutokomeza umaskini. Sisi sote tunawajibika kupambana na changamoto hizo katika kujenga uchumi imara wenye uwezo wa kukabiliana na ushindani. Ni vyema basi tukaendelea na juhudi zetu za kurekebisha uchumi wetu na kuimarisha miundombinu laini, migumu na ile ya kitaasisi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lutavi, ameridhika, sasa namwona, heeh! Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kichocheo kikubwa cha uzalishaji ni kupatikana kwa mikopo ambayo masharti yake ni nafuu kwa wakulima na kwa kuwa ziko asasi nyingi ambazo wananchi hawazielewi katika utoaji wa mikopo yao, je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha hizi asasi ambazo zinatoa mikopo zinakuwa wazi na rahisi kufikika kwa wakulima ambao ndiyo sehemu kubwa wanaoweza kuchangia Pato la Taifa letu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa moja ya kichocheo cha kuongeza uzalishaji ni upatikanaji wa mikopo hasa kwa wakulima wadogo wadogo. Serikali katika sera yake ya *Microfinance,* utoaji wa mikopo midogo midogo imeendelea kuhamasisha kwa kuelezea asasi hizo kwa mfano sasa hivi tumeanzisha Benki za Jamii katika maeneo mbalimbali. Tuna *Dar es Salaam Community Bank, Mwanga Community Bank* na kule Mufindi iko *Mufindi Community Bank.*

Lakini vile vile yako Mashirika ambayo siyo ya Kiserikali kwa mfano *PRIDE* na *SACCOS* ambazo pia zinahimizwa kuhamasisha wananchi kufikia mikopo hiyo ambayo inahitajika na wakulima wadogo wadogo. Kwa hiyo, kimsingi kutokana na sera yetu ya kukopesha wale wakulima wadogo wadogo, Serikali inaendelea na jitihada hizo ili wananchi hao wazifikie huduma hizo.

**SPIKA:** Narudi kwenye Chama Tawala, Mheshimiwa Henry Shekiffu. *(Makofi)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Waziri, lakini kutokana na uzoefu ambao umeonekana katika nchi zinazoendelea *(Tiger Nations),* Serikali za nchi hizo zimejitoa mhanga kuwezesha wananchi wake. Kutokana na majibu yanayotolewa na Serikali, haionyeshi dhamira ya kweli katika kuwawezesha wananchi. *(Makofi)*

Tunawezaje kuondoka bila Serikali kutamka na kuwekeza zaidi katika kuwezesha wananchi na uwazi ukawepo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa inaandaa sera ambayo itawawezesha wananchi kiuchumi katika nchi yetu. Sera hii karibu itakamilika na kama tutakumbuka hapa Bungeni tulishaleta semina kuhusu suala hili, lakini vile vile Serikali imeshaandaa Muswada wa kuwawezesha wananchi kiuchumi, nao utaletwa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge Watapata fursa ya kuujadili na kuupitisha. Lakini hii ni maendelezo tu ya sera ya zamani ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Kwa mfano, mifuko iliyoanzishwa huko nyuma ya wanawake, vijana na kadhalika.

Kwa hiyo, Serikali suala la kuwezesha wananchi limekuwa likishughulikiwa kwa muda wa miaka mingi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla hatujaendelea Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwatambua wageni walioko kwenye *Gallery* ya Bunge. Ni wageni kumi kutoka Ethiopia, ni wageni wa Askofu Dr. Mwamasika, wamekuja kumtembelea. Ni wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), tunawakaribisha Bungeni. *(Makofi)*

Tunaendelea, maswali kwa Ofisi ya Makamu wa Rais. Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar.

Na.33

**Fedha za Mfuko wa *TASAF***

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Kwa kuwa lengo la *TASAF* ni kupambana na hali ya kupunguza umaskini kwa kuwajengea wananchi shule, barabara, Vituo vya Afya, huduma za maji na kadhalika; na kwa kuwa katika Jimbo la Wawi imepitishwa miradi miwili ya maji katika Shehia ya Mvumoni na shule katika Shehia ya Wara tangu mwezi Februari mwaka 2003, lakini mpaka sasa miradi hiyo haijaanza kuteelezwa kutokana na ucheleweshwaji wa fedha za mfuko huo:-

(a) Je, Serikali itaanza utekelezaji wa miradi hiyo mipya katika Jimbo la Wawi mwezi gani?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kuendelea kuchelewesha fedha za miradi kunarudisha nyuma maendeleo ya maeneo husika na kuvunja nguvu na jitihada za wananchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, lenye sehemu (a) na (b) ningependa nitoe maelezo mafupi ya ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* una lengo la kupambana na umaskini kwa kuziwezesha jamii husika kupata huduma bora za kijamii hususan Elimu, Afya, Maji Miundombinu na kadhalika. Upatikanaji wa huduma hizo utategemea sana namna jamii husika inavyoweza kuwasilisha pendekezo la mradi unaolenga kuondoa kero kwa chombo chenye madaraka ya kupitisha miradi hususan Kamati ya Usimamizi ya Wilaya au Kamati ya Usimamizi ya Taifa. Mara baada ya kupitisha mradi, hufikishwa uongozi wa *TASAF* tayari kwa kupelekewa fedha baada ya kuridhika na rasimu iliyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya mafupi, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kuhusu miradi miwili ya Maji katika Shehia ya Mvumoni, kama alivyofanya masahihisho Mheshimiwa Mbunge na Shule katika Shehia ya Wara, Ofisi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* haijawasilishiwa rasimu ya miradi hiyo.

Hata hivyo, baada ya kuwasiliana na Ofisi ya *TASAF* ya Pemba, imefahamika kuwa miradi hiyo imepitishwa na Kamati ya Usimamizi ya Pemba tarehe 27 Agosti, 2003 na siyo mwezi Februari, 2003. Maelezo yaliyopo ni kwamba ukamilishwaji wa kumbukumbu muhimu unafanywa ili miradi hiyo iweze kuwasilishwa *TASAF* Makao Makuu kwa ajili ya hatua za tathmini na upelekaji wa fedha. Mradi wa Maji wa Shehia ya Mvumoni utalazimika kupitishwa na Kamati ya Usimamizi ya Taifa kwa sababu kiasi kinachotakiwa kuchangwa na *TASAF* ni shilingi milioni 56 ambacho kinazidi kiwango kinachoweza kupitishwa na Kamati ya Usimamizi ya Pemba ambapo kwa kawaida ni Shilingi milioni 25. *TASAF* Makao Makuu itachukua hatua mara tu maombi hayo yatakapowasilishwa.

(b) Kufuatana na maelezo yaliyotolewa hapo juu, hatuwezi bado kuzungumzia suala la ucheleweshaji wa kutuma fedha kutoka chombo husika.

Hata hivyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali daima itaelekeza jitihada zake katika kuunga mkono nguvu na jitihada za wananchi katika kujiletea maendeleo yao. Ni muhimu kusisitiza pia kuwa kuna taratibu zilizowekwa za kusimamia uendeshaji wa Mfuko huo wa Maendeleo ya Jamii yaani *TASAF.* Taratibu hizo ni lazima zifuatwe ili kuepuka hitilafu zinazoweza kujitokeza na hivyo kuathiri upatikanaji wa matunda ya Mfuko huo na maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa nina uhakika ripoti imeshapelekwa Makao Makuu na ripoti yenyewe mimi ninayo barua ambayo nimeipata na kwa kuwa katika kufuatilia kwangu juu ya miradi ya *TASAF* katika Jimbo langu la Wawi, nimepewa taarifa kuwa mpaka hivi sasa mradi utakaotekelezwa ni ule wa Shule tu katika Shehia ya Wara, lakini ule wa maji hautekelezeki kwa sababu kiwango ni kikubwa. Mimi nataka nimwulize Mheshimiwa Waziri, hii pesa ya *TASAF* kwa Pemba imemalizika au vipi? Kama haijamalizika kwa nini wanasema hautekelezeki na pesa ya *TASAF* maana yake ni kuhudumia wananchi katika maendeleo? Hilo la kwanza. *(Makofi)*

La pili, kwa kuwa katika hotuba yangu ya kuchangia bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais mwaka huu wa 2003 niliomba fedha za *TASAF* zipelekwe moja kwa moja *PBZ* Pemba kwa kuondoa usumbufu wa ucheleweshaji wa kupata wananchi, je, Serikali imetafakari vipi suala hili na utekelezaji wake ukoje? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimesema miradi hii miwili,

mmoja huu wa Shule uko chini ya uwezo wa Kamati kuidhinisha shilingi milioni 25. Ndiyo miradi mingi ambayo inatekelezwa iko kwa kiwango hicho na nimemthibitishia Mheshimiwa Mbunge hapa kwamba Mradi wa Maji siyo kwamba haupo, utatekelezwa lakini idhini yake inatakiwa itolewe kwenye Kamati ya Kitaifa na kwa sababu wameshapeleka takwimu zinazotakiwa, nimesema kwamba itapitiwa na wakiidhinisha utekelezaji utafuatwa.

Napenda nirudie kusema kwamba si kusema fedha za *TASAF* zimekwisha, isipokuwa tumejiwekea viwango ili walengwa wengi wafikiwe na pale ambapo kinavuka kiwango kile bado *TASAF* ina uwezo wa kuidhinisha kwa taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, mwisho niseme kwamba katika utekelezaji wa miradi hii ya *TASAF* vile vile Ofisi ya Waziri Kiongozi kwa upande wa Zanzibar, inahusika sana katika mgawanyo wetu wa madaraka.

Kwa hiyo, nina uhakika Ofisi ya Waziri Kiongozi itafuatilia vile vile kama tunavyofuatilia sisi Makao Makuu. Namwomba Mheshimiwa Mbunge kabla hajarudi Pemba, apitie Ofisi zetu pale Dar es Salaam ili tuweze kuona hatua gani zimefikiwa hadi sasa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali moja la mwisho la nyongeza. Mheshimiwa Msindai.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa vile miradi ya *TASAF* imeonesha mafanikio makubwa sana kwenye Wilaya zote ambazo zinatekelezwa hapa nchini, ni lini Serikali itaanza awamu ya pili ikiwemo na Wilaya ya Iramba?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, miradi ya *TASAF* imeonyesha mafanikio makubwa pale ilipotekelezwa na wananchi kuifurahia na ninachukua nafasi hii kuwapongeza wananchi pote nchini ambapo *TASAF* inatekelezwa kwa jinsi wanavyotekeleza miradi hiyo kwa ufanisi. *(Makofi)*

Kuhusu sasa kuingia kwenye awamu ya pili, ni kweli pia kwamba sehemu ya kwanza tulikuwa tumejihusisha na Wilaya 40, sasa tunataka twende nchi nzima na nilisema hapa wakati wa makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwamba *TASAF* imekwishajiandaa sasa kuingia awamu ya pili na imekwishafanya tathmini na wanaohusika kutoa fedha hizi ni *World Bank* na wameridhika kwamba utekelezaji ni mzuri na wameridhia kwamba sasa tunaweza kuingia awamu ya pili ambayo itahusisha nchi nzima. Tunatazamia kwamba miradi hiyo yaani awamu ya pili itaanza kutekelezwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2003/2004. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea, maswali kwa Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Abu Kiwanga.

Na.34

**Barabara ya Kidatu - Ifakara Kuunganishwa na Kihansi**

**MHE. ABU T. KIWANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa *Kilombero Sugar (ILOVO)* ndicho kiwanda kizalishacho sukari nyingi nchini tani 110,000 mwaka 2002/2003 na kwa kuwa *Ilovo* inakusudia kufungua kiwanda cha ukamuaji wa miwa huko Lwipa - Kuvuka Ifakara karibu kabisa na Kihansi ambapo uzalishaji wa *Kilombero Sugar* unakadiriwa kufikia tani 200,000 ambayo ni sawa na ya mahitaji ya sukari yetu hapa nchini baada ya ufunguzi wa kiwanda cha Lwipa na kwa kuwa Serikali imetenga fedha za kuwezesha kujengwa kwa barabara ya lami kutoka Kidatu hadi Ifakara jambo ambalo tunalipongeza sana:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa itakuwa vema ikiwa ya lami hiyo ingeendelezwa hadi kukutanisha na zile kilomita 25 zilizopo Kihansi hasa kwa kuzingatia uwezo mkubwa wa ki-hadhi uliopo kwenye sehemu hiyo ya Kilombero ya kukuza Sekta ya Kilimo nchini?

(b) Je, Serikali itakubaliana na mimi kuwa barabara ya lami hadi Mlimba itakuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo kwa wananchi wa Kilombero siyo tu kwa ulimaji wa miwa bali pia kwa kilimo cha pamba, alizeti na nafaka nyingine za mafuta, mazao ambayo yalishamiri hapo awali lakini yakatoweka kutokana na ukosefu tu wa miundombinu na kwamba mazao hayo hata kwenye Bajeti ya mwaka 2003/2004 yametiliwa mkazo?

(c) Je, ni lini barabara ya Kidatu - Ifakara itajengwa na itakamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero, kwa kuanzia na natoa ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Uswisi imepanga kuifanyia ukarabati barabara ya Kidatu hadi Ifakara kwa kiwango cha urefu wa Kilometa 74 ambayo ni sehemu ya barabara kuu itokayo Mikumi hadi Mahenge kwa hatua mbili tofauti.

Moja, ukarabari kwa kiwango cha lami na changarawe. Hatua ya kwanza itajumuisha jumla ya kilometa 34 kati ya kilometa 74 ambapo kilometa 12 kati ya hizo zitakarabatiwa kwa kiwango cha lami nyepesi *(Otter Seal)* na kilometa 22 zitakarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Aidha, mradi huu pia utajumuisha ujenzi wa madaraja mawili mapya ya Kiberege na Sagamaganga na madaraja mengine kadhaa yatakarabatiwa. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Uswisi kupitia Shirika lake la *SDC* na kuchangiwa na Serikali ya Tanzania. Jumla ya shilingi bilioni 3.0 zimetengwa kwa kazi hii.

Pili, matengenezo ya muda *(periodic maintenance),* kilometa 26 kati ya kilometa 40 zilizosalia zimepangwa kufanyiwa matengenezo ya muda maaluma na jumla ya shilingi milioni 310.0 zimetengwa na Serikali ya Tanzania kupitia Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi huu sasa napenda kujibu kwa ufupi kabisa swali la Mheshimiwa Abu Kiwanga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na inauona muhimu wa kuunganisha barabara ya Kidatu - Ifakara yenye urefu wa kilometa 74 na ile ya Ifakara hadi Kihansi yenye urefu wa kilomita 125 kwa kiwango cha lami ili kukuza Sekta ya Kilimo na maendeleo ya wananchi kwa ujumla. Kwa saa Serikali haina fedha kwa ajili ya kujenga barabara hiyo yote kwa kiwango cha lami. Aidha, barabara hii imekuwa ikitengewa fedha kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ili kuiwezesha kupitika wakati wote.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizra ya Ujenzi kwa niaba ya Serikali inakiri kabisa kuwa, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami hadi Mlimba kutachangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya wananchi wa kilombero na kunyanyua Sekta ya Kilimo si kwa Mkoa wa Morogoro tu, bali kwa nchi nzima. Kwa hiyo, Serikali itaendelea na juhudi zake za kutafuta fedha hatua kwa hatua ili kuwezesha barabara zinazounganisha sehemu muhimu kiuzalishaji kama Kihansi na kadhalika, zitengenezwe kwa kiwango cha lami.

(c) Mheshimiwa Spika, ukarabati na matengenezo ya barabara ya Kidatu - Ifakara kwa sasa yako katika hatua mbalimbali ya kuwapata Makandarasi ambao watazifanyia kazi hizo barabara. Kazi zote hizi zinategemewa kukamilika ifikapo mwaka ujao wa fedha.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize swali moja la nyongeza na kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyonipa na suala linahusu barabara ya Kidatu - Mahenge kwa sababu Wilaya hizi Mahenge na Ulanga zina historia ya kushirikiana kiuchumi, lini Wizara inafikiria itaanza kuangalia taratibu ya kuweka Daraja la Mto Kilombero? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninajua sana kwamba suala la daraja katika Mto Kilombero linauma sana na ndiyo kero kubwa. Lakini daraja lile ni kubwa mno, linafanana karibuni na urefu wake nusu ya daraja la Rufiji. Tumepata watu wanajitahidi, Waswisi wanataka hilo na Wajapani wanajitajidi kupima. Kwa hiyo, tungojee matokeo ya wenzetu hawa ili tuweze kuwa na uhakika tunapofanya maamuzi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Kepteni Kasapira. Uliza swali la nyongeza.

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba Wizara ifanye jambo moja. Inaweza kuliambia Bunge kwamba Serikali ina mpango wa kujenga daraja la Mto Kilombero ili wananchi wa Wilaya ya Ulanga na Kilombero wawe na matumaini hayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi mwenyewe. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kama jibu zuri lilivyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, ujenzi wa daraja huwa unahitaji fedha nyingi sana na kwa kutambua umuhimu wa usafiri katika Mto Kilombero na ndiyo maana Serikali katika Bajeti ya mwaka jana ilinunua kivuko chenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 800.

Kwa hiyo, napenda niseme wazi kwamba Serikali haiwezi ikatamka kwamba itatengeneza daraja, bali kivuko hicho kitaendelea kuhudumia mpaka hapo uwezo wa Serikali utakapowezekana wa kutengeneza daraja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa.

Na.35

**Ujenzi wa Barabara ya Makuyuni - Lalago**

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA** aliuliza:-

Kwa kuwa miaka minne iliyopita Serikali ilifanya upembuzi yakinifu kuhusu ujenzi wa barabara ya Makuyuni - Lalago kwa kiwango cha lami:-

(a) Je, utafiti na upembuzi uliofanyika umetoa taarifa gani na kwamba barabara hiyo inategemewa kupitishwa katika Vijiji na Miji ipi kati ya Makuyuni na Lalago?

(b) Kwa kuwa kazi ya upembuzi imefanyika katika kipindi cha miaka minne iliyopita, je, ujenzi wa barabara hiyo utagharimu fedha kiasi gani?

(c) Kwa kuwa sehemu ya barabara hiyo yaani kutoka Makuyuni - Njia Panda inategemewa kukamilika kwa kiwango cha lami, wakati wowote kuanzia sasa, je, sehemu ya barabara itakayokuwa imebaki itagharimu kiasi gani cha fedha na ujenzi wake unatarajiwa kuanza na kukamilika lini hasa ikizingatiwa kuwa barabara hiyo ni kiungo muhimu cha kuunganisha Mikoa ya Shinyanga na Arusha?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utafiti na upembuzi yakinifu uliofanywa kati ya Septemba, 1999 na kukamilika Aprili, 2000 na hivi kufikia takriban miaka minne iliyopita umeonyesha kwamba ujenzi wa barabara ya Makuyuni-Lalago yenye urefu wa kilomita 252 kati ya Karatu na Lalago kwa kiwango cha lami utakuwa ghali sana, hata hivyo Serikali bado inafuatilia tathmini hiyo na uwezekano wa kupata wafadhili wa

kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Utafiti ulipendekeza barabara hiyo kupitia maeneo ya Karatu, Makutano ya Oldean, Barai, Bukundi, Mwanhuzi (Wilaya ya Meatu) na Lalago.

(b) Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanyika wakati huo ulionyesha kuwa barabara hiyo itahitaji kiasi cha fedha za Kitanzania shilingi bilioni 102 kati ya njia panda ya Karatu na Lalago.

(c) Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu nilioutaja haukuhusisha sehemu ya barabara ya Makuyuni-*Ngorongoro Gate* yenye urefu wa kilomita 77 kwani wakati huo sehemu hii ilishapata ufadhili kwa msaada kutoka Serikali ya Japan. Hivyo gharama za ujenzi zilizokadiriwa na upembuzi yakinifu kwa sehemu iliyobaki kati ya Karatu Lalago inabaki kuwa fedha za Kitanzania shilingi bilioni 102. Utekelezaji wa sehemu hii ya mradi utafanyika muda wowote baada ya kuwapata wafadhili ama hali ya uchumi wetu itakaporuhusu.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Naomba nimwulize swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba Mheshimiwa Waziri apokee pongezi zetu kwa kukubali sasa barabara ya Karatu-Barai mpaka Matala ambayo iko mpakani na Shinyanga kuwa katika barabara za Mkoa. Je, atapokea shukrani hizo?

Pili, ni imani yetu kuwa kazi iliyofanyika kwa fedha nyingi haitapotea na ninaomba Mheshimiwa Waziri arudishe sasa ujenzi wa barabara hii katika mipango yake ya kila mwaka kwa sababu katika bajeti ya mwaka jana kwa bahati mbaya barabara hiyo haikuonekana tena. Kwa hiyo, ili isipotee tunaomba iendelee kufuatiliwa na iwe katika ratiba ya kawaida wakati utafutaji wa fedha unaendelea.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na kwa niaba ya Serikali napokea shukrani kutoka kwa Mheshimiwa Dr. Willbrod Peter Slaa, Mbunge wa Karatu na hii inaonyesha kwamba Serikali inafanya kazi zake. *(Makofi)*

Ya pili, ili mradi tulikwisha gharamia gharama za upembuzi yakinifu, maana yake barabara hii iko kwenye mipango ya Serikali. *(Makofi)*

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Ahsante Mheshimiwa Spika, bila shaka Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba barabara aliyotaja ina mgogoro kwa vile inapitia katika mapito ya wanyama kati ya Ngorongoro-Yaeda na Manyara na kwa vile wananchi hasa wadau wa usafirishaji wako mbele ya Serikali kwa vile sasa siyo ya chini ya mabasi ya abiria manne yanasifiri kati ya Meatu na Mbulu kupitia Mkundi na Ibada.

Je, Serikali itakubali hadi lini kuwaona wananchi wake wako mbele yake na kwa ajili hiyo basi itawapeleka wataalam wake kuangalia *traffic* kati ya Meatu na Mbulu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hiyo ni kweli ina magari mengi sasa. Tumepata taarifa kwa *Regional Manager* na hali kadhalika ina sehemu za wanyama. Lakini hili lisimsumbue Mheshimiwa Mbunge, hiyo ni wajibu wetu pale tunapotengeneza barabara na kuangalia *traffic* kiasi gani, tutafanya kazi hiyo. Ndiyo kazi yetu.

Na. 36

**Matatizo ya Chuo Kikuu cha Kimataifa *(IMTU)***

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH** aliuliza:-

Kwa kuwa taarifa nyingi toka kwenye vyombo vya habari zinaashiria kwamba kuna matatizo makubwa katika Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Uganga na Teknolojia *(International Medical and Technological University - IMTU)* ambayo yamesababisha wanafunzi kugoma kuingia madarasani:-

(a) Je, Serikali ina kauli gani kuhusu taarifa unazopata?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani katika kutafuta ufumbuzi?

(c) Je, haki na usalama wa wanafunzi wa Kitanzania vinalindwaje katika mzozo huo?

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata taarifa toka vyombo vya habari zinazohusu malalamiko ya wanafunzi wa *IMTU,* Wizara yangu kwa kupitia Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu *(BEJ)* iliunda Kamati ya watu wanne kuchunguza na kuchambua malalamiko ya wanafunzi kuhusu chuo hicho.

Kamati iliwahoji wanafunzi na wazazi wao na pia ilitembelea chuo na kukusanya taarifa mbalimbali. Kamati iligundua mapungufu mengi katika uendeshaji wa chuo pamoja na kwenye ufundishaji wa mtaala wa udaktari. Kamati iligundua pia kwamba chuo hicho kilikuwa na idadi ndogo ya wahadhiri wenye sifa zinazotakiwa. Mapungufu yote haya ni ukiukwaji wa miongozo na ushauri wa Baraza kwa vyuo vikuu.

Kutokana na mapungufu haya, Baraza lilisitisha haki za *IMTU* za kudahili wanafunzi wapya hadi watakapohakikisha kwamba kasoro zote zilizoonekana

zimesahihishwa. Chuo kiliarifiwa kuhusu mapungufu yaliyoonekana na kutakiwa kuchukua hatua za haraka za kurekebisha hali hiyo.

Chuo kilikaguliwa tena mwezi Mei , 2003 ili kuona kama marekebisho yaliyotarajiwa yamefanyika kikamilifu na hivyo kuliwezesha Baraza kurejesha haki za *IMTU* kudahili wanafunzi wapya. Kamati ya Baraza ya uchunguzi haikuridhika na matokeo ya hatua zilizochukuliwa na chuo hicho. Hivyo bado Baraza halijaridhika kwamba *IMTU* inaweza kuruhusiwa kupokea wanafunzi wapya.

Mheshimiwa Spika, tarehe 1 Oktoba, 2003 chuo kilitembelewa tena kujadili njia za chuo kuharakisha utekelezaji wa maagizo ya Baraza ili ikibidi kikao maalum cha Baraza kiweze kuitishwa kwa ajili yao. Chuo kinaendelea kutekeleza maagizo ya Baraza na kujiwekea malengo ya kuyakamilisha kabla ya mwisho wa mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, katika kulinda haki za wanafunzi waliokuwepo chuoni hapo, Baraza lilikitaka chuo hicho kutekeleza yafuatayo:-

- Kuhakikisha wanafunzi watakaotaka kuhamia vyuo vingine kuendelea na masomo yao wanasaidiwa kufanya hivyo.

- Kuhakikisha chuo kinawapatia wanafunzi watakaoendelea na masomo chuo hapo masomo ya ziada kinadharia na kivitendo ili waweze kufikia kiwango cha elimu ya udaktari kinachokubalika kimataifa.

- Kuhakikisha chuo kinaajiri wahadhiri wa kutosha na wenye sifa za kufundisha katika ngazi ya chuo kikuu.

**MHE. KIDAWA HAMAD SALEH:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza.

Kwa vile Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kuwa Chuo hiki kina mapungufu makubwa na kinaendelea kusuasua katika kurekebisha matatizo hayo yaliyokuwepo. Je, Serikali inaweza kutuambia inakadiria ni lini Chuo hiki kitaweza kutambulika ili na wale wanafunzi ambao walishatumia pesa zao nyingi na muda wao mkubwa na kumaliza bila kutambulika waweze kutambulika na kuwa madaktari halisi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi. Chuo cha *IMTU* kitarejeshewa haki zake za kudahili wanafunzi wapya na kutambulika hapo tu kitakapoweza kutekeleza mapungufu yote ambayo yamejitokeza. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza na naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Kwa kuwa tatizo la *IMTU* ni mfumo na uongozi mzima na kwa kuwa maamuzi ya *IMTU* yanatokea India na kwa kuwa mhusika mkuu yuko India na lazima atoe kibali ili maelekezo haya ya Serikali yaweze kutekelezeka na kwa kuwa ameelekea kutokushirikiana, je, Serikali inatoa uhakika gani kwamba haya maelekezo yatatekelezwa ili vijana Watanzania ambao wamepoteza muda wao wasipoteze haki zao baada ya kukaa zaidi ya miaka minne au mitano pale? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba matatizo ya chuo kikuu cha *IMTU* yanatokana sana na mfumo na uongozi hivyo basi katika mambo muhimu ya kuzingatiwa ambayo wamepewa Chuo cha *IMTU* ili warejeshewe haki zao za udahili na chuo kutambulika ni pamoja na kuwa na Baraza thabiti la Chuo Kikuu hicho na hiyo ina maana kwamba, Mwenyekiti wa Baraza asiwe yule anayeishi nje ya nchi awe anaishi hapa nchini. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. *(Makofi)*

Kwa kuwa Naibu Waziri ametuambia kwamba baada ya kupata malalamiko kwenye vyombo vya habari ndipo Tume iliundwa, nilitaka kujua Serikali ina mikakati gani na utaratibu gani wa kuweza kuviratibu hivi vyuo si *IMTU* peke yake, badala ya kungojea malalamiko kwenye vyombo vya habari. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuona umuhimu wa kudhibiti mwenendo na hadhi ya elimu ya juu nchini, kupitia Bunge lako Tukufu ilipitisha Sheria ya kuunda Baraza la Elimu ya Juu, ambalo inakutana si chini ya mara nne kwa mwaka na linafanya ukaguzi wa vyuo vikuu vyote, vyuo vikuu vya binafsi na vyuo vikuu vya Serikali na wale ambao wanaenda chini ya hadhi ya chuo kikuu, Baraza hili ni kali kweli kweli, halitawaonea haya kuwateremsha hadhi.

Kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hatungojei taarifa za magazeti au zinazotoka kwenye vyombo vya habari. Tuna utaratibu kamilifu wa kwenda katika kila chuo kudhibiti na kuhakiki ubora wa elimu ya juu. *(Makofi)*

Na. 37

**Utaratibu wa Kujiunga na Chuo Kikuu - Dar es Salaam**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa njia mojawapo inayotumika kuchagua wanafunzi wa Shahada za Kwanza kujiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni kuwa na *Private Sponsorship,* utaratibu ambao haufahamiki na watu wengi:-

(a) Je, Serikali kwa kushirikiana na Chuo hicho inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba utaratibu huo unafikishwa kwa wananchi wengi?

(b) Kwa kuwa masharti ya kujiunga na Chuo hicho kwa utaratibu uliowekwa ni pamoja na mhusika kwenda Chuoni hapo kuchukua fomu maalum za kujiunga na Chuo baada ya kuonyesha vyeti, kufanya mtihani wa *matriculation* na kadhalika. Je, isingefaa utaratibu huo ukafanyiwa pia kwenye vituo tofauti yaani *Zonal Centers* ili kurahisisha zoezi hilo?

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dar es Salaa kimeweza kupanua udahili au kuongeza idadi ya nafasi za masomo ya shahada ya kwanza, kwa njia ya mpango kamambe wa Chuo hicho. Hata hivyo hivi sasa waombaji wenye sifa za kujiunga na masomo ya Shahada ya Kwanza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni wengi kuliko uwezo wa Serikali wa kuwadhamini wanafunzi hao.

Maombi ya nafasi za masomo hupelekwa chuoni. Chuo ndicho kinafanya kazi ya kuchambua na kuchagua wanafunzi wenye sifa za kujiunga na chuo na vile vile wanafunzi ambao watadhaminiwa na Serikali. Vigezo vinavyotumika ni sifa za kitaaluma. Mwenye sifa nzuri zaidi za kitaaluma ana nafasi nzuri zaidi ya kupata ufadhili wa Serikali. Baada ya uchaguzi huu wa swali, hatua inayofuata ni chuo kutangaza nafasi zilizobaki, ambazo zinaweza kujazwa na waombaji wenye sifa na uwezo wa kujilipia.

Matangazo hayo hutolewa kwenye magazeti kadhaa yasomwayo na wananchi wengi zaidi yakiwemo Mtazania, Uhuru, Majira, *Daily News, Sunday News, The Guardian* na *The Sunday Observer.*

Ili kuwafahamisha wananchi wengi kuhusu ufadhili binafsi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeanzisha utaratibu wa kusambaza taarifa mbalimbali za chuoni hapo, zikiwemo zinazohusu udahili kwenye shule mbalimbali za sekondari na pia katika Ofisi za Maafisa Elimu wa Mikoa. Pia taarifa hizo zipo kwenye tovuti *(Website)* ya Chuo Kikuu ambayo ni *(www.udsm.ac.tz).*

Vile vile kwenye banda la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwenye Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara hapo Uwanja wa Maonyesho wa Mwalimu Nyerere, *Kilwa Road* kila mwaka Chuo Kikuu hutoa taarifa mbalimbali kwa wananchi kuhusu Chuo, zikiwemo zile za udahili wa wanafunzi na ada mbalimbali zinazotozwa. Fomu za kujiandikisha kujiunga na Chuo pia hupatikana hapo.

Aidha, kwa lengo la kurahisisha na kupunguza gharama kwa waombaji, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeanzisha utaratibu wa upatikanaji wa fomu za maombi

*(application forms)* Mikoani. Hivyo licha ya kupatikana hapo Chuoni na kwenye tovuti, fomu hizi pia sasa zitakuwa zikipatikana kwenye Ofisi za Maafisa Elimu wa Mikoa, kama ilivyotangazwa na Chuo hivi karibuni kwenye magazeti ya Uhuru tarehe 3 Novemba, 2003 na *The Guardian* tarehe 4 Novemba, 2003. Vile vile taarifa zote kuhusu programu zitolewazo hapo Chuoni zitakuwa zikipatikana pia kwenye Ofisi hizo za Maofisa Elimu wa Mikoa.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa mara kadhaa Serikali imekuwa ikitamka kwamba itasaidia kusomesha wanafunzi wa vyuo vikuu binafsi. Je, utekelezaji wa azma hiyo utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, Serikali inapotoa ahadi ina azma ya kufanya hivyo na Mheshimiwa Mwanne Mchemba, anafahamu kwa uhakika jinsi ambavyo Serikali yetu ilivyo makini katika kutekeleza ahadi zake. *(Makofi)*

Hivyo namhakikishia kwamba wanafunzi wanaosoma katika vyuo binafsi na tuliahidi ni wale wanaochukua Udaktari, watalipiwa na Serikali kama ilivyoahidiwa. *(Makofi)*

Na. 38

**Mifereji ya Maji ya Umwagiliaji ya Asili**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi haiwezi kutegemea mvua tu katika kilimo na kwa kuwa katika jimbo la Bumbuli ipo mifereji ya maji ya umwagiliaji ya asili ya Ngwezii, Kata ya Soni na Mbuzii, Magila, Kata ya Soni, Mayo, Kata ya Mayo, Kwanguruwe, Kilangwi na Mbokoi, Kata ya Bumbuli:-

(a) Je, Serikali ina habari za mifereji hiyo ya asili na inatumika kumwagilia hekta ngapi za mazao?

(b) Je, ipo mifereji mingine ya asili zaidi ya hiyo iliyotajwa hapo juu katika jimbo la Bumbuli?

(b) Je, Serikali imeshatoa misaada ya aina gani ya kusaidia juhudi za wananchi wanaotumia mifereji hiyo ya asili na ina mipango gani ya kutoa misaada ya kitaalam kwa ajili ya mifereji hiyo ili itumike zaidi wakati huu wa uhaba wa mvua?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ina habari na mifereji ya asili ya Ngwei, Magila, Mayo, Kwanguruwe, Kilanwi na Mbokoi aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge. Mifereji hiyo inatumika kumwagilia eneo lenye ukubwa wa jumla ya hekta 274.

(b) Katika jimbo la Bumbuli ipo mifereji mingine 59 ya asili yenye uwezo wa kumwagilia eneo lenye ukubwa wa jumla ya hekta 2800.

(c) Katika kusaidia juhudi za wananchi wanaotumia mifereji hiyo ya asili, Serikali kwa msaada wa Serikali ya Uholanzi, ilifanya ukarabati wa mifereji hiyo chini ya Mradi wa ukarabati wa mifereji ya asili ambao sasa imebadilishwa kuwa Shirika lisilo na Kiserikali *(NGO)* linaloitwa *Traditional Irrigation Improvement Project (TIP).*

Aidha, wataalam wa Wizara wa Umwagiliaji wa Kanda ya Kaskazini wanashirikiana na Mafundi Sanifu wa Umwagiliaji wanne waliopo Wilayani Lushoto katika kuendeleza kilimo cha Umwagiliaji maji mashambani kwa kutmia mbinu zilizoanzishwa na mradi wa *TIP*. Wataalam hao ndio waliofanya usanifu na kusimamia ukarabati wa mifereji katika skimu za Magila, Mayo, Kwanguruwe, Kilanwi na Mbokoi.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa imedhihirika wazi kabisa kwamba kilimo cha kutegemea mvua hakiaminiki na kwa kuwa nchini kuna mifereji mingi, je ni lini Serikali itatuletea master plan ya kuendeleza mifereji hii ili tuitegemee kwa ajili ya kuzalisha mazao ya biashara na chakula? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, tunayo *master plan* kwa kuwa swali liliulizwa juu ya mifereji hiyo, sikutaka kuelezea *master plan* lakini nitakapohitajika kufanya hivyo nitafanya.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, inafahamika kwamba Tanzania inalo eneo lenye ukubwa wa hekta milioni 6 ambazo zinafaa kwa ajili ya umwagiliaji maji na vile vile inafahamika kwamba Tanzania ina maji mengi chini ya ardhi. Ukichukua yote hayo tuna maji mengi kuliko nchi yoyote katika Tanzania au nchi za jirani.

Je, Waziri hata kama hakuwa ameulizwa swali hilo hawezi kulieleza Bunge hiyo *master plan* kama ipo kuwa ataigawa kwa Wabunge ili tuweze kujua anafanya nini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, tulieleza wakati tulipotoa hotuba hapa Bungeni kwamba tulikuwa tunaandaa *Irrigation Master Plan* na katika *Irrigation Master Plan* hiyo hatua za kwanza zinaonyesha kwamba Taifa lina hekta zipatazo 29.4 zinazoweza kumwagiliwa maji. Kwa hiyo, tunaendelea kuandaa *Master Plan* hiyo itakapokamilika tutalipa tena Bunge hili taarifa na utekelezaji utafuata.

**SPIKA:** Tunaendelea! Namwomba radhi mwuuliza swali linalofuata kwamba kumbukumbu za Bunge hazijarekebishwa, bado tuko katika kumbukumbu za zamani. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. *(Makofi)*

Na. 39

**Mfereji wa *FIDIA* kwa maji ya Umwagiliaji**

**MHE. ANNE K. KILANGO** aliuliza:-

Kwa kuwa mnamo mwaka 1959 - 1960 Serikali kwa kushirikiana na wananchi wa kata ya Ndungu Wilayani Same ilichimba mfereji uitwao *FIDIA* wenye urefu wa takriban kilomita 8 kwa madhumuni ya umwagiliaji ili wananchi wajipatie mazao ya chakula na biashara, na kwa kuwa mfereji huo ulikuwa na uwezo wa kumwagilia ekari zipatazo 600 ambazo ziliweza kuwanufaisha zaidi ya wananchi 16,000 wa kijiji hicho na kile cha Kalemawe:-

(a) Je, Serikali inayo taarifa kwamba mfereji huo umeharibika kabisa na kuzifanya ekari 600 zilizokuwa zikilimwa kwa umwagiliaji zisilimwe tena kwa kipindi kirefu sasa?

(c) Je, Serikali kwa nia ya kuwapunguzia kero ya umaskini wananchi wa kata hiyo, inaahidi kuchukua hatua gani za makusudi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Kuteuliwa, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mfereji wa *FIDIA* ulijengwa na Serikali ya Kikoloni ya Waingereza kati ya mwaka wa 1958 na 1960 kwa lengo la kumwagilia eneo la ekari zipatazo 600. Baada ya ujenzi wa mfereji huo kukamilika, Serikali ilisimamia uendeszhaji wake kwa muda na kisha ikaukabidhi kwa wakulima ili wausimamie uendeshaji wake wenyewe.

Mnamo mwaka wa 1983, Serikali ya Tanzania kwa ushirikiano na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan *(JICA),* ilianza maandalizi ya ujenzi wa mfereji wa Bonde la Mkomazi linalojumuisha eneo la Ndungu chini ya mradi uliojulikana kama *Ndungu Development Project.* Ujenzi wa mfereji huo ulikamilika mwaka wa 1990 na ulikuwa na uwezo wa kuhudumia eneo la hekta 680 ambazo zingeweza kulimwa mara mbili kwa mwaka na wakulima 13,000 wa vijiji vya Ndungu, Misufini na Kalemawe. Wakulima ambao hawakupata mashamba kwenye mfereji wa Ndungu waliendelea kutumia mfereji wa *FIDIA,* jambo ambalo lilianzisha mgogoro wa kugombea maji kati yao na wale wa mradi wa Ndungu.

Mwaka 2000, Serikali ilifanya uchunguzi wa mgogoro huo wa kugombea maji na ikabainika kwamba maji mengi yalikuwa yakipotea kabla hayajafika mashambani kutokana na mfereji huo kuwa mrefu sana na pia kutokana na mfereji kujaa mchanga kutokana na wakulima kutokuwa na utaratibu wa kuutunza.

Baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kutokana na maelezo niliyotangulia kutoa, ni dhahiri kwamba Serikali ina taarifa juu ya kuharibika kwa mfereji wa *FIDIA* ambako kumefanya eneo lililokuwa likihudumiwa na mfereji huo lisitumiwe kwa kilimo cha umwagiliaji maji.

(b) Kazi za awali za kubaini matatizo ya mfereji huo zilishafanyika tangu mwaka wa 2000. Serikali itashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Same kuandaa makisio ya gharama za kurekebisha uharibifu uliotokea kwenye mfereji huo na kuzuia upotevu wa maji kwa kuzama ardhini na kutafuta fedha za kuyagharamia. Aidha, Serikali itawahamasisha na kuwapa mafunzo wakulima juu ya kuunda na kuimarisha vikundi vya umwagiliaji maji mashambani ili wakulima wenyewe waweze kutunza mifereji na kusimamia matumizi bora ya maji.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, je, isingekuwa bora kwa Serikali kukarabati mfereji wa *FIDIA* badala ya kuendelea kukarabati mfereji wa Mradi wa Japan ili yote miwili iweze kufanya kazi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI YA KILIMO NA CHAKULA :** Mheshimiwa Spika, hayo yote yanafanyika siyo mfereji mmoja, lakini tunashughulikia mradi wote kwa ujumla.

Na. 40

**Uamuzi wa Daktari wa Kuondoa Uhai wa Binadamu**

**MHE. SALOME J. MBATIA** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni huko Iran imefanyika *operation* ya kuwatengenisha mapacha wa miaka 29 waliozaliwa wakiwa wameungana kichwa; na kwa kuwa upasuaji huo haukufanikiwa hivyo kusababisha mapacha hao kufariki dunia:-

(a) Je, ni wakati gani daktari anaweza kufanya uamuzi wa kutoa uhai wa binadamu mmoja ili kumnusuru mwingine kuliko kusababisha kifo cha binadamu wote wawili?

(b) Je, madaktari wa Tanzania wanasema nini juu ya kifo cha mapacha hao; na je, isingewezekana kuwa na uamuzi tangu mwanzo wa kumwokoa mmoja tu katika *operation* hiyo?

(d) Kama majibu katika sehemu (a) na (b) hapo juu ni hapana; je, inakuwaje wakati mwingine baadhi ya madaktari wanafanya uamuzi wa kusitisha mimba ili kuokoa maisha ya mama?

(e)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Salome Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mara zote inapothibitika kitaalam kwamba kutochukua hatua za upasuaji *(Surgical Intervention)* kutasababisha vifo vya binadamu wawili (iwe kwa mapacha walioungana au mama na mtoto aliye tumboni), kwa mujibu wa maadili ya Kidaktari *(Medical Ethics)* ni lazima wataalam wafanye upasuaji huo kwa madhumuni ya kuwaokoa wote wawili au angalau mmoja wao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salome Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wakati ambapo kutofanya upasuaji kutasababisha vifo vya watu wawili, daktari anaruhusiwa kufanya uamuzi wa kutoa uhai wa mmoja wao ili kunusuru maisha ya mwingine kwa masharti yafuatayo:-

(i) Uamuzi huo lazima ufikiwe na madaktari zaidi ya wawili na wawe wamefikia uamuzi huo kila mmoja peke yake *(independently).*

(ii) Lazima ipatikane ridhaa ya mama mwenyewe kwenye suala la kutoa mimba au kwa ndugu wa karibu.

(iii) *Operation* lazima ifanyike katika hospitali inayojulikana kuwa na mwenendo unaokubalika kimaadili.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu vifo vya mapacha toka Iran waliofariki Singapore, Wizara yangu inasikitika kwamba upasuaji huo haukufanikiwa. Nia ya upasuaji ilikuwa ni kuwatenganisha wakiwa hai wote wawili na wala sio kumnusuru mmoja wao.

Uamuzi wa kuwatenganisha mapacha hao tangu wakiwa wadogo haukuweza kuchukuliwa kwa sababu wakati huo teknolojia ya upasuaji haikuwa kubwa kama ilivyo hivi sasa.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, madaktari wanaweza kufanya uamuzi wa kuchukua hatua ya upasuaji endapo itadhihirika kitaalam kwamba kutofanya hivyo kutapoteza maisha ya watu wawili badala ya mmoja, mfano, ni pale ambapo kutoa mimba kunakuwa lazima ili kunusuru maisha ya mama au kwa watoto mapacha pale ambapo kutowatenganisha kunaweza kusababisha wote wawili wakafariki.

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Inapotokea ya kwamba panatakiwa kufanywa *operation* ya watu wawili ili mmoja abakie na mmoja afe; je, wale wahusika wanaofanyiwa *operation* wanaarifiwa juu ya taarifa hiyo? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nieleze kwamba inapofikiwa uamuzi wa kuondoa maisha ya pacha mmoja ili mwingine aweze kuishi, inatakiwa utaratibu wa kitaalam unaoonyesha kwamba bila ya kufanya hivyo wote wawili watapoteza maisha. Baada ya hilo huwezi ukafanya *operation* kama hiyo bila kujadiliana suala zima *either* na wazazi wa mapacha hao endapo mapacha ni wadogo na kama wana umri mkubwa basi wenyewe pia wanatakiwa wajadiliane suala hilo. Nasema hivyo kwa sababu moja kwamba, ni wakati gani uamuzi wa kuondoa maisha ya mmoja unachukuliwa, pale ambapo inaonekana wazi kwamba bila ya kufanya hivyo watafariki wote wawili kwa hiyo, kuwaeleza inakuwa siyo jambo la ajabu.

Na. 41

***Health Basket Fund***

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilianzisha Mfuko wa pamoja wa huduma za afya *(Health Basket Fund)* mwaka 2001 kwa ajili ya kuboresha huduma za afya nchini katika ngazi zote za huduma kuanzia zahanati, vituo vya afya na hospitali:-

(a) Je, Serikali inatathmini na kuratibu vipi ufanisi wa Mfuko huo tangu ulipoanzishwa?

(b) Je, isingekuwa busara kama Serikali ingetumia fedha za Mfuko huo kujenga majengo mapya kama vile wodi za wagonjwa, vyoo, matanki ya maji na kadhalika katika Zahanati za Vijijini kama zile za Isaka, Segese, Ntobo, Ngaya, Bulige, Chela, Ngogwa na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, shughuli za Mfuko huu zinazingatia miongozo na vigezo vilivyotolewa na Wizara yangu kwa ushirikiano wa pamoja na Wizara ya Tawala za

Mikoa na Serikali za Mitaa. Hivyo kila mdau anayotumia fungu hili hupaswa kuandaa mpango wa afya na mpango huo hupitiwa na kupitishwa na timu ya wataalam toka Wizara zote mbili. Baada ya kupitishwa mpango huo ndio hutumika kama mwongozo wa matumizi. Aidha, kila mdau ikiwa ni pamoja na Mikoa na Halmashauri hupaswa kutoa taarifa za matumizi kabla ya kupewa fedha zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, Mfuko huu hukaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ambaye huteua Shirika la kufanya kazi ya ukaguzi kwa niaba yake. Kazi hiyo kwa sasa inafanywa na *Pricewaterhouse Coopers.* Aidha, kila mwaka timu ya pamoja na wataalam kati ya Serikali na wahisani hufanya tathmini.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia Kamati ya pamoja kati ya Serikali na wahisani iliona ni vyema Mfuko huu ulenge katika kuboresha huduma za afya za msingi na kiasi cha 35% kitumike kuongeza ubora wa huduma za hospitali. Kwa kuwa nchi yetu ina mtandao mkubwa wa vituo vya kutolea huduma za afya, ilikubalika kwamba kwa kuanzia fedha za Mfuko huu utumike katika ukarabati wa vituo hivyo pamoja na kununua vifaa tiba *(Medical Equipments).* Baada ya hatua hii ya awali, Wizara yangu itawashauri wahisani wakubali kutumika kwa fedha hizi kwa ujenzi wa majengo mapya ya kutolea huduma kama Mheshimiwa Mbunge anavyoshauri.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa hivi sasa ni vyema tuoanishe mipango mbalimbali ya Serikali kama vile Mfuko wa *TASAF* ambao unajenga majengo mapya ya kutolea huduma za afya na huu wa *Basket Fund* ambao unatumika kufanya ukarabati wa majengo ya zamani na kununua vifaa ili kuwa na mwelekeo wa pamoja na kuongeza ufanisi katika kumhudumia mwananchi.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja ndogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuzungumzia hasa ukaguzi au tathmini. Pengine umekuwa ukifanyika ukaguzi wa vitabu vya hesabu kuliko kazi zinazofanyika kule, kuna maeneo ambayo ukarabati umefanyika, ni ukarabati wa kiwango cha chini sana kuliko ambavyo mahesabu yanaonyesha; je, hao Wakaguzi wanakwenda kuangalia huko kwenye *site* kazi zinazofanywa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba ukaguzi unaofanyika, unafanyika katika mahesabu ya fedha zilizotolewa. Lakini ni jukumu la Halmashauri ya Wilaya kuhakikisha ya kwamba ukarabati unaokusudiwa unafanyika kama inavyotakiwa, endapo kuna tatizo la kutofanyika ukarabati kama mahesabu yanavyosema, basi ni jukumu la Halmashauri kutoa taarifa kwa Wizara ili hatua zichukuliwe.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kuboresha ni pamoja na kuboresha majengo na vifaa; na kwa kuwa Serikali imefanya vizuri sana

katika mpango wa elimu ambapo imeshirikisha nguvu za wananchi; na katika swali la msingi la Mheshimiwa Emmanuel Kipole, ameeleza ya kwamba wananchi wapo tayari kujenga majengo mapya kwa kutumia Mfuko huu; je, Serikali haioni ni busara pale ambapo wananchi wako tayari waungwe mkono kwa kutumia Mfuko huu wa *Basket Fund* kama ilivyofanya katika Mfuko wa *MMEM? (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nilikwishasema kwamba uamuzi uliochukuliwa kati ya Kamati ya wataalam ya Wizara za Afya na ile ya TAMISEMI pamoja na watoa fedha hizi ambao ni wahisani, waliamua kwa pamoja kwamba kwa awamu hii fedha hizi zitumike kwa ukarabati. Tunaelewa fika kwamba nchi yetu ina mtandao mzuri sana wa Vituo vya Huduma za Afya lakini kwa bahati mbaya siku nyingi havijapata ukarabati na hivyo huduma hizo hazitolewi inavyostahili. Kwa hiyo, kwa awamu hii, inatakiwa tuhakikishe ya kwamba tunafanya ukarabati wa vituo vyote wakati huo huo katika kipindi hiki kuna Mfuko wa *TASAF* ambao unajenga majengo mapya. Lakini vile vile nilisema ya kwamba baada ya awamu ya ukarabati basi tutawashawishi wahisani hao, wakubali kutumia fedha hizi katika ujenzi wa majengo mapya hapo ndipo tutawaomba wananchi wajitolee katika kuhakikisha hilo linafanikiwa.

Na. 42

**Fedha za Kupunguza Umaskini kwa Njia ya Mikopo**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa shilingi 1,000,000/= kwa kila Wilaya kwa ajili ya kupunguza umaskini kwa njia ya kutoa mikopo kwa wanawake:-

(a) Je, ni vigezo gani vinavyotumika katika kutoa fedha hizo hasa ikizingatiwa kuwa kuna baadhi ya Wilaya zenye watu wengi na nyingine zina watu wachache?

(b) Kwa kuwa Sensa ya watu ya mwaka 2002 inaonyesha kwamba kuna ongezeko kubwa la watu; je, kiwango kinachotolewa kwa sasa si kimepitwa na wakati na kwamba sasa kuna haja ya kuongeza kiwango hicho?

(c) Je, fedha hizo hutolewa mara ngapi kwa mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kigezo kikubwa kinachotumika katika kutoa fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake kwa Halmashauri ni ugawaji sawa wa kijiografia *(Equitable Geographical Distribution).* Ni kweli inawezekana kutumia kigezo cha idadi

ya watoto katika Wilaya lakini haitakuwa endelevu ikizingatiwa kuwa Wilaya inaweza kuwa na watu wengi lakini sio wote wanaohitaji mikopo. Hii ni kutokana na sababu kuwa mahitaji ya mikopo ni hiari na hutegemea mazingira ya jamii iliyopo na shughuli ambazo wanaohitaji wanapenda kuzifanya.

Kigezo kingine ni urejeshaji wa mikopo. Utaratibu mpya wa sasa ni wa kimkataba kati ya Wizara na Halmashauri. Halmashauri zitakazorejesha mikopo kwa wakati uliopangwa zitaendelea kupewa fedha nyingine kwa kiwango kikubwa zaidi kutokana na ongezeko katika marejesho yake. Kigezo cha idadi si endelevu kwani idadi ya watu inaweza kuongezeka na kupungua kila wakati.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli idadi ya watu imeongezeka kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002. Inawezekana pia kukawa na mahitaji zaidi ya mikopo. Hata hivyo, uwezo wa kiuchumi wa Serikali hauwezeshi kutoa mikopo kutokana na ongezeko la watu. Ni kwa sababu hiyo pamoja na kuwepo kwa *WDF,* Serikali imeziagiza Halmashauri kuchangia asilimia kumi katika Mfuko wa Wanawake na ule wa Vijana kutokana na mapato yake.

Vile vile, Serikali imeweka mazingira mazuri ya uanzishwaji wa Mifuko mingine ya kupambana na umaskini ya mashirika ya umma na yale yasiyo ya Kiserikali. Hatua zote hizi ni katika kusaidia wananchi kupata mikopo ili kupunguza umaskini.

Pamoja na hayo, msingi mkubwa wa ukopeshaji ni marejesho ya mikopo hiyo. Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ni Mfuko wa mzunguko. Katika utaratibu wa sasa niliooutaja mwanzoni, unatarajiwa kuwezesha marejesho kwa kiwango kikubwa zaidi na hivyo kuufanya Mfuko uzunguke na kuwanufaisha walengwa wengi zaidi.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kawaida Serikali hutoa fedha hizo kwa mkupuo mmoja kwa mwaka. Hata hivyo, baada ya marejesho Halmashauri husika inakuwa na sifa ya kupewa fedha nyingine za mkopo kwa utaratibu wa mzunguko niliokwishautaja.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara hii kwa kuongeza kiwango cha shilingi milioni moja kufikia shilingi milioni nne. Mheshimiwa Naibu Waziri katika kujibu swali langu la msingi amesema ya kwamba wameandaa utaratibu kimkataba, tangu wameandaa huu utaratibu wa mkataba Serikali imezaa matunda gani katika kufanikisha kuboresha marejesho ya mikopo hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa niaba ya Serikali naomba kupokea pongezi hizo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kwa upande wa utaratibu huu mpya tuliouanzisha, hapa nina muhtasari wa Halmashauri za Wilaya, Miji na Jiji ambazo zimerejesha fedha baada ya uanzishwaji wa utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba nitaje baadhi tu ya Wilaya maana orodha ni ndefu tutawasambazia Waheshimiwa Wabunge hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kati ya Halmashauri 114 zilizopelekewa kiasi cha shilingi milioni nne kila Wilaya na walitakiwa kufanya marejesho kufikia mwishoni mwa mwezi Septemba mwaka huu, Halmashauri zilizofanya marejesho kwa viwango tofauti maana wako wengine hawakukamilisha shilingi milioni nne na laki nne, zile shilingi laki nne ni za asilimia kumi za riba, ni Halmashauri 27 kati ya Halmashauri 114. Halmashauri tatu tu ndizo zimerejesha kikamilifu yaani shilingi milioni nne na laki nne. Halmashauri hizo ni Halmashauri ya Geita, Jiji la Mwanza na Manispaa ya Morogoro. Kwa hiyo na mimi sina deni. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwani amesimamia vizuri mikopo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Halmashauri ambazo zinadaiwa, ni kwamba Halmashauri ya Mbulu shilingi laki moja. Sasa napenda kuomba kwamba Halmashauri ambazo hazijafanya marejesho kikamilifu, wafanye hivyo ili wapate mkupuo wa pili. Tunapenda kuwaongezea shilingi milioni nne nyingine. Wale ambao hawatafanya marejesho haya, kwa kweli hawatapata mkupuo wa pili. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nami napenda kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuendelea kutambua umuhimu wa wanawake katika Taifa hili lakini ninapenda nimwulize Mheshimiwa Waziri kama atakubaliana na mimi ya kwamba matatizo mengine yanatokana si kwa sababu wanawake hawataki kurejesha, isipokuwa inatokana na ubovu wa utendaji wa *Local Government;* je, hatakuwa tayari tufanye mchanganuo kidogo tuone kama tunaweza kupata njia nyingine zitakazorahisisha kuwafikishia wanawake hawa pesa hizi na kutafuta njia nyingine za kutunisha Mfuko huu?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, Halmashauri ambazo tumeingia nazo mkataba mpaka sasa zimeonyesha ya kwamba zinaweza zikafanya kazi vizuri. Mkataba huu ndio kwanza tumeingia nao mwaka huu kwa hiyo bado haujafikia wakati wa kufikia mawazo ya kwamba Halmashauri hazifanyi kazi vizuri. Hivi sasa tunaboresha mkataba huo na kutokana na marejesho ambayo mpaka sasa yamefanywa, tumeona ya kwamba Halmashauri zimekuwa na uwezo mkubwa zaidi kuliko utaratibu wa pale mwanzo.

Mheshimiwa Spika, katika hizo asilimia kumi ambazo zinatarajiwa katika mkopo huu, ni kwamba hizo asilimia kumi ambazo ni shilingi laki nne kwa sasa kutokana na zile shilingi milioni nne, zitatumika kwa ajili ya mafunzo na ufuatiliaji wa vikundi. Kwa hiyo, hiyo itarahisisha urejeshaji wa mikopo.

Na. 43

**Uvunaji wa Msitu wa *Sao Hill***

**MHE. PHILIP A. MAGANI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Semina ya Wizara ya Maliasili na Utalii iliyofanyika tarehe 5 Aprili, 2003 kwa Wabunge hapa Dodoma, Waziri wa Maliasili na Utalii alieleza kuwa Mwekezaji aliyepewa kibali cha kujenga Kiwanda huko *Sao Hill* alikuwa hajapewa kibali cha kuvuna msitu, lakini msemaji wa *Tanzania Investment Centre (TIC)* katika kauli aliyoitoa Jumatatu tarehe 7 Aprili, 2003 alithibitisha kuwa Mwekezaji huyo amepata kibali cha kuvuna msitu kwa kiwango cha mita za ujazo 100,000 kila mwaka baada ya kupitia ngazi zote husika:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya kauli hizo mbili?

(b) Ikiwa kibali cha kuvuna msitu kimetolewa; je, ni kwa miaka mingapi na kwamba mita za ujazo wa 100,000 ni sawa na hekta ngapi za msitu huo wa kupandwa?

(c) Je, mvunaji huyo amepewa sharti la kata mti, panda mti na kuwa na mpango rasmi wa upandaji miti kama sera yetu inavyosema na kama jibu ni hapana; je, mwekezaji huyo atatuachia nini kama sio jangwa?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Philip Magani, Mbunge wa Ruangwa, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Shamba la Miti la *Sao Hill* kama mashamba mengine ya miti yanayomilikiwa na Serikali, limeanzishwa na linaendelezwa kwa ajili ya biashara. Miti ikikomaa huvunwa na kuuzwa na maeneo yaliyovunwa hupandwa miti mingine. Hivyo, mashamba ya miti ni maeneo ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philip Magani, Mbunge wa Ruangwa, kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba Kampuni ya *RAIPLY* kutoka Kenya aliahidiwa kupatiwa mita za ujazo 100,000 za miti kwa mwaka kutoka katika Shamba la Miti la *Sao Hill* kwa ajili ya kiwanda chake cha kuzalisha plaiwudi kitakapojengwa na kufanya kazi. Ahadi hii ilizingatia uwezo wa shamba la miti wa kutoa malighafi na uwezo wa viwanda vilivyopo. Mwaka 2002/2003 kulikuwa na wavunaji 82 ambao kwa pamoja walikuwa na uwezo wa kuvuna mita za ujazo 239,873.6 ikilinganishwa na uwezo wa shamba wa kutoa mita za ujazo 602,475. Aidha, ilizingatiwa kuwa kama *RAIPLY* wataruhusiwa kuvuna mita za ujazo 100,000 za miti kwa mwaka katika Shamba la Miti la *Sao Hill,* kutakuwa

na salio la mita za ujazo 262,475 ambazo zinakidhi mahitaji ya Kiwanda cha Karatasi cha Mgololo.

(b) Ahadi waliyopewa *RAIPLY* haikuwa na muda wa mwisho ikizingatiwa kuwa Kiwanda cha Plaiwudi ni uwekezaji wa muda mrefu. Kama kitajengwa, kiwanda hicho kinategemewa kutumia miti ya Misindano aina ya *Pinus Patula* na *Pinus Elliottii* ambayo Shamba la Miti la *Sao Hill* lina uwezo wa kuzalisha kwa wastani wa mita za ujazo 450 kwa hekta moja. Hivyo, mita za ujazo 100,000 alizoahidiwa *RAIPLY* ni sawa na wastani wa hekta 222 kwa mwaka za shamba hilo.

(c) Maeneo ya Shamba la Miti la *Sao Hill* yanayovunwa na wavunaji wote yanapandwa miti upya na Serikali. Hivyo, *RAIPLY* haikupewa sharti la kata mti, panda mti. Serikali inapanda miti katika maeneo yaliyovunwa kutumia fedha za tozo ya *Logging Miscellaneous Deposit Account (LMDA)* ambazo wavunaji wote hulipa shilingi 3,400/= kwa kila mita moja ya ujazo inayovunwa.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu huu, Serikali imefanikiwa kupanda miti upya katika maeneo yaliyovunwa miti hekta 910 mwaka 1999/2000, hekta 503 mwaka 2000/2001, hekta 1,289 mwaka 2001/2002 na hekta 1,484.7 kwa mwaka 2002/2003 katika shamba hili. Aidha, hekta 158 zimepandwa miti kwa mwaka 2002/2003 katika maeneo mapya ambayo hayajawahi kupandwa miti. Hivyo kwa utaratibu huu, mwekezaji huyo hawezi kutuachia jangwa.

Hata hivyo, pamoja na utaratibu wa *LMDA, RAIPLY* walifahamishwa kuwa Wizara itaendelea kujadiliana nao kuhusu upandaji miti.

Na. 44

**Mti wa Ajabu katika Kijiji cha Runzewe**

**MHE. ROBERT K. MASHALA** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ina vivutio vingi vya utalii ikiwemo milima, mbuga za wanyama, maziwa na kadhalika; na kwa kuwa Serikali inatambua kuwepo mti wa ajabu kwenye Kijiji cha Runzewe Wilayani Bukombe na watafiti wamefika pale kwenye eneo hilo:-

(a) Je, ni nini matokeo ya utafiti huo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuuandalia mazingira mazuri na salama mti huo ili uwe kumbukumbu na kivutio cha watalii nchini?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Robert Mashala, Mbunge wa Bukombe, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali haina

taarifa za kisayansi juu ya kuwepo kwa mti wa ajabu kwenye Kijiji cha Runzewe, Wilayani Bukombe. Wananchi wa Kijiji hicho ndio wanaodai kuwepo kwa mti wa ajabu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata taarifa za kuwepo kwa mti unaodaiwa kuwa wa ajabu katika Kijiji cha Runzewe, Serikali ilituma wataalam wake kutoka Kitivo cha Misitu na Hifadhi ya Mazingira, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwenda Kijijini hapo na kufanya utafiti kuhusu mti huo kuanzia tarehe 18 hadi 31 Juni, 1999. Taarifa kamili ya utafiti huo inapatikana Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Robert Mashala, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu ya (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utafiti kuhusu mti huu unaonyesha kuwa siyo mti wa ajabu kama inavyodhaniwa. Mti huu unajulikana kisayansi kama *Blighia Unijugata* na kwa kiswahili unaitwa Mkivule au Mwakamwatu. Miti hii inapatikana maeneo ya Magharibi, Kati, Mashariki na Kusini mwa Bara la Afrika. Hapa Tanzania unapatikana katika Msitu wa Hifadhi wa Rubya, Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, Milima ya Usambara, Songea na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, miti huu ulipelekwa Kijijini Runzewe mwaka 1932 na Mtemi Muhelezi kutoka Kigoma, hivyo siyo wa asili katika eneo hilo. Mti huu una tabia ya kuota maeneo yenye vichuguu vya mchwa na utafiti zaidi unahitajika kupata sababu za ushirikiano wa mti huu na mchwa. Mti wa aina hii una jinsia ya kike na kiume, hivyo inahitajika miti ya jinsia zote ili kizazi chake kiweze kuendelea. Jinsia ya mti uliopo Kijijini Runzewe haijatambulika mpaka hapo utafiti utakapokamilika. Mti huu umeota machipukizi mengi kutoka kwenye mizizi yake na hutengeneza msitu mdogo kuzunguka chanzo cha maji ambacho kinatumiwa na zaidi ya wananchi 20,000 wa Kijiji hicho. Mkivule unafaa kupandwa kwenye vyanzo vya maji na kwa kivuli.

(b) Mheshimiwa Spika, mti huu kwa sasa unalindwa na asasi na visasili *(myths)* vilivyowekwa na aliyekuwa Mtemi wa eneo hilo, Muhelezi Lwasa ambaye ndiye aliyeupanda. Serikali inawapongeza wananchi wa Runzewe kwa kuulinda mti huo katika misingi aliyoweka Mtemi Muhelezi Lwasa na inahimiza waendelee kuulinda ili waendelee kupata maji ambayo chanzo chake kinahifadhiwa na mti huu. Aidha, Serikali inawahimiza wananchi wa Kijiji hicho wapande Mkivule zaidi katika eneo hilo ili waendelee kuhifadhi chanzo hicho cha maji ambacho ni muhimu kwa maisha yao. Hata hivyo, kwa kuwa miti ya aina hii ipo mingi nchini na siyo ya ajabu, hakuna haja ya kuuandalia mti huu mazingira ya kuwa kivutio cha watalii.

**SPIKA:** Ahsante. Mwuliza swali la msingi ameridhika na muda wa maswali umekwisha kwa hiyo tunaendelea na shughuli nyingine.

Kwanza kabisa, ningependa nimkaribishe tena Bungeni mwenzetu ambaye amekuwa mgonjwa kwa muda mrefu na hatukuwa naye hapa, leo amerudi Bungeni naye ni Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Bujiku Sakila. *(Makofi)*

Matangazo ya Vikao vya Kamati kwa leo. Kwanza, ni Kamati ya Huduma za Jamii, Mwenyekiti, Mheshimiwa Omar Kwaangw', anaomba Wajumbe wake wakutane saa tano asubuhi kwenye chumba cha Kamati Na. 231, Kamati ya Huduma za Jamii.

Kamati ya pili ni Kamati ya Maliasili na Mazingira, Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, anaomba wajumbe wa Kamati wakutane kupitia ule Muswada wa *Fisheries* saa tano hiyo hiyo katika chumba Na. 428, ghorofa ya nne.

Tangazo kwa Wabunge wanamichezo, Katibu wa Umoja wa Wanamichezo wa Bunge anasema mazoezi yanaanza tarehe 7 Novemba, 2003, kesho kama kawaida kuanzia saa kumi na mbili hadi saa moja asubuhi kila siku.

Taarifa kutoka kwa Kamishna wa Maadili anawakumbusha Wabunge kwamba ile kazi ya kila mwaka ya kujaza fomu wakati wake umefika na fomu ameshaziwasilisha kwa Katibu wa Bunge na zinatakiwa zijazwe na kurejeshwa kabla ya tarehe 31 Desemba, 2003. Kwa hiyo, nawakumbusha Waheshimiwa Wabunge juu ya wajibu huo. Mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper.*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kuunda Chombo cha Majadiliano ya Utatuzi wa Migogoro ya Kikazi katika Sekta ya Utumishi wa Umma wa Mwaka 2003
### *(The Public Service (Negotiating Machinery) Bill, 2003)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Majadiliano ya pamoja katika Utumishi wa Umma *(The Public Service (Negotiating Machinery) Bill, 2003),* sasa usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, akisaidiwa na Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri iliyotupatia wakati wa kujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Vyama Huru vya Wafanyakazi chini ya Shirikisho lao la Vyama Huru vya Wafanyakazi hapa nchini *(TUKTA)* inayoongozwa na Mama Margareth Sitta, pamoja na Jumuiya ya Serikali za Mitaa *(ALART)* chini ya Mzee Siovelwa, kwa ushirikiano wao mzuri na maoni yao ambayo yamechangia kuuboresha Muswada huu.

Aidha, napenda kumshukuru Mwakilishi wa Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* nchini kwa ushirikiano na kutupa uzoefu wake wa Kimataifa katika masuala ya majadiliano ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia nafasi hii, naomba pia kumshukuru na kumpongeza Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Makatibu Wakuu wa Wizara za Afya, Elimu na Utamaduni, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Makatibu wa Tume za Utumishi wa Walimu, Tume ya Utumishi wa Serikali Kuu na Tume ya Utumishi wa Serikali za Mitaa kwa ushiriki na michango yao pamoja na wataalam wetu wote.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni mojawapo ya hatua mbalimbali ambazo Serikali inachukua kwa madhumuni ya kutekeleza Sera ya Chama cha Mapinduzi. Katika Ibara ya 89(1) ya Ilani ya Uchaguzi, Chama cha Mapinduzi kilidhamiria kwamba nanukuu: "Kitahakikisha kuwa demokrasia inapewa kipaumbele katika Taifa letu hata kama ni ya ghali."

Aidha, CCM inabainisha katika Ibara ya 92 ya sera zake katika miaka ya 2000 - 2010 kwamba kutokana na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii yanayoendelea suala la ushirikishwaji wa wafanyakazi sasa litakuwa la kisheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanya jitihada za kupata maoni ya wadau wote kwa lengo la kuuboresha Muswada huu na pia kama njia mojawapo ya ushirikishwaji wadau katika kufikia maamuzi ya pamoja yalifanyika majadiliano ya pamoja baina ya wataalam wa Ofisi yangu na uongozi wa Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi Tanzania *(TUKTA).* Aidha, mazungumzo kama haya yalifanyika na viongozi wakuu wa Vyama Huru vya Wafanyakazi vyenye wanachama katika utumishi wa umma ambapo ni Chama cha Walimu Tanzania, *TUGHE, TALGWU* na *RAAWU.*

Mheshimiwa Spika, mikutano hiyo inaashiria kuanza kwa majadiliano ambayo ndio madhumuni makubwa ya Muswada huu. Katika majadiliano hayo tuliweza kufikia muafaka katika maeneo mengi na pia kutofikia muafaka katika baadhi ya maeneo kama nitakavyoeleza hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miongo miwili iliyopita yamekuwepo mabadiliko mengi ya kiuchumi na kijamii si tu katika Taifa letu bali duniani kote. Sekta ya utumishi wa umma pia inaendelea kufanyiwa marekebisho kwa madhumuni ya kuongeza tija na ubora wa huduma zinatolewa kwa wananchi.

Katika kutekeleza mabadiliko haya Serikali ilitunga Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 ambayo utekelezaji wake ulianza tarehe 1 Julai 2002. Sheria hii imepeleka mamlaka ya maamuzi ya masuala ya kiutumishi katika kila ngazi ya utendaji na usimamizi. Hapo hapo, sheria hii imeweka utaratibu wa kuunganisha makundi ya utumishi katika masuala ya kanuni na maslahi na sheria ili Taifa liwe na utumishi wa umma uliounganishwa au *unified service* katika nyanja zote.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni mwendelezo wa hatua na juhudi za Serikali za kujenga utaratibu thabiti wa kuwa na utumishi wa umma unaoendeshwa kwa majadiliano na maelewano kati ya watumishi na wasimamizi wao ili kuleta utulivu kazini

na kupunguza migogoro hivyo unaongeza tija na ubora wa huduma zinazotolewa kwa wananchi na wateja wote.

Utaratibu wa majadiliano uliomo katika Muswada unatoa fursa kwa wawakilishi wa wafanyakazi na wasimamizi wao yaani management kujadiliana kuhusu masuala ya uendeshaji, masuala ya tija, masuala ya huduma kwa wateja, masuala ya kitaalam na maslahi na kufikia maafikiano ambayo yanaweza kuidhinishwa na kusajiliwa kama makubaliano ya pamoja. Pale ambapo hawajafikia muafaka Muswada unaelekeza hatua za kuendelea na majadiliano na hatimaye kufikia maamuzi kwa ngazi za juu zaidi. Iwapo makubaliano hayatafikiwa kabisa, Muswada unaweka utaratibu ambao wafanyakazi wanaweza kuitisha mgomo lakini hili halitarajiwi kutokea mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, ili kwenda na mabadiliko haya, wafanyakazi kupitia vyama vyao wamekuwa wakidai utaratibu mzuri wa majadiliano. Aidha, Serikali imeridhia mikataba ya Kimataifa maarufu kama *Geneva Convention* ya mwaka 1948 ambayo inasisitiza umuhimu wa wafanyakazi kujadiliana na waajiri wao au *collective bargaining.*

Hivyo basi kutungwa kwa sheria hii ya majadiliano ya pamoja katika utumishi wa umma kuna lengo la kuweka msingi imara kwa watumishi wote wa umma ya kuwawezesha kujadiliana na Serikali kama mwajiri kuhusu maslahi, mazingira ya kazi na hivyo kuepusha migogoro na migongano katika maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa majadiliano ya pamoja katika utumishi wa Serikali kuu uliundwa mnamo mwaka 1962 kwa Sheria ya Majadiliano ya Pamoja inayojulikana kama *Civil Service Negotiating Machinery Act* Na. 52 ya mwaka 1962. Mnamo mwaka 1970, Serikali kupitia Waraka wa Rais Na.1 wa mwaka 1970 ilitoa agizo la kiutawala kuzitaka mamlaka zote za ajira kuunda Mabaraza ya Wafanyakazi katika sehemu za kazi. Aidha, mnamo mwaka 1963 ilitungwa Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika utumishi wa Serikali za Mitaa ambayo ilifanyiwa marekebisho baadaye mwaka 1982.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo pamekuwepo na mapungufu ambayo yamefanya mfumo tuliona nao sasa wa majadiliano ya pamoja kutokuwa na ufanisi. Kasoro hizo ni pamoja na kutoshirikisha baadhi ya makundi katika utumishi wa umma kama vile Walimu. Aidha, kwa makundi yaliyokuwa na chombo cha majadiliano kama vile Serikali za Mitaa vyombo hivyo vilikuwa havifanyi kazi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu huu na kama utakavyoona katika Muswada uliopo mbele yako lengo la Serikali ni kupanua wigo wa ushirikishwaji wa watumishi wa umma katika kufanya maamuzi kwa kuzingatia mabadiliko yanayoendelea katika Taifa letu kwa kuweka msingi wa kisheria kama Ilani ya Uchaguzi ambayo ndio dira ya maendeleo ya Taifa letu inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu ni mpya ukilinganishwa na mfumo tuliouzoea wa majadiliano ya pamoja kati ya mwajiri na mwajiriwa. Lengo na madhumuni ni kuhakikisha kuwa makundi yote ya watumishi chini ya sheria mpya ya utumishi wa umma yanakuwa na fursa ya kuwa na majadiliano na Serikali kwa masuala yanayohusu kila kundi la utumishi wa umma.

Hata hivyo, kwa kuwa utumishi wa umma ni mmoja sharti uwepo utaratibu wa kuwa na chombo kimoja cha kuainisha na kuidhinisha maamuzi na mapendekezo yote yanayotokana na majadiliano ya makundi mbalimbali ya utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma itakuwa ni chombo cha juu cha majadiliano na ushirikishwaji wa watumishi katika utumishi wa umma. Chombo hiki kitakuwa na jukumu la kujadili, kuidhinisha na kusajili makubaliano na itokeapo ulazima wa kurejesha mapendekezo ya Mabaraza ya makundi ya watumishi ili kuyatafakari zaidi kwa ngazi ya awali. Vile vile kitakuwa na jukumu la kujadili, kupendekeza na kuishauri Serikali katika masuala yanayohusu maslahi na masharti ya kazi ya watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kuundwa kwa Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma kunaenda sambamba na kuundwa kwa Mabaraza ya Majadiliano ya Pamoja kwa kila kundi la utumishi chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma. Mabaraza haya ambayo yatajulikana kama *Service Joints Staff Councils* yatakuwa na jukumu la kujadili, kushauri na kupendekeza Serikalini masuala yanayohusu maslahi na ustawi wa watumishi. Maamuzi ya Mabaraza haya yatawasilishwa kwenye Baraza la Majadiliano ya Pamoja ili kusajiliwa na kuidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Muswada ulio mbele yako unakusudia kuzifuta Sheria za Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Serikali Kuu Na.52 ya mwaka 1962 na Sheria ya Majadiliano ya Pamoja ya Watumishi wa Serikali za Mitaa Na.11 ya mwaka 1982.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unazo sehemu kuu sita. Sehemu ya kwanza inaonyesha masuala ya jumla ikiwemo tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada huu.

Sehemu ya pili inaanzisha chombo cha majadiliano ya pamoja baina ya Serikali na wafanyakazi wake. Aidha, utaona kwamba pamoja na kuwa na chombo hiki sheria inakusudia kutoa fursa kwa waajiri mbalimbali kuunda Mabaraza ya Majadiliano ya Pamoja ya kila kundi la utumishi chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya majadiliano ya masuala yanayohusu maslahi, mazingira ya kazi na taaluma ya kila kundi. Tumeafikiana kwamba Mabaraza hayo yatatajwa katika kifungu cha 4(1) cha Muswada huu.

Aidha, tumeafikiana kuongeza kifungu cha 4(4) kinachohusu wajumbe wa Baraza la Majadiliano kuwa na mamlaka kamili ya kufanya maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo katika sehemu ya pili ambayo hatukufikia muafaka katika majadiliano yetu kutokana na sababu za msingi. Eneo la kwanza ni kifungu 4(3) kinachohusu kundi lenye wanachama wengi zaidi kuwakilisha makundi yenye wanachama wachache. Hatukufikia muafaka kwa sababu kufanya hivyo ni kinyume cha msingi wa demokrasia ya uwakilishi ambapo hata wachache wana haki ya kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu inaonyesha utaratibu wa majadiliano na utoaji wa tuzo pale ambapo Serikali itafikia makubaliano na wafanyakazi kwa njia ya majadiliano ya pamoja. Sehemu hii pia inafafanua taratibu na hatua za kuchukuliwa pale ambapo upande mmoja hautaridhika. Katika sehemu hii hatukufikia muafaka kuhusu kifungu cha 23 ambacho kinampa Rais mamlaka ya kutoa tuzo. Hatukufikia muafaka kwa vile migogoro inayohusu maslahi ya wafanyakazi hupelekwa Mahakamani na Waziri. Hivyo hayumkiniki Waziri kurejeshewa maamuzi ya Mahakama kuyatolea uamuzi tena. Sababu ya pili ni kumpa fursa Rais atoe maamuzi ya mwisho iwapo maamuzi ya Mahakama yatasababisha kuvuka ukomo wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne, inapendekeza vipengele kuhusu migomo na kufungia viongozi nje ya ofisi na hata kufungia wafanyakazi nje ya ofisi. Pia yapo masharti yanayopaswa kutimizwa kabla ya kufanyika mgomo wowote na hili ni lazima kwa sababu tusingependa kuwa na migomo kila wakati.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano, inahusu uundwaji wa Baraza Kuu la Wafanyakazi, muundo wake pamoja na majukumu yake, mambo yanayohusu Katibu wa Baraza pia yameelezwa katika sehemu hii.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita, inampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya Utumishi wa Umma kutengeneza kanuni zitakazosimamia utekelezaji wa sheria hii. Aidha, kama nilivyoeleza awali sehemu hii inaonyesha kwamba sheria zinazosimamia majadiliano ya pamoja katika utumishi wa Serikali Kuu *(Civil Service Negotiating Machinery Act)* ya mwaka 1962 na Utumishi wa Serikali za Mitaa *(Local Government Service Negotiating Machinery Act)* ya mwaka 1982 zinafutwa.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa maelezo haya yatakuwa yameonyesha japo kwa muhtasari maeneo muhimu ya Muswada huu na kwamba yatasaidia kulifahamisha Bunge lako Tukufu nia ya Serikali kutunga sheria mpya ya majadiliano ya pamoja katika utumishi wa Umma ambayo kimsingi inalenga kuwashirikisha watumishi wake katika kutoa maamuzi kama njia mojawapo ya kuimarisha demokrasia na utawala bora katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kabla hajaitwa Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua Muswada huu, namwomba Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Simpasa anipokee.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE (k.n.y. MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawasilisha maoni ya Kamati yangu juu ya Muswada wa Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma wa mwaka 2003, kwa mujibu wa Kanuni Na.70(2) ya Kanuni za Bunge, napenda nieleze kwa ufupi hatua iliyotangulia kabla ya Kamati kuufikiria Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya utaratibu wa *public hearing* unaowezesha watu mbalimbali kuhudhuria vikao vya Kamati za Bunge na kutoa maoni yao, tarehe 27 hadi 28 Oktoba, 2003, Kamati yangu ilikutana na kupokea maoni ya wadau mbalimbali wa Muswada huu. Wadau walioshiriki ni wawakilishi kutoka *CWT, TUKTA, TUGHE, RAAWU, ALART* na *TALGWU.* Kamati yangu inawapongeza wadau hao kwa umakini waliouonyesha katika kuuchambua Muswada huu kwani maoni yao kwa kiasi kikubwa yameisaidia Kamati katika kuikamilisha kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati inaunga mkono na imeridhika na nia nzuri ya Serikali kuanzisha chombo kitakachosaidia kutatua migogoro katika sehemu ya kazi kwenye mfumo wa utumishi wa umma ili kuongeza ufanisi kwa manufaa ya nchi yetu. Hata hivyo, Kamati ina ushauri katika maeneo kadhaa ili kuuboresha zaidi Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na maoni ya jumla, Kamati inashauri kuwa kifungu Na.6 (6) cha Sheria Na.8 ya mwaka 2002 kilichofutwa kirejeshwe ili kuzipa Halmashauri mamlaka ya ajira badala ya mamlaka hayo kuachwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kuwa ndio mamlaka ya ajira badala ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sehemu ya Kwanza, Kamati inashauri kwamba kwa kuwa Mahakama inayohusika na utatuzi wa migogoro ya kikazi *(industry court)* ni vema tafsiri ya neno hilo iwekwe katika kifungu cha pili badala ya neno *court* kama ilivyo sasa.

Aidha, katika kifungu hicho cha pili, tafsiri ya *Service Scheme* iliyotajwa katika kifungu cha 4(1) pia itolewe. Pamoja na tafsiri hiyo sheria itaje *Service Scheme* hizo kama zilivyofafanuliwa katika Sheria Na.8 ya mwaka 2002 kuwa ni *Public Service Scheme, Civil Service Scheme, Local Government Service Scheme, Teacher Service Scheme, Health Service Scheme, Fire and Rescue Service Scheme.* Aidha, kiongezwe kifungu kipya cha 4(4) kitakachoweka sharti kwamba wajumbe wote watakaoshiriki vikao vya *service joint staff council* wawe ni wale wenye uwezo wa kutoa maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sehemu ya Pili ya Muswada, Kamati yangu inashauri kifungu cha 7(2) kifanyiwe marekebisho ili vikao vya *service joint staff council* viwe vinafanyika mara mbili kwa mwaka ili kurahisisha ufuatiliaji wa masuala yanayotolewa maamuzi na chombo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sehemu ya Tatu, Kamati inashauri kuwa maneno: *"such a manner as the Minister may think fit,"* yaliyomo katika kifungu cha 17(7) yafutwe na badala yake yawekwe *in the official gazette.* Kamati inaamini hii itasaidia kuharakisha utekelezaji wa maamuzi au tuzo zinazotolewa. Aidha, neno *may* lifutwe na badala yake liwekwe *shall* ili kitendo cha kutangaza tuzo zinazotolewa kiwe ni lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 23 Kamati ilijadili utaratibu unaowekwa wa maamuzi ya migogoro ya kazi kutolewa na Rais wa nchi badala ya Waziri mhusika kumpelekea ripoti kutoka Mahakama iliyosikiliza shauri hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Kamati ilikubali ufafanuzi uliotolewa na Waziri kuwa Rais ni mwajiri mkuu wa watumishi wote wa umma na kwamba maslahi ya wafanyakazi huchukua 35% ya matumizi ya Bajeti ya Serikali. Hivyo ni vizuri Rais akahusishwa katika masuala yanayohusu matumizi hayo. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba kifungu hiki kifanyiwe marekebisho kwani Mheshimiwa Rais tayari ana majukumu mengi na migogoro ya kikazi inahitaji kutolewa maamuzi haraka ili kuzuia athari zinazoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotamka awali ushauri wetu kwa kiasi kikubwa umezingatiwa na Serikali. Ni matumaini yangu kuwa yale ambayo sikuyagusia wajumbe wa Kamati hii na Waheshimiwa Wabunge watachangia watakapopata fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati. Pia nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi), Katibu Mkuu, Ndugu Joseph Rugumyamheto na wataalam wote walioshirikiana nao kwa maelezo ya kina na ufafanuzi walioutoa mbele ya Kamati. Aidha, niwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nawashukuru sana wajumbe wa Kamati yangu kwa kushiriki kikamilifu katika vikao na kutoa michango ya kina ambayo imewezesha Muswada kuwa katika sura ionekanayo sasa.

Wajumbe waliochambua Muswada huu ni hawa wafuatao, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Jenista Muhagama, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Ramadhani Khalfan, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Pascal Degera, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa

Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe na Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai bila kuwasahau Makatibu wa Kamati hii Ndugu Nenelwa Mwihambi na Ndugu Ernest Zulu, kwa kuihudumia vema Kamati hii na kutayarisha maoni wakati unaofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada huu.

Pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, kwa mchango wake katika Muswada huu na kukubali kufanya marekebisho kama yalivyoainishwa na wadau.

Vile vile nawashukuru watendaji wote katika Ofisi ya Mheshimiwa Waziri kwa kutoa ushirikiano bila kuwasahau Waheshimiwa Wabunge wote hasa wale walio kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa michango yao ambayo imewezesha Muswada huu kufika katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania baada ya kuridhia mkataba Na.87 wa mwaka 1948 kuhusu Uhuru wa Kujumuika na Kinga ya Haki ya Kupanga *(Freedom of Association and Protection of Rights to Organize)* na mkataba Na.98 wa mwaka 1949 kuhusu Haki ya Kupanga Majadiliano ya Pamoja *(Rights to Organize and Collective Bargaining)* utekelezaji wake unapaswa kuzingatiwa kama sehemu ya mikataba hiyo. Ili kuhakikisha utekelezaji wa mikataba hii, baadhi ya maoni kuhusu uhuru wa kujumuika na majadiliano ya pamoja yanawasilishwa na Kambi ya Upinzani ili Mheshimiwa Waziri aweze kuyafanyia marekebisho kabla Bunge letu halijapitisha Muswada huu kuwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu na ibara tofauti katika Muswada huu umetumia maneno *Chairman* na *Vice Chairman* hivyo kutoa upendeleo kwa jinsia moja na kuinyima haki jinsia nyingine. Kambi ya Upinzani inamshauri Mheshimiwa Waziri atumie maneno ambayo yatakubalika kimaana na jinsia zote katika sheria hii. Ili kuondoa utata wa kisheria unaoweza kujitokeza maneno kama *Chairperson* na *Chair* yanapendekezwa yatumike kwenye sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu, Ibara ya 17(1) kuhusu zawadi zote kutolewa na Mheshimiwa Rais, kutokana na majukumu mengi aliyonayo Mheshimiwa Rais, Kambi ya Upinzani inaonelea na inapendekeza kifungu kinachomhusu Mheshimiwa Rais kiondolewe na badala yake kazi hii ifanywe na Mheshimiwa Waziri kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anatekeleza majukumu yake kwa niaba ya Mheshimiwa Rais hivyo lolote alitendalo Mheshimiwa Waziri kwa njia moja au nyingine limepata baraka za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne, Ibara ya 20(1) inayohusu mambo yanayotakiwa kutimizwa ili mgomo uwepo, Mheshimiwa Waziri mgomo kwa watumishi wa umma ni haki yao na inatokana na migogoro ya kazi lakini kuna makundi ya utumishi wa umma yamenyimwa haki yao ya kugoma. Makundi haya ni waajiriwa walio katika huduma muhimu na waajiriwa wa kada ya chini walio katika huduma muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri watoe haki mbadala kwa waajiriwa wa umma kwenye *special service* kama fidia kwa kuwanyima haki yao ya kushiriki kwenye mgomo. Vile vile sheria ieleze bayana ni kundi gani la waajiriwa linakuwa kwenye tabaka la *special service.* Mheshimiwa Waziri kwa kuwapatia waajiriwa wote haki inayolingana kuhusiana na utatuzi wa masuala yanayohusu utendaji wa kazi kila siku litazidisha tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya kawaida ambapo Vyama vya Wafanyakazi vinapewa mamlaka ya kusimamia masuala ya waajiriwa ingawa ni halali kama sheria hii inavyosema na taratibu zifuatazo zinatakiwa zifuatwe ili kukinga *safe guard* isitokee bila sababu za msingi.

(a) Kunapaswa kuwepo na mgogoro au malalamiko.

(b) Mgogoro au malalamiko yasiyotatuliwa katika muda uliowekwa maalum.

(c) Mgorogoro uliokwishatangazwa na unasimamiwa na Afisa wa kazi na unaungwa mkono na waajiriwa walio wengi.

(d) Taarifa ya siku 30 imetolewa na Chama cha Wafanyakazi kwa Serikali kuhusu nia ya kugoma na muda huo umekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 28(1)(a) kinapingana na kifungu cha 29(1) ambacho kinampa mwajiriwa haki ya kushiriki kugoma. Hivyo Kambi ya Upinzani inamshauri Mheshimiwa Waziri afute kifungu cha 28(1)(a) na (b) ambacho kinawanyang’anya haki waajiriwa waliokwishapewa na kifungu nilichokieleza hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kwanza na mimi nitoe maoni yangu kwenye Muswada huu. Muswada huu mimi nauunga mkono moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina maoni pengine ni binafsi nilivyouona Muswada huu. Mimi naona kwamba Muswada huu upo upande wa kujihami zaidi kati ya Serikali na wafanyakazi. Muswada huu naona unawabana sana watumishi kwamba wasiwe huru sana kutoa maoni yao. Lakini mimi nadhani Miswada ya namna hii haiwezi kusaidia sana kuleta mabadiliko ya ufanikishaji wa utendaji kazi katika nchi yetu. Iko haja ya wafanyakazi waelewe kwa nini wapo pale na sheria zetu ziwalenge wafanyakazi

kwa kuwafanya wafahamu kwa nini wameajiriwa na wajibu wao ni nini ili wawajibike kuleta mafanikio. Hili nadhani lingetusaidia sana kuliko hivi sheria inavyoeleza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ingeelekeza wajibu wa watumishi kwa mwajiri na mwajiri kwa watumishi. Lakini hapa inaonekana Serikali inajihami tu wasifanye hivi, wasifanye migomo na nini lakini imeacha kuwaambia wao wenyewe watambue wanawajibika vipi kwa Serikali na umma uliowaajiri. Imekuwa ni tabia ya nchi hii mtu akishaajiriwa na Serikali basi kazi yake ni kunyamaza tu kudai haki, bila kutekeleza wajibu na matokeo yake ndiyo haya unakuta mfanyakazi anafika asubuhi saa mbili, saa tatu amekwenda kutafuta mikate ya kunywea chai saa nne. Maana anajua hana tatizo hata asipokuja kazini anajua yeye atapata mshahara wake upo pale, hataki kuwajibika na hapa ndipo wenzetu wakoloni walipotushinda, maana wao ukiingia kazini lazima utekeleze kazi ile, masuala ya huko nje hayapo. Lakini hii sheria ikiwa hivi masuala ya wafanyakazi kuhudhuria vilio, kwenda kuhani yatakuwa ni kawaida. Maana haionyeshwi popote pale kwamba kuna uzito na ndiyo maana hata huu Mkataba wa watumishi kwa wateja si rahisi kutekelezeka kwa sababu wafanyakazi hawajapewa wajibu wao waelewe ni vipi wafanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro hutokea wakati watumishi wanadhani hawapati haki zao kulingana na kazi zao wanazofanya. Serikali inapoona watumishi hawatekelezi wajibu wao kama inavyohitaji ndipo inapowashutumu na kutoa adhabu pengine ya kuwadhalilisha. Sasa hapa hatuwezi sheria inavyosema mazungumzo, unafanya mjadala gani hapa wakati mtu hafanyi kazi, hatekelezi yale yanayotakiwa, leo unasema mjadala wa haki yake wa nini?

Wenzetu wa Uholanzi walipokuwa wananyang’anya bahari ardhi, wao waliamua yeyote anayeishi pale lazima kwanza aache kuvuta sigara, kunywa pombe mpaka watakapomaliza shughuli hizo za kuinyang’anya bahari ardhi na walifanikiwa na hakuna yeyote aliyefanya kinyume cha hayo. Lakini sasa sisi tunaweka sheria katika sehemu nyingine bila misingi ya kuwajenga hawa wanaoajiriwa wafanye nini, hili ndilo tatizo tulilo nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani Serikali hapa katika kifungu hiki ingeweza kuorodhesha vipengele kuhusu hivi vikundi ambavyo vinaunda Baraza hili kwa mfano, *Civil Service Joint Staff Council, Local Government Joint Staff Council, Teachers Service Joint Staff Council, Health Service Joint Staff Council* na *Fire and Rescue Service Joint Staff Council,* ziorodheshwe kuwa hizi zinatambulika na zifanye shughuli za kuwaendeleza wafanyakazi wao wajue kwamba maisha yao yanategemea kazi wanazozifanya, ndipo katika kikao cha Baraza lao kuu wajadiliane wanafanikisha vipi.

Kwa mfano, watu wa afya wanafanikisha vipi masuala ya afya, wana matatizo gani na haya wanapoyaleta kwenye Baraza yaweze kuonekana na kuzungumzwa kufikia muafaka. Lakini hii ya kuleta migogoro inatokana na watu kuona kwamba pengine wanahitaji malipo zaidi na hii ni ubinadamu mtu kuhitaji zaidi kuliko ambacho hastahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vikundi hivi vikikaa katika maeneo yao ndivyo vingejadili viweze kufikia makubaliano na kupata uamuzi ambao wataupeleka kwenye Baraza la Wote kama lilivyoainishwa katika sheria hii. Hilo litaweza kutuletea manufaa na kwamba matatizo haya ya migogoro hayawezi kutatulika kwa kuwapa tu watu upande mmoja nafasi ya kutoa uamuzi au kutoa manufaa yao wanayotaka kwa sababu migogoro hasa inatokana na upendeleo kwa baadhi ya watumishi ambao waziwazi wanaeleweka hawafanyi kazi ya kuridhisha. Lakini unakuta huyo huyo amepata nafasi na kufikiriwa kupata *promotion,* anapandishwa daraja mtu ambaye kila mmoja pale anajua kuwa huyu kwa kweli hastahili. Sasa migogoro hapo itaonekana.

Sasa sheria hii haimbani huyu anayesababisha migogoro kwa manufaa yake huyu haionyeshi hapa. Kwa hiyo, hatutasaidia kuepusha migogoro kikazi kama hatutazingatia hili, haitawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatakiwa kwa kweli waonyeshwe uwajibiko wa kila mfanyakazi, asiyetekeleza basi huyo Kamati zao zile zile zimalize masuala yake kuwa wewe hujatimiza hili ambalo ndilo msingi wa kazi yako. Kwa hiyo, asiwe na haki ya kuwa anazungumza, mtu asiyetekeleza wajibu wake anazungumza na nani?

Kamati hizi zipo tano, zifanye kazi kwenye vikundi vyao, walimu wajadiliane kwa walimu wasiotii utaratibu, mwalimu yupo pale hafundishi, anakunywa pombe, wajadiliane kwenye sehemu yao, wamalizane huko kabla ya kuleta huku kwenye mambo mengine na kama anapendelewa na ndiye huyo hafanyi kazi kwa vyovyote ataleta chuki kati ya wafanyakazi wengine, hamtaweza kufanikisha. Kwa hiyo, hili nilikuwa nadhani ni vema likaangaliwa kwa hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hapa nadhani ni elimu zenye kuwawezesha watumishi kujua namna ya kuwajibika kikazi. Jana Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo alikuwa anatwambia kwamba wapo Watanzania huko Botswana ndiyo waangalizi wa mifugo kule na wanafanikisha sana, lakini hawa hawa watu hapa hawafanyi kazi, hatuna mwongozo wa sheria unaowapa nguvu na kulinda haki zao katika kazi. Sheria zetu ziwe zinaonyesha haki ya mtu anayefanya kazi, anafikiriwa vipi na anaangaliwa vipi, ndipo tutajenga nguvu ya mafanikio ya kazi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kazi ya Baraza iwe ni kudhibiti haki kwa sehemu zote kwa mwajiri vile vile na kwa mtumishi mwenyewe. Kwa namna hii nadhani kwenye kifungu kile cha sita cha sheria ni vizuri wakaongeza kifungu cha (e), kwamba wafanyakazi wanaelimishwa na kujua wajibu wao ili waweze kutoa michango inayokubalika na yenye msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tuzo, mimi nadhani tunampa Rais matatizo bure tu bila sababu. Waziri ameteuliwa na Rais ili amwakilishe, hivi Rais huyu tukisema kweli aje atoe tuzo ana mambo mangapi.

Kwa hiyo, tuzo hizi zitachelewa tu na kusababisha manung'uniko kwa watu waliofanya kazi kwa juhudi zote na moyo. Iwe ni kazi ya Waziri anapoona tuzo hii

imekwishaamuliwa na Baraza limeridhika, aende kumweleza Rais hata kwa muda ambao si wa kikazi, amweleze afahamu halafu yeye atamke kwa niaba ya Rais. Hili nadhani halina tatizo, tusiongeze makaratasi mengi tu na kazi ambayo haitatusaidia wala kuleta manufaa yoyote hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani tukifanya hivi tutakuwa tumepunguza mradi tu hizi Kamati za kila kikundi ziaminike, ziteuliwe, zieleweke na wajumbe wachaguliwe huko huko na vikundi vyao katika misingi inayoeleweka na kuaminika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Naomba nianze na kuipongeza kwanza Serikali kwa kukubali kuanzisha chombo hiki cha majadiliano ambacho kinawapa wafanyakazi nafasi ya kuongea na mwajiri. Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa wakati wake huu kuweza kulivalia njuga hili na chombo hiki kuanza. Mheshimiwa Waziri Nagu tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa mtumishi chombo hiki tulikiomba tangu mwaka 1996. Tumekuwa tukihangaika na Serikali ilionyesha kutokuwa na nia ya kutusaidia, lakini kwa nguvu zako Mheshimiwa Waziri nafikiri na wewe ni wa aina yake, umetuwezesha kutusaidia tumeweza kufikia hapo kwani ilifikia mahali tulitaka kukata tamaa. Chombo hiki ni muhimu sana kwa watumishi na kwa Serikali na hasa kupunguza migogoro. Chombo hiki tunategemea Serikali sasa itakiheshimu au waajiri wote wataheshimu chombo hiki kwa kweli kinaleta matumaini japokuwa nilipokuwa nasoma Muswada nimejaribu kuangalia kwa undani sana kama alivyosema msemaji aliyetangulia inaelekea katika kujihami, nafikiri tutaendelea kuboresha. Lakini ni vema kama ni majadiliano chombo hiki kielekee kwenye majadiliano mtumishi awe na nafasi ya kuweza kueleza matatizo yake na mwajiri vile vile kuwe na sehemu ambayo anaonekana kwamba anawajibika. Maana yake inaelekea kwamba mtumishi atawajibishwa kama hatatimiza wajibu wake lakini mwajiri je, huyu ambaye hatimizi wajibu wake?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema tungeanza kuangalia kwamba mwajiri anawajibika vipi kwa mtumishi wake au anachukuliwa hatua zipi. Nitatoa mfano kwa baadhi ya mambo ambayo yanajitokeza wakati mwingine yanakatisha tamaa watumishi na ndiyo maana wamekuwa wakiomba chombo hiki. Tuna imani labda yataanza kupungua hasa kama kungekuwa na kipengele cha kwamba mwajiri anatakiwa na yeye kuwajibika inapoonekana kwamba hatimizi wajibu ikiwezekana analipa riba anaposhindwa kumtimizia haki mtumishi wake.

Kwa mfano, nitachukua kundi dogo tu la watumishi kwa mfano walimu katika Mkoa wa Mwanza, Wilaya ya Magu wanadai milioni 101, Wilaya ya Sengerema wanadai milioni 187, Wilaya ya Misungwi wanadai milioni 169, Wilaya ya Ukerewe wanadai milioni 67, Wilaya za Jiji wanadai milioni 86, Wilaya ya Geita wanadai milioni 380 na Wilaya ya Kwimba wanadai milioni 166.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mwanza unadai karibu bilioni moja. Tukichukulia Wilaya ya Geita, mishahara ya walimu wapya wanadai milioni 35, mapunjo ya mshahara milioni 51, *disturbance allowance* milioni 15, *subsistence allowance* milioni 186, likizo milioni 19, matibabu milioni 30, walio masomoni wanadai milioni karibu 41. Sasa hapa hawatendewi haki ni kwamba ni wapi waweze kupeleka malalamiko yao chombo hiki nafikiri kinaweza kuwasaidia, ndiyo mawazo yangu yanavyofikiria kwamba kitawasaidia.

Sasa huyu mwajiri ambaye hakuwajibika anatoa fidia gani au nyongeza kwa sababu fedha inashuka kila siku, anawajibika vipi, hii nilitarajia katika chombo cha majadiliano suala kama hili lingewekwa kama halipo basi litafutiwe chombo, mwajiri na yeye awajibike, tusiangalie upande mmoja kumwambia acha kugoma au kufanya nini. Hapo tutakwenda lakini hatua tuliyofikia mimi nampongeza Waziri kwa kweli amefanya kazi nzuri na tunakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye Muswada kuna baadhi ya vipengele ambavyo vimetajwa lakini nilikuwa nafikiri labda vingewekewa mkazo zaidi kwa mfano aya ya nne, kipengele cha kwanza, ukurasa wa tano, hizi *departments* ambazo zimetajwa kwenye aya zitajwe siyo kutu-*refer* kwenye sheria namba nane ya mwaka 2002.

Kwanza ile sheria siyo *negotiation machinery,* hiyo inazungumza kabisa jambo inatuambia lakini kitu tofauti, hizi zitajwe hapa kwani kuna tatizo gani? Mimi niliingia kwenye Kamati kama msikilizaji, nafikiri walikubaliana kwamba zitajwe, Mwenyekiti nashukuru amesema zitajwe. Lakini mimi nafikiri zitajwe kwa lugha ifuatayo, *Civil Service Negotiating Machinery, Local Government Negotiating Machinery, Teachers Service Negotiating Machinery,* hili neno liwepo, zitajwe, zipo tano. Tusiwa-*treat* kama ni kitu kimoja hawa watu ni tofauti, walimu wana matatizo yao, waganga wana matatizo yao na labda hawa watu wa *fire* nao wana matatizo yao. Mwalimu anaweza kudai labda *overtime allowance,* mganga akadai *call allowance,* sasa wakati wa kudai ni vizuri wawe wazi hawa watu katika makundi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuoni ugumu kwa nini wasiweke kitu hiki au katika kifungu hicho hicho Waziri amelizungumzia *the most represented Trade Union.* Mimi nashawishika kwamba hili neno ni vema waliweke kwa sababu tunapokwenda, kwa mfano tuchukue Chama cha Walimu, kinaweza kufikia mahali kikagawanyika kwa sababu sheria inaruhusu wakishafika watumishi ishirini tayari wanaweza kuanzisha *Trade Union* yoyote ile.

Kwa hiyo, mnaweza kuchukua Chama cha Walimu cha Kariakoo kwamba kinawakilisha wengine wote wale wa nchi nzima, mkachukua wawakilishi wawili tu. Sasa mawazo yangu ni kwamba tuchukue wale walio wengi, amesema kwamba hata wachache wana haki, ndiyo wana haki lakini nafikiri *majority* wanakuwa ni *sample* nzuri zaidi kuliko kuchukua mtu mmoja. Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Waziri aliangalie mara mbili ili aturekebishie angalau nyoyo zetu zisuuzike kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kipengele cha hapo hapo kifungu cha nne, kuna mahali kiongezwe kipengele cha *Members from both sides should have power to make decisions.* Tunasema wawakilishi wawe na uwezo wa kupitisha maamuzi siyo tuchukue wawakilishi ambao hawatakuwa na ile *mandate* ya kuamua ya kuja kushangaa shangaa kwenye ule mkutano kwa sababu wanazungumzia masuala ambayo ni *very sensitive.* Namwomba Waziri hicho kipengele kiongezwe, hakina gharama lakini ni muhimu sana kwa sababu tunafanya kitu, watu wanakwenda kufanya maamuzi siyo watu wanakwenda kule wanakaa, kifungu hiki kitawalinda kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala hili la kumpa mamlaka au mamlaka pekee kutoka kwa Rais ya uamuzi au kutoa *award.* Mimi nafikiri tusiende nalo kwa woga, Rais tunafahamu ni nani. Rais anaangalia kila kitu siyo kwamba anaangalia watumishi tu, nasema ndiyo mkuu wa watumishi wote, lakini vile vile ni mkuu wa wavuvi wote, vile vile ni mkuu wa wakulima wote, ni mkuu wa wafugaji wote, ni mkuu wa wawindaji wote, matatizo yote yanapelekwa kule, sasa wameteuliwa Mawaziri kuweza kufanya kazi hizo za ukuu ambazo yeye hazifanyi.

Sasa jamani huyu Rais huyu Mungu wangu hata huruma hamna jamani, rekebisheni sehemu hii angalau baadhi ya mambo ambayo lazima yaende kwa mfano kama fedha ime-*exceed* kiasi gani basi yaende kwake. Hii itasaidia kuondoa hii *red tapism* au ile *bureaucracy* ya kufanya mtu anakuwa anapiga chenga, anasema Rais hajatoa uamuzi kumbe yeye analo kwenye faili. Tumekuwa tukiona mengi, mtu anazunguka nalo kwenye faili halijapelekwa kwa Rais au haijafika kwa Rais, anazunguka hapa hapa tu. Anadanganya tunasubiri jibu la Rais, wakati bado hajapelekewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri mamlaka tuliyopewa naomba Bunge hili Tukufu likubali kwamba Rais atapelekewa majukumu ambayo yaliyochujwa labda yale ya mwisho mwisho lakini tusimpe kila kitu, atakuwa na tabu huyu, tutamwuguza sana, atapata tabu sana. Kuna kesi nyingi za walimu ambazo Miswada ilipitishwa kwamba lazima ziende kwa Rais, zipo kule zinasubiri mpaka zije kujibiwa sijui ni lini. Tungeomba kipengele hiki kwa kweli kirekebishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda katika kutengeneza Miswada hii naomba vile vile tujiangalie na sisi, tusifikiri kwamba tunawatengenezea watu wengine, tunajitengenezea wenyewe. Nashukuru Mheshimiwa Waziri ameliona hili ameleta hiki chombo lakini watu tuna *tendency* kwamba unatengeneza kitu kwa ajili ya watu wengine, unasahau kwamba mtoto wako atakuwa kwenye *system* hiyo hiyo baadaye na wewe utakuwa kwenye *system* hiyo. Tuna *experience* watu wengi wamekuwa kwenye *system* wametengeneza mipango ya ovyo ovyo, anapotoka anaaanza kuilaumu Serikali, tena anakuwa mkali kweli, kumbe yeye alikuwemo humo humo. Sasa mimi nafikiri kwa mwanya huu hebu tutengeneze hiki kitu kipendeze, kitawafaa watumishi, watumishi kwa kweli wananyanyasika kwa sababu hawana mahali pa kusemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya kusema hilo naomba kuunga mkono hoja hii lakini tutapenda kuona marekebisho wakati wa hitimisho la Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi angalau nichangie machache katika Muswada ulioko mbele yetu. Naomba nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake yote wakiongozwa na Katibu Mkuu.

Mimi ni mjumbe kwenye Kamati, kwa hiyo, kwanza niwashukuru kwamba mengi ya yale tuliyozungumza kwenye Kamati kwa kweli yamezingatiwa. Kwa hilo naomba niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuzingatia yale yaliyokuwa yametokana na Kamati napenda kuongelea mambo kadhaa. La kwanza ni dhana nzima ya *coordination* ya mfumo katika Serikali. Kwa bahati mbaya au nzuri mara tu baada ya kutoka kwenye kikao cha Kamati pamoja na Waziri na timu yake sisi wajumbe wa Kamati tukaenda kwenye semina nyingine inayoshughulikia *Labour Institution Act, 2003* ambayo jana imewasilishwa kwa mara ya kwanza Bungeni.

Sasa tatizo ninaloliona ni kwamba katika Miswada hii miwili *Public Service Negotiating Machinery* na *Labour Institutions Act, 2003,* sina hakika kama wenzangu wamesoma lakini kuna mawazo ambayo yanakinzana na kupingana na nilimwandikia Waziri kwamba ayatazame ili tusije tukapata mgongano baadaye kwenye sheria na nilisema kwamba nia yetu ni kuwa na sheria nzuri ambayo inaondoa migongano katika Taasisi au asasi mbalimbali zilizoko katika nchi yetu na kurahisisha utekelezaji. Sasa mimi nisingependa kuwa na sheria ambayo baadaye utekelezaji wake unakuwa ni mgumu na tumeshaona mambo ya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri tu haraka kwamba mambo ya namna hiyo ni vizuri Mheshimiwa Waziri atusaidie ili kuondoa sheria hizi zisije zikagongana na mambo mengine ni ya msingi.

Mimi sikujua na siku ile kwenye Kamati walitwambia kwa mfano hata tafsiri ya *Court* na Mheshimiwa Waziri akisaidiwa na mtaalam waka-*insist* kwamba kuna sheria inakuja ndiyo hatukujua kwamba mtu huyo yeye mwenyewe yupo kwenye ile Kamati nyingine na hatukujua kwamba hiyo *bill* kwa kweli ipo tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Waziri katika ufafanuzi akatueleza kwamba *The Industrial Court* inayozungumziwa katika sheria yake ni sehemu ya *Executive,* kwa hiyo mambo yake yangeishia kwenye *line* ya *Executive.*

Lakini tulipozungumziwa katika hii semina ya pili hii ni *proper Court* na ni *department* ya *division of High Court* kama ilivyo chini ya *Land Act* na kwa tafsiri tuliyopewa na kwa bahati nzuri kulikuwa na Majaji pale, kwa tafsiri tuliyopewa pale kitu kikishakwenda kwenye *Industrial Court* kwenye hiyo *Labour Court* hakirudi tena kwenye *Executive.* Kwa hiyo, ni dhana mbili ambazo zinaonekana kwamba zipo tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani ilikuwa ni muhimu sheria hii ikaainisha ni kitu gani *specifically* kiende katika hiyo *line* ya *Court* na kikitoka kule kisirudi tena kikaingia kwa Rais. Tulishapata kama ilivyotokea ile sheria ya nyuma Mahakama ikaamua kima cha chini cha mshahara kiwe kiasi gani ile *Industrial Court* kwa taratibu na sheria iliyoko lakini baadaye ikafika kwa Rais, Rais akaitengua.

Sasa huko mbele kwenye ile semina tahadhari hiyo pia ilitolewa, tusingependa migongano hiyo ili sheria iwe wazi toka mwanzo na tuwe na vitu viwili ambavyo vinaungana.

Kwa mfano, Jaji Mwaipopo alitusaidia sana pale akatupa vitu vya msingi ambavyo ningependa vingelioanishwa hata katika sheria hii. Sasa bahati nzuri au mbaya Kamati iliyotengeneza hii sina hakika kama baadaye wamekaa pamoja.

La pili, ambalo nilifikiri ni muhimu kulisema, ameshalisema Mwenyekiti wa Kamati yetu lakini napenda kulirudia, ni dhana nzima ya tafsiri. *Local Government,* inatajwa katika sehemu mbalimbali na sheria hii inazungumzia *Public Service Negotiating Machinery,* inazungumzia *employer* na mgogoro ni kati ya *employer* na *employee.* Sasa kwa kuwa kifungu cha 6(6) kiliondolewa, dhana nzima ya *employer* katika *Local Government* haikutafsiriwa tena. Kwa hiyo, hatujui mgogoro unapotokea katika *Local Government* ni mgogoro kati ya nani na nani. Huyu *employer* ni nani, ni *management* ya Utumishi wa Umma, ni Serikali Kuu kwa maana ya ile *Management* au Idara Kuu ya Utumishi tulivyozoea kuiita, ni nani huyu ambaye anakuwa na mgogoro au ni Mkurugenzi?

Kama ndiyo hivyo, sheria haitafsiri. Ni vizuri tukapata tafsiri na ndiyo maana tulisema Mheshimiwa Waziri angeturudishia kile kipengele haraka na tulitegemea anapoleta hii sheria, angeleta pia marekebisho ya Sheria Namba 8 ya mwaka 2002, iliyoondoa kifungu cha 6(6) katika ile sheria. Lakini bahati mbaya Mheshimiwa Waziri ameleta hii hakuleta yale marekebisho. Kwa hiyo, matokeo ni kwamba, tuna sheria hiyo inataja kwamba, kuna mgogoro katika *Local Government* na mgogoro ule utakapotokea, *the first problem* tutakayopata sasa hivi ni mgogoro unamhusu nani, ni Mkurugenzi, ni Madiwani pamoja na *Council* yao, kwa tafsiri ile iliyoko katika Sheria Namba 8 ya mwaka 1982 au ni nani? Hiyo Tafsiri haiko wazi na Mheshimiwa Waziri, nafikiri utatusaidia katika kuleta marekebisho hayo haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia haraka tu kwenye *interpretation,* Mheshimiwa Waziri, anatafsiri mambo mengine yote, anasema *Public Servant* ni nani, *has a meaning ascribed to it under the Public Service Act, 2002.* Hiyo *Public Service Act, 2002* ndiyo hiyo Namba 8 tunayoizungumza. Lakini hiyo imeondoa *Council* kama *employer,* imemweka Mkurugenzi. Sasa Mkurugenzi ni nani na tafsiri ya Mkurugenzi mwenyewe hapa haiwekwi? Kuna tafsiri *very vague* ya *grades* mbalimbali tena wakaweka kitu kingine cha ajabu. *Staff Grade Officer* kwa mfano, *means any public officer who holds or acts in any of the following offices: Permanent Secretary, Deputy Permanent Secretary,* wakawaorodhesha wale wengine wote na *Regional Administrative Secretary, Director and Commissioner,* sasa huyu *Director* ni nani, ni *DED* au ndiyo mtu

gani? Kwa hiyo, tunaanza kutengeneza mazingira ya mgogoro katika sheria hasa inapohusu sehemu kubwa ya waajiriwa katika *Public Service.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani idadi ya Watumishi katika *Local Government* kama siyo kubwa zaidi, inalingana na idadi katika Serikali Kuu. Sasa umeweka sheria, lakini haiwachukui sehemu kubwa ya Watanzania walioajiriwa na hatma yao inabaki haijulikani. Mimi, nina mfano wa mfanyakazi, yaani kuna mgogoro, lakini katika huo mgogoro unaenda wapi. Hata wao wanapokutana na Mkurugenzi wao, wana mgogoro na Mkurugenzi waende katika hatua zipi. Chini ya sheria iliyokuwepo ambayo inakuwa *repealed say* leo, sheria ya mwaka 1982, *at least* kulikuwa na *mechanism* pamoja na kwamba, haijawahi kutumika. Kwa nini haikutumika ni kwa sababu ya matatizo ya aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri, anajua kabisa na tulikwambia siku ile kwamba, tuna sheria tunayoiondoa ya mwaka 1982 haijawahi kufanya kazi hata siku moja, kwa sababu ya *contradictions* za namna hii. Tuna Sheria Cap.484 ya mwaka 1962, *Public Service Negotiating Machinery*, haijafanya kazi, miaka 30 baadaye kwa sababu ya migogoro ya namna hii. Kwa hiyo, tunapoyasema haya, hatuyasemi kwa nia mbaya, tunayasema kwa nia ya kwamba, tunataka sheria ambayo kweli ina lengo na nia ya kuweza kutusaidia katika nchi yetu tuwe na utulivu. *(Makofi)*

La tatu, ni dhana ambayo pia inajitokeza katika sheria zote mbili. Ni kweli katika sheria ya sasa mgogoro hasa unapohusu mshahara wa kima cha chini, una chombo kingine katika Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Lakini unapohusu maslahi ya wafanyakazi na hili swali halijapata jibu mahali popote. Kinachojitokeza sasa ni makundi na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri, anaijua kwa sababu atakuwa ameisoma, huku imeelezwa kabisa kwamba, sasa na *negotiation* ya mishahara itafanyika kisekta. Kwa hiyo, kila sekta kama ni Madini, wana uwezo wa kupanga mishahara yao katika *Trade Union* ya kisekta, labda Sekta ya Madini. Kwa hiyo, wale wengine walioko kwenye Kahawa na Chai watapanga ya kwao. Matokeo tutakayoyaona katika nchi hii ni kwamba, kuna watu watapata mishahara ya milioni moja kwenda juu na watu wengine watapata mishahara ya shilingi 5,000/=. Kwa mfano, kwangu mimi mashamba yote ya kahawa sasa hivi mishahara wanayopata pamoja na tangazo la Serikali imebaki kiwango cha shilingi 5,000/= na hakuna kitu ambacho Serikali inakifanya kwa sababu wale wanasema sisi ndiyo uwezo wetu, sasa tukifikia hapo Serikali haiweki misingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa kabisa na tulijibiwa pale na nashukuru hata Katibu Mkuu tulipomtembelea katika Ofisi yake alijibu. Lakini mimi siridhiki na maelezo hayo kwamba, lazima tutatofautiana, hakuna mwenye kubisha. Mwenye *Ph.D,* mwenye *Masters* na mwenye cheti cha darasa la saba, hakuna ubishi kwamba tutatofautiana, lakini tunatofautiana kwa viwango gani na kwa *ratio* gani? Nadhani tusipoangalia usemi wetu kwamba, Tanzania tuna mshikamano, tuna umoja na tunapendana, yote iliwezekana kwa sababu tulikuwa na sura fulani katika nchi na tulijenga huu mshikamano, sasa hivi kwa sheria hizi tunaanza kuubomoa. Mimi ninaomba na ninarudia tena kuiomba Serikali iangalie tofauti kubwa za mishahara katika Idara hasa za Serikali, ni lazima tuitafutie dawa, mimi sina jibu. Lakini hatutaruhusu

kabisa watu wengine wapate mshahara wa shilingi milioni mbili na wengine wapate mshahara wa shilingi 100,000/=, ni vigumu sana. Wote wana cheti kimoja kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wamemaliza mwaka mmoja, wana *qualification* za aina moja, halafu wanakwenda kufanyakazi, mmoja yupo Idara ya Serikali na mwingine yuko *Executive Agency,* chombo ambacho ni cha Serikali, tumekipitisha hapa Bungeni, mmoja anapata milioni mbili na mwingine anapata shilingi 100,000/=! Tutakuwa tunaruhusu kitu cha ajabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama Bunge hili linaweza likafika mahali likaruhusu vitu vya namna hiyo. Pamoja na maelezo mazuri ambayo wataalamu wanatupa, pamoja na maelezo mazuri kabisa kwamba, sasa hivi ni tija ndiyo inayo *determine* ni kitu gani tupate. Katiba yetu inasema Tanzania bado ni nchi ya Ujamaa na Kujitegemea, kama Mheshimiwa Waziri alivyokiri kwamba, tunatekeleza Ilani ya CCM na naomba tuitekeleze vizuri. Ilani ya CCM inajenga kwa upande fulani kwamba, lazima kuwe na mshikamano, lakini tusikubali kumomonyoa na mimi nakubali kwamba, hicho kipengele ni kizuri kwa sababu kinaleta umoja katika nchi yetu. Lakini ukishaanza kujenga mgawanyiko katika matabaka kwa Watanzania, tunaanza kuruhusu kitu ambacho hatukukidhamiria na siyo lengo la nia tuliyoijenga katika miaka 30, 40 iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo vilevile suala hili la kipengele cha Rais. Kipengele cha Rais pia kinanipa tatizo kubwa sana na ni kipengele cha 17 katika Sheria ya *Public Service Negotiating Machinery,* kinanipa matatizo kwa sababu kwanza, niseme kwamba, Mheshimiwa Mary Nagu, sasa hivi yuko ndani ya Ofisi ya Rais na kwa kweli yuko ndani ya Ofisi ya Rais na Menejimenti ya Umma iko ndani ya Ofisi ya Rais. Lakini sitegemei kwamba, siku zote itabaki ndani ya Ofisi ya Rais, kuna siku Wizara hii itakuwa nje itajitegemea kama ilivyowahi kuwa huko nyuma.

Lakini kama itajitegemea, *then* lengo langu na nia yangu kabisa ni kwamba, Mheshimiwa Waziri, anapofanya kazi kuna *collective responsibility,* kwa hiyo, mambo yote yanayoamuliwa ndani ya Serikali na hasa yanayohusu maslahi ya kifedha, kwa sababu *at the end of the day,* Rais ndiye anayegawa na Kikatiba Rais ndiye anayeamua ni kiwango gani cha fedha kitumike kwa mishahara, kwa hiyo, hilo sina tatizo. Lakini naamini kabisa kwamba, *process* itakuwa imekamilika kabla ya kufikia hatua hizi za migogoro na kama kuna mgogoro ambao unaweza kumalizika, *consultation* itakuwa imekwisha kufanyika kati ya Mheshimiwa Waziri mhusika na Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, tunapofikia kwenye hatua ya mgogoro turuhusu vile vyombo vijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mifano ya nchi nyingine, kwa mfano, Ulaya, ukichukua Ujerumani, ukichukua Italia, Italia ni nchi ambayo ina migogoro mikubwa sana kila wakati na hata sheria zetu ni *more limiting* bado. Lakini ukichukua nchi kama Italia, kuna kitu kinaitwa *Scala Mobile Italy,* ambacho kina-*determine* hata *level* ya mishahara *automatically* kwa kutumia labda *index* mbalimbali katika nchi. Uchumi unakua kwa kiwango gani na *inflation* imekua kwa kiwango gani, unachukua hiyo unakwenda na ile *scala mobile. Scala mobile* maana yake ni ile ukiwa *airport* pale inabeba watu inajipandisha yenyewe. Kwa hiyo, inapanda *automatically* kadri *index* zile

zinavyopanda. Sasa sitaki tuchukue haya ya wenzetu kwa sababu mazingira ni tofauti, lakini *machinery* yetu ni watu ambao tunaweza ku-*negotiate.*

Sasa tukimhusisha Rais katika hatua za mwisho, kitu kikifika kwa Rais, hakuna namna yoyote ya kumsukuma Rais. Ndiyo maana kesi za walimu, kesi za watumishi, zimefika katika Ofisi ya Rais, Rais hakupangiwa kipengele chochote, japo Mheshimiwa Waziri alisema kwamba, atarekebisha, kwenye marekebisho aliyoleta sikuiona kwamba, Rais ataandikiwa angalau isikae zaidi ya muda fulani, lakini hata ungemwandikia Rais, akikaa bila kulishughulikia unafanya nini? Mheshimiwa Waziri, unaweza kumsukuma lakini Rais huwezi kumsukuma, yeye ni *final.* Lakini hapa tunazungumzia haki ya wananchi, sasa unazungumzia haki ya Watanzania labda Watumishi, walimu zaidi 100,000 hawana haki zao, imekwenda *appeal* mpaka kwa Rais, imenyamaza kule, umekaa kimya, huna chombo chochote cha kumsukuma Rais, unafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kipengele hicho kiishie kwa Mheshimiwa Waziri na kule nyuma kwa sheria Namba 484 iliishia kwa Mheshimiwa Waziri. Kama tuliweza katika sheria ile tukaimalizia kwa Mheshimiwa Waziri, kwa nini leo tunamwingiza Rais, tumeshindwa kitu gani? Mimi nafikiri hapa ni vema tukapata ufafanuzi wa kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kuligusia ni kipengele cha 11(7) na kipengele cha 24. Katika Kipengele cha 11(7), mimi sipendi lugha inayotumika hapa na sikuiona kama imekuwa *amended* japo tuliisema. Ni kengele ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nichangie katika Muswada huu, ambao utaleta kuwepo na chombo cha majadiliano ya pamoja katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi napenda nimpongeze sana Waziri, Mheshimiwa Mary Nagu, kwa jinsi alivyoshughulikia masuala haya kwa uvumilivu kabisa, kwa kuhusisha kila aliyekuwa mdau na mpaka tukafikia siku ya leo kupata chombo kama hiki. Hii ni dalili ya kukomaa katika kuendesha Serikali na huu ndiyo Utawala Bora, kwa sababu Utawala Bora unaozungumzwa kila siku, kama hauendi kwenye vitendo inakuwa ni nadharia zinazotupotezea muda. Lakini hii imetafsiriwa kwa vitendo na Wizara hii na eneo hili ambalo analisimamia Mheshimiwa Mary Nagu, napenda nimpongeze. Niongeze kwamba, *this is the gender quality.* Kwa hiyo, ajisikie tu kwamba, mwenzetu anayewakilisha *gender* nyingine, ameifanya kazi ambayo italeta mapinduzi katika Utumishi katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, kuna wadau ambao ningependa niwataje tu, wao pia nimewaona wamesimama kidete na hasa nikiwa ni Mwalimu Mstaafu, napenda nimpongeze Rais wa Chama cha Walimu kwa sababu kazi hii Mama Margareth Sitta ameisimamia vizuri sana. Nilisoma naye Tabora akiwa *junior,* akiwa anaitwa Margareth Mwanza, sasa ni Margareth Sitta, amesimamia kidete

sana kutetea haki za walimu na nadhani kwa niaba ya Walimu wa Tanzania, ni vizuri nimpongeze pia kwa kazi hiyo nzuri anayoifanya na kwa ushirikiano ambao amempa Mheshimiwa Waziri wetu kuweza kufikia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ningependa tu niseme kwamba, sasa hivi sheria hii inakuja katika mazingira tofauti na yale tuliyoyazoea. Imekuja katika mazingira ambayo tunaanza kuona kupanuka kwa ajira ya sekta binafsi, ambayo ni ya humu humu nchini na ya Mashirika yanayotoka nje ya nchi. Sasa tusipokuwa na utaratibu unaompa nguvu mwajiriwa wa umma, tutakuwa tunamsononesha. Ukiangalia Watumishi wa Umma, wamekuwa ni watu wa kusononeka na watu wa kusumbuka katika kutafuta haki zao. Kwa hiyo, chombo hiki nina matumaini makubwa kwamba, kitawatoa katika hali hiyo, waweze na wao kuchangamka, kuweza kujua ni wapi wanapopeleka matatizo yao na nani ambaye atayashughulikia matatizo hayo ili wapunguziwe kero za kuhangaika wanapokuwa wanatafuta haki zao na kupoteza muda mwingi ambao wangeutumia katika kufanya kazi na kujipima na wenzao. Kwa sababu katika ajira binafsi, vitu vingi vinaonekana wazi, pamoja na mapungufu mengi ambayo tunategemea kwamba, baadaye Mheshimiwa Waziri, atayaangalia pia. Kwa sababu katika sekta binafsi pia kuna unyanyasaji wa hali ya juu kwa Watanzania wanaofanya kazi katika sekta binafsi, pamoja na kulipwa vizuri, lakini kuna haki nyingi za binadamu zinakiukwa katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti na hapa ningependa niseme labda ingawa siyo mahali pake, niseme kwa mfano, kwa upande wa akinamama sasa hivi walioajiriwa katika sekta binafsi, hata *maternity leave* wanaipata kwa shida, ambayo ni haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, pia ninapenda niseme kwamba, kuna vitu ambavyo wenzangu wamevizungumzia, nisingependa nivirudierudie nitawachosha, lakini nataka niongeze tu pale ambapo wenzangu wamesisitiza. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, aelewe kwamba, tunajaribu kuboresha tu wala haya yanayoongezwa hayapunguzi ubora ila yanaongeza ubora tu. Moja, ambalo limezungumziwa ni kwamba, yaainishwe kabisa makundi haya katika kifungu cha 4, izungumzwe kama ni kikundi cha Madaktari, kikundi cha Walimu na wafanyakazi wengine. Kwa sheria zetu mtu anapokwenda kuhukumu analeta utata, kwa sababu tu kitu hakikukaa wazi, kwa hiyo, hiki Mheshimiwa Waziri hakitapunguza ubora wa Muswada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limesemwa na wenzangu ni hili la kumpelekea Mheshimiwa Rais na kumlundikia kazi. Nadhani nalo siyo baya, kama Mheshimiwa Waziri, ameweza kuleta Muswada huu, atashindwaje kutoa *award?* Kwa hiyo, tuiondoe kwa sababu si kila mara tutampata Waziri, Mheshimiwa Mary Nagu, watu wabaya wasije wakaingia humu wakatupingisha chenga tu ya kwamba, suala lenu liko kwa Rais, Rais analifikiria kumbe hata Rais hajapelekewa. Kwa hiyo, tunaomba tu kwa sababu Waheshimiwa Mawaziri tunakutana nao mara kwa mara, wapate tu uwezo na Waheshimiwa Mawaziri, wanayo madaraka mengi tu katika sheria nyingine. Kwa hiyo na hili naomba tu nilisisitizie kwamba lifikiriwe kuwekwa kwamba, Mheshimiwa Waziri achukue madaraka haya na alisimamie ili Watumishi wa Umma wasisumbuliwe tena

katika kwenda kwenye Mamlaka ambayo hawawezi hata kuomba *appointment* kwa urahisi. Lakini kwa Mheshimiwa Waziri, tuna uhakika ni rahisi kumfikia ndani ya Bunge na mahali pengine popote. Kwa sababu Mheshimiwa Rais ana majukumu mengine. Migogoro hii ni mingi, anaweza kufika mahali Rais kazi yake ikawa ni ya migogoro badala ya kutazama katika kuweka dira ya maendeleo ya Taifa hili, anakaa kila siku ni kushughulikia migogoro ya Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka na mimi nilisisitize ni hilo hilo la kusema ya kwamba, Watumishi wa Umma, wale watakaokuwa wanaamua katika mijadala hiyo, wawe na madaraka kamili ya kuamua. Kwa sababu kuna tabia haendi mwenye madaraka anaweza akasema aah huu mgogoro wa walimu acha tu nenda wewe anampeleka mtu ambaye ni *Junior,* walimu wanazidi kuumia na walimu wanaumia jamani. Walimu katika nchi hii wanaumia lakini ni watu ambao wanafanya kazi, ikija Sensa wamo, ukija uchaguzi wamo, vikija vitu vingine wamo na kipindupindu wamo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninao mfano, mwalimu mmoja nimesahau jina lake, lakini mmoja namkumbuka Marehemu Lwakahele, aliyefariki akiokoa vijana wake majini, akafariki pale Ziwani, hatumkumbuki mara nyingi. Lakini kuna mwalimu mmoja katika Visiwa vya Ukerewe, alikuwa anafundisha katika Kisiwa cha Bwiru, alikuwa na bahasha ya mitihani ya darasa la saba anaivusha kuipeleka Wilayani, mtumbwi ukazama, alikuwa anaogelea kwa mkono mmoja kuokoa bahasha ya mitihani ya wanafunzi, mpaka ng'ambo ya pili, wenzake wanamwambia achia hiyo mitihani utakufa, akasema wanafunzi hao wamesoma miaka 7, sihitaji wakapoteza muda wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja alilolisema Mheshimiwa Faustine Kabuzi, hawa ni miongoni mwa wanaonyimwa haki zao. Hayo aliyoyasema kuhusu madai yalihitaji chombo kama hiki kusimama kwa niaba yao kudai haki yao, kwa sababu hii ni dhuluma. Unawezaje mwalimu huyu anayepaswa kuingia kwenye maji kuhangaika, kupigwa na mawimbi, unamnyima fedha zake za likizo, unamnyima fedha zake za uhamisho, unamnyima haki zake za afya na unamnyima haki zake za nyongeza? Mshahara wenyewe ni mshahara gani ule, ukishamnyima ndiyo umemuua kabisa, nani anasimamia hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri hiki chombo lazima kifanye hivyo. Wafanyakazi wenye mishahara midogo midogo hawana *allowance,* akishapangiwa shule ya msingi katika Kisiwa cha Burubi, ambako hata wengine hamtaweza kufika katika maisha yenu, anavuka visiwa vitatu kabla hajafika kwenye kisiwa chake, unamnyima fedha ya uhamisho na unamnyima fedha zake za likizo! Kijana labda ametoka Kigoma anakwenda kufundisha katika visiwa hivyo unamnyima fedha zake za kwenda likizo, hiyo ni dhuluma na ni wizi kwa walimu hao. Walimu ndiyo wanaojenga Taifa hili, bila walimu wale kuelimisha Taifa hili, tusingekuwepo, bila madaktari hawa kutuhudumia katika hali ngumu, hatuwezi kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haki inapaswa itendeke na mimi nafikiri kwamba, hiki chombo kitakuwa ni chombo cha kuleta haki, kwa sababu Watumishi wa Umma kwa kweli bado ni wamisionari, wanajitolea. Wakiwaangalia wenzao katika

Mashirika mbalimbali ya binafsi, wengine hata wanapata robo ya mishahara ambayo wenzao katika Mashirika binafsi wanapata, kwa hiyo, hatuhitaji kuwasononesha zaidi, ni lazima masuala yao yaangaliwe kwa haraka zaidi. Kwa hiyo, ndiyo maana tunampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuleta Muswada huu, ambao kwa kweli utasaidia sana katika kuboresha maslahi ya Watumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wengine tunajivunia kwamba, tumeweza kulitumikia Taifa hili kwa muda mrefu katika Utumishi wa Umma. Kwa mfano, nilipokuwa Balozi India, hakuna kitu ambacho Mhindi anajivunia kama kuwa Mtumishi wa Umma, lakini kuna kila njia inayomfanya Mtumishi wa Umma aweze kuhudumiwa ili aweze kujisikia hata kama mshahara wake haulingani na kufanya kazi katika Mashirika mengine binafsi. Kwa hiyo, tunafikiria kwamba, hii *negotiating machinery* itawasaidia. Kwanza, hiki chombo kitawapa Watumishi wa Umma uwezo wa kujitawala, unapopewa nafasi ya kuzungumza na kutoa dukuduku lako, unapata nafasi nzuri sana ya kujitawala, lakini unapokuwa ni mtu unayefanya kazi unalalamika tu, unakuwa huna uwezo. Kwa hiyo, napenda tena niseme kwamba, hili ni suala ambalo ni muhimu sana. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikuwa na ombi dogo tu kabla sijakaa kwamba, sheria ya zamani, nilipoanza kazi ilikuwa *circular* zikija unapewa mwalimu unaweka kwenye *file* lako ili kila wakati uweze kurejea. Je, inawezekana sheria hii ikawa haki ya kila mfanyakazi itakapokuwa imepita? Kwa sababu matatizo tunayoyapata unakuta kwamba, watendaji wachache wasiokuwa na nia nzuri, hawawaonyeshi Watumishi wa Umma hizi *circular* na hawawaonyeshi Watumishi wa Umma hizi sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningemwomba tu Mheshimiwa Waziri kwamba, katika kuboresha hii sheria na kupunguza malalamiko na kupunguza kudanganywa kwa Watumishi wetu wa Umma, ambao wengi wako vijijini na wako katika maeneo magumu ya kupata taarifa, basi iwe ni haki ya kila Mtumishi wa Umma, kupata nakala ya sheria hii anapoajirwa, iwe ni sehemu ya *document* muhimu ya kuwa nayo ili asilalamike bila sababu na haziwezi kuvuruga utaratibu wa utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo na baada ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri, nina matumaini kwamba, atakapokuwa anahitimisha hoja yake, hataona vigumu kutia haya machache ambayo hayabomoi Muswada ambayo yamesemwa na wenzangu, isipokuwa yanaboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH AGNES MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu. Kwanza, kwa ujumla nitoe pongezi kwa Serikali na hasa kwa Wizara inayosimamia masuala ya Watumishi wa Umma, kwa jina kabisa Mheshimiwa Waziri, mshika dhamana, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu kwamba, *finally* au hatimaye kamtoa mwali uwanjani. Kwa sababu suala la chombo cha majadiliano kama wenzangu walivyosema, mimi nilikuwa Mtumishi wa

Umma, mwalimu na nikawa kiongozi kwenye Chama cha Walimu ngazi ya Taifa, suala hili tulianza kushughulika nalo mwaka 1996, kwa kudiriki hata kuandaa sisi wenyewe chombo cha majadiliano kiweje, kukipeleka Serikalini, tukaambiwa aah *step* hiyo siyo. Kwa hiyo, naamini jitihada zimeendelea kufanyika kiasi kwamba, leo tunazungumzia mambo yaliyowezekana na yaliyo hai kwa manufaa ya wafanyakazi wote wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi hizi nazitoa kwa sababu sheria zilizotangulia, kama alivyotueleza Mheshimiwa Waziri, Sheria ya mwaka 1962, ikabadilishwa na sheria ya mwaka 1970. Kwa kweli amesema kabisa kwamba, makundi mengine ya watumishi wa Umma wala hayakuwa na nafasi hiyo basi ya kuzungumza na waajiri wao. Kwa mfano, wakiwemo walimu, hata hawa wa *Fire and Security,* sidhani kama wenzetu hao walikuwemo humo, lakini kwa leo makundi yote haya naona yamepata nafasi kwamba, wataweza kuzungumza masuala yao kisheria. Labda kama huko nyuma walitimiziwa baadhi ya malalamiko, basi ilikuwa tu ni hisani ya mhusika kwamba ni hisani. Lakini kwa sasa hivi kutokana na sheria hii, itakuwa ni wajibu wa kisheria mwajiri na waajiriwa kuweza kuzungumzia masuala yao wakafikia muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na pongezi hizo pia naomba niseme kwamba, naipongeza Wizara kwa sababu imejitahidi sana kuwashirikisha wadau wote wanaohusika na masuala ya Utumishi wa Umma kama wenzangu walivyosema. Ni kutokana na mchango huo kwamba, imesaidia sheria hii kwanza kurekebishwa rekebishwa, kwa sababu mwanzoni tulivyogawiwa Muswada wa Sheria, ulivyoandikwa ni kidogo tofauti na huu, lakini huu ni mpya, nasema ni mpya umetokana naamini na marekebisho baada ya kupata mawazo na michango ya wadau mbalimbali ndipo Serikali ikaridhia kuyaweka haya jinsi ambavyo imeyaweka kwa ufanisi zaidi na kwa uzuri zaidi na kwa kueleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo na maelezo ya jumla, kama wenzangu walivyotangulia kusema, ningeomba Wizara iendelee kuboresha na kuufanya Muswada huu uwe peupe zaidi kusomwa hata na mtu ambaye haelewi lugha za kisheria, ile sehemu ya 4 ukurasa wa 5 kuweka kabisa zile aina za Utumishi wa Umma zitajwe waziwazi. Hiyo nikiilinganisha na aliyoyasema msemaji aliyenitangulia, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mwalimu wangu kwamba, tukiweka wazi *scheme of service,* itawatia moyo zaidi na faraja walengwa wote kwa sababu ndiyo wataona kabisa kwamba, hii sheria ya chombo cha majadiliano na mimi nimo kwa uwazi. Kwa sababu kwa ku-*refer* tu sheria ya mwaka huu ya *Public Service,* Mtumishi mwingine wa Umma hata hajawahi kuiona hiyo sheria. Sasa unapomwambia aka-*refer* kule, inakuwa ni kazi ambayo kwa kweli haiwezekani. Kwa hiyo, naomba iwepo hiyo na ielezwe wazi kusudi kifungu hiki kiweze kujitosheleza kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa huo huo wa 5 pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri, katika kutoa taarifa yake,alisema kabisa kwamba, hawakukubaliana na kipengele cha 3 cha *the most representative* ili awe ndiyo mwakilishi katika hayo majadiliano, mimi nilikuwa nashauri basi hawa watu wasiwe wawili, isiwe *two persons,* wawe zaidi basi kwa sababu ninachelea, kwa uhuru wa wafanyakazi ambao Serikali imeutoa kutokana na sheria ya nyuma kwamba, watu 20 wanaweza wakaunda chama

chao cha wafanyakazi na kwamba hawa tusiwanyime demokrasia kuwakilishwa, basi tuongeze huu wigo wasiwe wawili. Kwa sababu watu watakuja kugombana bure hapo kwamba, nani sasa akawakilishe na Vyama vitakuwa saba katika *Service Scheme* moja, itakuwaje?

Kwa hiyo, ninashauri kwamba, ili tusiwanyime basi hata hao wachache watakaokuwa wamejiunga katika vyama, basi isiwe wawili, tuongeze idadi ya watu wawe wengi zaidi ili kuleta huo uwakilishi wa jumla wa watu wengi.

Sina cha ziada sana, sehemu iliyopendekezwa kwamba, pawe na kifungu cha 4 ukurasa wa 6, Wawakilishi wawe ni wale wenye uwezo wa kutoa maamuzi, naafikiana sana na pendekezo hilo. Kutakuwa na kupigana chenga, mtu anasema ngoja nikamwulize Waziri aje aseme. Sasa, katika hali za dharura na nyeti za kugombana gombana kikazi, hiyo itakuwa ni kuchelewesha muda na kuwaweka wafanyakazi katika hali ya roho juu juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine wamekwisha sema, napenda tu kuunga mkono waliyoyasema wenzangu, kwa sababu yalikuwa na msingi wake, ila tu niendelee kushukuru kwamba, kwa kweli mimi kama mwalimu wa zamani, ambaye nimestaafu kutokana na Ubunge, naona kama kazi yangu ya mwanzo katika uongozi ule wa awali leo na wenzangu waliokaa pale tumefanikiwa kwa sababu hatimaye *negotiation machinery* ya walimu na wafanyakazi wengine imepatikana. Ni faraja kwa walimu na wafanyakazi wengine ambao hawakuwa kwenye mlolongo huu wa kusaidiwa huko nyuma kwamba, sasa hii itatupa moyo wa kuweza kufanya kazi kwa bidii. Lakini kama wenzangu walivyotangulia kusema, Elimu ya Muswada huu ni muhimu sana kwa wafanyakazi wote. Ningeomba basi kile kipengele cha wajibu wa watumishi na wajibu wa waajiri kiwekwe wazi katika kanuni zitakazotungwa kutokana na Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia hayo machache, naunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwamba, kwa kweli *she has been a hero* katika kupigania haki za wafanyakazi nchini na hatimaye ameweza kuleta kitu kinachoeleweka na kitakachowalinda. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Margareth Mkanga. Mheshimiwa Fundikira amesema: *"She is a heroine."* Basi, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupewa nafasi hii na ningeomba nimpongeze Waziri kwa Muswada huu ambao naamini kabisa, utaboresha ufanisi katika Sekta ya Ajira ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri kidogo kuhusiana na *Joint Staff Council,* pamoja na *Wages Award Board*. Ni kweli kabisa sababu kubwa ni kuhakikisha Serikali iweze kuhudumia kwa uwezo ilionao, lakini kwenye *section 11* ya hiyo *Bill* Namba 17, inazuia *Joint Staff Council* isijihusishe na mambo ya mishahara pamoja na ajira. Lakini kimsingi nadhani ajira ni mshahara, kwa sababu tunataka *capacity* ya Serikali iweze kutumika kwa kuajiri watu wasije wakaomba vitu ambavyo havipo. La

msingi ni kuwa, *negotiating machinery* hii ifanye kazi, lakini hapo hapo iwahusishe wahusika, wadau wote kulijadili suala la mshahara ili wajue mwongozo wa kulishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kuwa, *Joint Council* na *Wages Award Board,* kwa wakati wao pia nao wakutane, wajadili ili wajue taratibu za *remuneration* ziwe vipi. Lakini kusema tu hawa wasishughulikie mambo ya mishahara, wasishughulikie mambo ya ajira, nadhani ni kubana ule wigo wa *negotiation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimeangalia kwenye matoleo yote mawili, naona jinsia kidogo imeachwa. Wanazungumzia *'The Minister'* wanaweka *'he',* hawajaweka *'she'* na Waziri wetu ni mwanamke. Sasa naona hilo lingerekebishwa, iachwe hiyo *gender* au ikiwezekana itajwe Waziri tu, kwa sababu hiyo nadhani itakuwa siyo sawa sawa kuifanyia jinsia.

Kwa hayo machache, ninaamini kabisa hii *negotiating machinery* iliyoanzishwa itasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna sehemu nyingine ambayo ningeshauri Serikali pia iangalie. Nakumbuka wakati nachangia kwenye Muswada wa Wizara ya Afya, nilizungumzia matatizo ya ajira ya wafanyakazi walioajiriwa na Hospitali Teule, mfano hospitali ya *Saint Francis* Ifakara. Wafanyakazi wale wanafanya kazi katika mazingira ya aina moja na wote wana shahada sawa, lakini kwa ajili ya taratibu za kisera za nchi za ubinafsishaji na kiuchumi imekuwa vigumu wa kuwatambua hawa wafanyakazi wako kwenye *category* gani ya ajira. Kwa hilo, ningeomba pia kwenye *machinery* hii mpya inayoanzishwa, iangalie uwezekano wa kuwachukua hawa watu ambao wanaegemea sana kwenye kutoa huduma za umma waingie kwenye *negotiating machinery* hii, pia kwa taratibu za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaamini kabisa *negotiating machinery* hii itapunguza migogoro Serikalini na huenda ikaongeza kabisa ufanisi katika kazi kwenye sekta ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nashukuru sana kwa kupewa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, ambaye ametoa hoja na ameiwasilisha vizuri. Lakini vile vile niwashukuru wale wataalam wake wote alioshirikiana nao katika kufikia uwasilishwaji wa hoja hii. Napenda nimpongeze Mheshimiwa Dr. Nagu, kwa jinsi ambavyo amewashirikisha wadau kutoka Sekta mbalimbali za watumishi ili kuhakikisha kwamba, hoja hii inawasilishwa kwa ufasaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii inakuja kwa lengo la kuleta mabadiliko katika Sekta nzima ya masuala ya Utatuzi wa Migogoro ya Utumishi. Kwa hiyo, ni jambo ambalo ni zito na ambalo limechukua kipindi kirefu, lakini napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa jinsi ambavyo amekuwa mvumilivu, ametoa nafasi ya kupokea maoni yaliyokuwa yanatoka kwa wadau na ameyafanyia kazi na hata kwa kweli tumeweza kuona jinsi ambavyo amewasilisha Muswada ukiwa pia na michango mingi iliyotoka ndani ya Kamati iliyohusika kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu, ambao unalenga kuunda Mabaraza ya Majadiliano ya pamoja ya Utumishi, ambayo kwa kweli yanakusudia kuboresha utumishi wa umma na kuboresha tija, lakini zaidi kuhakikisha kwamba, migogoro inapungua na pale inapojitokeza inatatuliwa kwa urahisi kwa sababu mahali ambapo kuna migogoro isiyokwisha ni mahali ambapo kuna matatizo na mahali penye matatizo, hakuna tija. Pia, kutakuwa na chombo ambacho watumishi wa umma watashirikishwa, tofauti na zamani ambapo watumishi ilikuwa mara nyingi wajibu wao mkubwa ni wao kupokea na kutekeleza na hata zikawepo sheria nyingi kwamba, ni wajibu wa mtumishi kupokea na kutekeleza, kama kuna maswali basi ayaulize hapo baadaye. Hii inalenga kuhakikisha kwamba, uongozi unatekeleza majukumu, lakini pia watumishi wanatekeleza majukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mawazo yangu, nafikiria kwamba, Muswada huu ni ukombozi wa mtumishi. Naona kama Muswada huu unalenga kuwasaidia watumishi tofauti na wakati uliopita. Kwa hiyo, ninapolenga kuwaangalia zaidi hawa wenzangu, watumishi ambao wanafanya kazi za wito, ambao kwa wakati mwingi wamekuwa wanafanya kazi kubwa na nzito, maslahi kidogo, wanafanya kazi kwa muda mrefu na hawana mahali pa kushauriana na mwajiri wao. Kwa mfano, tumekuwa tunaona matatizo yanayowakumba walimu wanapohamishwa, tunawaona wanapofanya kazi kwa muda mrefu na wakiwa wanastahili kupandishwa madaraja lakini hawapandishwi na hata wakipandishwa zile tofauti za mishahara yao haziwafikii na pia tumekuwa tunaona wanahitaji mafunzo. Hata Afisa wa Afya aliyeingia katika kazi akiwa na cheti ni lazima kumsaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayati Mwalimu Nyerere, aliwahi kusema kwamba: “Elimu ni sawa sawa na panga, unapolinunua ni lazima uendelee kulinoa, kama hulinoi linakuwa butu.” Kwa hiyo, mwalimu ama mtaalam yeyote akipata nafasi ya kujielimisha zaidi, pia ni haki yake, lakini walikuwa wanapata tabu wanapohitaji kujielimisha na wanapata tabu wanapohitaji kupata huduma za afya zinazoboresha afya zao ili kuweza kufanya kazi zaidi. Sasa, haya yamepata jibu kwa sababu watakuwa wanapata mahali ambapo watazungumza wakati wakiwa kazini, hatma yao na hata baada ya kazi na masuala ambayo yanakuwa yanawakumba wale wanaostaafu. Unakuta mtu anastaafu ama anafariki, lakini haki zake zinakuwa hazipo wakati yeye aliitumikia nchi kwa uaminifu mkubwa. Kwa hiyo, ninapongeza sana Muswada huu na ninaamini kwamba, sasa unakwenda kuwa majibu kwa yale ambayo yamekuwa ni kikwazo kwa muda mrefu kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, naomba kutoa ombi kwamba, Sekta binafsi isiachwe kwa sababu Watanzania wengi pia wanafanya kazi kwenye Sekta binafsi, waangaliwe ili kuondoa manyanyaso makubwa wanayoyapata. Nao waweze kupata haki kwa sababu kufanya kazi ndani ye Sekta binafsi, hakumaanishi hawawatumikii Watanzania. Kwa hiyo, hilo nalo liangaliwe ili waweze kupata haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuipongeza Serikali pia kwa marekebisho mbalimbali ambayo imeweza kuyaonyesha katika vipengele mbalimbali ambavyo viko ndani ya Muswada huu. Katika ibara ya 4 (1), uanzishwaji wa *Joint Staff Council,* ambayo kimsingi itakuwa inawakutanisha wahusika na kuweka taratibu nzuri za mashauriano, nakubaliana kabisa na wenzangu ambao wameeleza kwamba, pale kwenye *Service Scheme* patajwe kabisa kwa sababu sasa hivi sheria tunazo nyingi, ukitaka kuiweka sheria hii isomwe pamoja na sheria nyingine, maana yake ni kwamba, kama mtumia sheria hii atakuwa hana hiyo sheria nyingine, hawezi kufanyia kazi hiki kipengele ambacho kitakuwa kinahusika na kwa hiyo atajikuta amebaki sasa hawezi kuitumia sheria hii ipasavyo na lile tatizo litaendelea kuwa pale pale. Kwa hiyo, itamlazimu kuweza kufuata hizi sheria mbili zote pamoja.

Hivyo, katika *Service Scheme* ibara ya 2 (b), ifahamike kama ilivyo kwenye Sheria ya *Public Service* ibara ya 7 sehemu ya 2 ya mwaka 2002, iwekwe waziwazi kabisa, zile *schemes* nyingine zote pale zitajwe zionekane, zile zinazohusu Watumishi wa Serikali za Mitaa, Walimu, Watu wa Zimamoto na sehemu nyingine ambazo ni muhimu ziwekwe pale, pia na Watumishi wa Afya ili kuweza kuwapa nafasi waziwazi na kuitumia sheria hii moja ikiwa imekamilika badala ya kuwa kama ni vipande vipande. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ya pili ambayo tulikubaliana katika Kamati, lakini nimeona kama vile pengine wakati wa kuiandika labda wamefikiria vinginevyo, basi ninaendelea kuisisitiza kwa umuhimu wake, ni pale ambapo Wizara ilikubali kuongeza, naona Serikali imeongeza sehemu ndogo ya (d) katika ibara ya 4 pale 3(d) kwamba, kila *Joint Staff Council* itaundwa na Wajumbe ambao miongoni mwao wanne watakuwa ni Watumishi wa Serikali wanaoteuliwa na Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kipengele hiki pale chini kwa kuepusha kupeleka wawakilishi katika mjadala huu, ningetegemea kuwe na msisitizo kwamba, wapelekwe watu ambao wana maamuzi. Tumekuwa tunapata matatizo ya ucheleweshwaji wa masuala ambayo hata ni ya msingi kwa sababu mara nyingi wenye maamuzi wanakuwa na shughuli nyingi. Kwa hiyo, wanapeleka wasaidizi wao ama watu walio chini kabisa maadam yeye anaamini kwamba amemtuma, basi. Lakini anapokuwa amekwishafika kwenye lile eneo, kwenye sehemu ya mjadala, basi hushindwa kutoa maamuzi na badala yake husema ngoja kwanza katika hili nadhani sina kauli nirudi nikamwulize mkubwa wangu wa kazi, naona hili liko juu ya uwezo wangu. Kama kweli tunakusudia kuweka mabadiliko na kuhakikisha kwamba tunakuwa na maamuzi ambayo yanatekelezwa bila kuwa yamechelewa chelewa, Wajumbe wa pande zote mbili ni lazima wawe ni wale wenye uwezo wa kutoa kauli, wenye uwezo wa kufanya

maamuzi bila kurudi tena kwenda kuhitaji kufanya *consultation* zaidi na zaidi, ambazo zitachelewesha maamuzi ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wangu ningependa nizungumze kidogo kuhusu hii ibara ya 23. Kwa jinsi ambavyo tulijadili nafikiri Mheshimiwa Waziri pia katika kuwasilisha ameeleza kwamba, hili hatukukubaliana, labda hatukufikia muafaka, lakini tulilizungumza. Katika muafaka huo kwa jinsi tulivyozungumza, nilikuwa najaribu kutazama athari ambazo pengine zingeweza kutokea na nimekuwa nikirudia kusoma ibara hii ya 23 kuanzia sehemu ya kwanza mpaka sehemu ya nne, lakini kila nikizisoma kwa kweli kwa upande wangu, sikuona kama kuna matatizo yoyote yale ambapo *award* hizo zikitolewa na Rais zitaweza kuleta madhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuzifanyia sheria hizi marekebisho mengi. Nadhani nikisoma hata hili eneo la kwanza tu anasema: *"Where the report of the Court in respect of any dispute referred to it, is submitted to the Minister, he shall in any case, without delay and within fourteen days of such receipt, submit the report with any comments he may wish to make with thereon to the President."* Kwa hiyo, Waziri naye amepewa muda kuhakikisha kwamba anaiwasilisha kwa Rais. Vile vile, Rais kwenye kipengele kinachofuata naye amepewa siku 21 kuwa amefanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiria kwamba, kwa sababu masuala haya baadaye yatakuwa yanaugusa uchumi wa nchi na anayesimamia uchumi ni Mkuu wa Nchi na kwa kuwa tunaendelea kufanya mabadiliko haya, kama sisi hatutakuwepo watakuwepo wengine, watayazungumza haya wayaone kwa wakati huo athari zake zitakuwa zinafanana vipi. Lakini la msingi ninaloliangalia ni kuiona haki ya kumpa mfanyakazi nafasi yake ya kujadili haki yake katika kufanya kazi ya kujadili maslahi yake ya kukataa kuonewa kwa kupewa zile haki ambazo zamani zilikuwa hazipo, kwa mfano, hizo za kufungia wafanyakazi ama waajiri nje zilikuwa hazipo, sasa hivi zipo. Nafikiri pengine inawezekana tukabeba mabadiliko mengi sana kwa wakati mmoja na baadaye yakatuletea matatizo na tukalazimika labda kurudi tena hapa kuyazungumza. Kipengele hiki kimoja nadhani hakina matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninapenda kurudia kukushukuru kwa kunipa nafasi, lakini vile vile nirudie kumpongeza Mheshimiwa Waziri, nikiwa na imani kabisa kwamba, yale yote ya msingi ambayo naye anaamini kwamba yanaenda kuboresha Muswada huu, atayaleta mbele ya Bunge lako Tukufu ili yaweze kuwekwa pamoja na kuweza kuwa sheria. Ninapenda kutoa shukrani zangu na ninaunga mkono hoja.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniruhusu nami nichangie katika Muswada huu.

Kwanza kabisa, tunaishukuru Serikali, pamoja na Waziri, kwa kutuletea Muswada huu ili sasa wafanyakazi pamoja na waajiri, waweze kujadiliana na kwa kuwa tunadhani Serikali yenyewe haikushtakiwa Mahakamani wala haikushinikizwa ili iweze kuleta

Muswada huu, basi ile nia yake thabiti na njema, itaendelea kuwa nayo ili kuweza kusikiliza kama ilivyotuletea tujadili, mengine tunadhani yanaweza yakakubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza hapa kuna Wajumbe wanasema walikuwa kwenye Kamati iliyojadili Muswada huu, lakini wakawa wanachangia hapa na ndiyo wengi, kinyume na utaratibu ambao tumeuzoea. Kwa sababu mkishakubaliana kwenye Kamati, ndiyo inakuwa hivyo hivyo, unapoamka unashangilia kwamba, tumeshakubaliana na Waziri. Kilichokuwepo hapa ni kwamba, baadhi ya waliokuwepo wanasema, Mheshimiwa Waziri, lakini tulivyokubaliana kuna mahali umetuangusha, tungeomba yale maneno yetu uyaweke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaosema ambao hatukuwa kwenye Kamati na sisi ndiyo mawazo yetu hayo. Kumbe tunakuta kwamba, mawazo ya waliokuwa kwenye Kamati na sisi ambao hatukuwemo yanaoana. Kwa hiyo, huo ndiyo utashi wa Wabunge/Wawakilishi wa Wananchi katika kuishauri Serikali. Kwa hiyo, katika hatua kama hiyo, kwa heshima kubwa ambayo Waziri mwenyewe amejizolea na tunavyojua anavyochapa kazi, kwa kweli tunadhani mapendekezo yale atayasikiliza kwa sababu na sisi hatuna nia ya kwamba, wafanyakazi wapambane na Serikali na Serikali ipate hasara katika kuhudumia watumishi ambao imewaajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa misingi hiyo, utaniwia radhi kama nitarudia baadhi ya mambo kwa sababu kuna mtu alikuwa anauliza: "Mbona kila asubuhi mtu akiamka hunawa usoni na mbona uso hauwi tofauti na sehemu nyingine ya mwili wake?" Lakini nadhani ni katika utaratibu wa kawaida kwamba, unapoamka unanawa usoni na hauwi mweupe kwa sababu ya kuunawa, kama ni mweusi, ni mweusi tu, lakini ni katika kuondoa yale matongotongo. Kwa hiyo, kama nitarudia baadhi ya ambayo yamesemwa ni kwa ajili ya kuondoa kabisa yale matongotongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hii sehemu ya *Joint Council,* kwa sababu ndiyo kitu ambacho kinatupa tabu, nilikuwa naangalia katika kipengele cha 4, kama walivyosema wale wengine, kwa kweli tunaomba kama mlikubaliana kwenye Kamati na sisi ambao hatukuwepo, zile *Service Scheme* zitajwe pale, kama ni ya walimu itajwe, kama ni ya waganga itajwe, kama ni ya wavuvi itajwe, wavuvi siyo wafanyakazi wa serikali, lakini kama ni ya wanaohusika, nafasi zote hizo zitajwe ili tuweze kujua bayana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya hatuwezi kujadili kitu ambacho hakipo kwenye Shughuli za Bunge. Lakini kuna Muswada ambao unakuta tumeshapewa na kule wametaja, kama wanakuwa wametaja tumepata bahati hiyo ya kujua kwa ajili ya ile ya *labour* ambayo wameleta, wametaja hizo. Inakuwa ni vizuri kwamba, kunakuwa na vitu ambavyo vinaoana na viko kwenye sehemu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ilikuwa ni kwenye kifungu namba 4 (3), anaposema: *"Every Service Joint Staff Council shall consist of (a) a Chairman and a Vice-Chairman, who shall be appointed by the Minister from amongst two persons who shall be recommended by a Trade Union representing the category of the service scheme*

*in question and two other persons recommended by the Minister responsible for the Service Scheme in question."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwenye huu mstari wa tatu wa hicho kifungu kidogo (a) *recommended*, kama hiyo *Trade Union* itakuwa na watu 20, labda tuseme ni walimu, kuna walimu watasema sisi wenye cheti tunaunda ya kwetu. Watu wengine watasema, sisi walimu wenye stashahada, wengine watasema, sisi walimu wenye *degree*, wengine watasema, sisi walimu wa kanda fulani, lakini *all in all* huenda tukakuta kwamba, katika huo utumishi wa walimu kuna kundi ambalo ni kubwa na kinachogombewa pale ni maslahi ya walimu kwa ujumla, lakini kwa sababu sheria nyingine inaruhusu walimu 20, walimu kutoka sehemu fulani wajianzishie *trade union*, halafu wengine hawa kwa *influence* wanayoijua wao, ile ndogo ndogo ndiyo mnapeleka wale wawakilishi, itatupa tabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana watu wanasema kwamba, tu-*recommend* hapa kwamba, hayo maneno yasomeke: *"A Chairman and a Vice-Chairman who shall be appointed by the Minister from amongst two persons who shall be recommended by the most representative trade union representing the category of the Service Scheme.* Nilimsikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri, alisema na wachache wasilikizwe, ndiyo na wachache wasikilizwe. Lakini sasa wachache wasikilizwe kwa ajili ya wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sisi hapa tuna kanuni kwamba, ninyi watu wa Upinzani kama kuna Chama chenye watu wengi, kama ni *CUF* kinaunda Viongozi wa Upinzani, kikitaka kuwaita na nyie kinawaita. Lakini sasa hatuwezi kuwadhulumu tukawanyima haki zao kwa kusema kwamba, basi ili mradi na wale wachache wasikilizwe. Nadhani ndiyo inakuwa mantiki hiyo kwamba, kwenye ile kada kuna watu ambao wanakuwa ni wengi, hata unapo-*negotiate* nao kama kuna mgogoro utautanzua, kwa sababu huwezi kuwafungia wengi kwa kudhani kwamba, unawapa wachache haki. Tuna uhakika kwamba, kama wanaozungumza ndiyo wengi, basi ni maslahi ya wengi, kwa sababu hata wale wachache watapata, kwani wale wachache wanakuwa wanazuiliwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, inazungumziwa mishahara ya walimu na walimu kwenye Shule za Msingi kuna wale wenye *diploma* na kuna wenye cheti. Wengine wanasema, sisi wa *diploma* kwa sababu tuko Shule za Msingi, tuna chama chetu na tunataka kujadili. Wakati huo huo wale wa cheti ni wengi kuliko wao. Sasa unataka kuwasikiliza hao wenye *diploma* uwaache wale wa cheti, kuna nini wakati hawa ni wengi? *That is the logic. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa huo huo kuna kile kipengele kidogo (b) ameiainisha pale akasema: *"two public servants nominated by trade union, the respective trade union, Chairman and the Secretary, four Government Officials appointed by the Minister being ..."* Ameziorodhesha pale kwenda mpaka (iv). Baada ya pale wengine ndiyo wakawa wanauliza kwamba, hawa unaowaleta wawe ni watu gani? Unamtuma *Director* wa Wizara ya Fedha, unamtuma *Commissioner* au unamtuma nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ndipo tunaposema kwamba, iwekwe *provision* baada ya maneno yale kwamba, wale watu watakaotumwa kutoka kwenye Wizara hizo na wale wanaohusika wawe ni watu ambao wana uwezo wa kufanya maamuzi ili kuweza kuokoa muda, kwa sababu kuna vitu vingine vinaweza kuchukua mwezi au mwaka na yule unayemtuma kwa sababu ya jinsi alijibu akiwa hana uhakika, akasababisha migogoro badala ya kwenda pale ku-*solve* matatizo, kwa sababu hana majibu ya uhakika. Anasema nikisema hivi huenda mkubwa wangu kwenye Wizara ataniuliza au huenda Katibu Mkuu ataniuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo itatuokolea fedha za umma, kwa sababu haiwezekani tumtume mtu ambaye hana maamuzi, atapata posho atakwenda pale na gari halafu baadaye atasema, nitarudi. Unaongeza tu siku za vikao na kwa hiyo, unatupotezea muda tu. Ndiyo tuna-*argue* kwamba, tupeleke pale watu ambao wanaweza kufanya maamuzi ambayo ni ya msingi na itaharakisha hata maamuzi, kwa sababu kama amekuja mtu ambaye ni mzito pale, anapoondoka akimwona Waziri, basi wanazungumza *once and for all* yale mambo yanakwisha. Ndiyo maana tunaomba mawazo hayo wayaweke, lakini pale hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, kwa heshima na taadhima,asije akatukamata kwamba sasa hiyo mnaileta kwa kanuni gani. Tunadhani kwa hekima na busara zake anaweza akaiweka pale badala ya kugombania kwenye misingi ya usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa jinsi majadiliano yalivyokwenda, ni matumaini yangu kwamba, Mheshimiwa Waziri ameyasikiliza na sisi kwa hakika tunaunga mkono huu Muswada na mabadiliko haya yakipita kwa kweli tutachekelea kabisa na kuunga mkono vizuri sana. Tunashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mawazo yangu katika kuchangia Muswada huu ulio mbele yetu. Natoa shukrani za dhati kwa Waziri, Mheshimiwa Dr. Nagu, kwa kuwashirikisha wadau wengi ili kuujadili Muswada huu. Pia, natoa shukrani kwamba, katika Wizara yake kwa upande wa utendaji, Katibu Mkuu na wataalam wake, nao pia walipata nafasi ya kuuzungumzia kwa kina Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hivyo kwa sababu mimi pia ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kwa hiyo, mengi niliyaona, ambayo yamenifurahisha sana kwa jinsi Serikali ilivyoleta Muswada huu na jinsi watu wengi walivyoshiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwa ni kazi bure kuwa na Muswada ambao haukidhi matakwa ya walengwa na kwa kiasi kikubwa Muswada huu umejitahidi sana kukidhi matakwa ya walengwa.

Tulipokuwa katika Kamati, wadau walileta mapendekezo mengi, binafsi nafurahi kusema kwamba, ninavyouangalia Muswada huu, pamoja na zile *amendments* zilizoletwa, Serikali imejitahidi sana kuingiza karibu yale yote yaliyokuwa yameombwa na wadau ili yawepo katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unaunda Chombo cha Majadiliano katika Utumishi wa Umma na hii ni nafasi nzuri sana ya kuhakikisha kwamba, ngazi mbalimbali zinahusishwa na zinashiriki katika maamuzi mbalimbali ya utendaji Serikalini. Marekebisho yanayofanywa ukiangalia zaidi katika Wizara hii ya Maendeleo ya Watumishi, unaweza ukasema kwamba, ni *dynamic,* yaani yanakwenda mbio na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nasema ni utaratibu mzuri hasa kwa hali ya sasa, kwa sababu hapo zamani kama mtakumbuka, wale wengi ambao walikuwa Watumishi Serikalini, walikuwa wamezoea sana *Staff Circular* au *Establishment Circular* ndizo mara kwa mara zilizokuwa zinatawala mambo mengi ya Utumishi Serikalini, lakini ukiangalia sana utaona ilikuwa *Top Down Approach,* yaani maamuzi yalikuwa yanatolewa kutoka juu kwenda chini.

Kwa hiyo, hii ni mara ya kwanza kuon Muswada ambao unashirikisha ngazi mbalimbali toka chini mpaka juu na mimi nafikiri utaratibu huu utakuwa mzuri zaidi. Ni kweli sasa itahitajika elimu kubwa kwa watumishi wetu ili waweze kuuelewa Muswada huu sawa sawa na pia waweze kujadiliana mambo mbalimbali. Hasa kwa mfano, katika uanzishaji wa *Scheme of Service,* hapo kama tukishirikisha watumishi wakijadiliana wanafikiria ni mfumo gani uwepo katika sekta yao na hatimaye wakija kukubaliana kwamba mfumo tunaotaka ni huu na ngazi zake ziwe namna hii, nafikiri hiyo itapunguza sana migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo, nimeona siku hizi Idara ya Utumishi imebadili jinsi ya upashanaji wa habari. Kwa maana kwamba, siku hizi semina na warsha ziko nyingi mno kiasi kwamba kama unakwenda ofisini, ukitaka kwenda kumwona Katibu Mkuu au Mkurugenzi, ni vigumu sana kuwakuta, aidha wanakwenda kwenye mikutano au wanakwenda kwenye semina au warsha, kongamano, ambazo haziishi. Mimi naona kama tukiendelea namna hii, ufanisi wa kazi Serikalini utapungua sana. Ni lazima Wizara itoe miongozo ya jinsi ya kudhibiti hizi semina na warsha zilizojaa.

Zamani tulikuwa na *staff circular* katika kufahamishana lakini imefika mahali, kwa mfano, hasa Wabunge wengi watakumbuka, ukienda katika Wilaya zetu nyingi *DEDs* mara nyingi wanahudhuria Mikutano ya Halmashauri au ya Kamati ya Fedha na Uchumi, lakini baada ya hapo ukiuliza *DED* yuko wapi? Unaweza ukaambiwa kwa mfano, *DED* wa Masasi kuwa yuko Mwanza, amekwenda kuhudhuria warsha au *DED* wa Mwanza yuko Sumbawanga amekwenda kuhudhuria warsha.

Mimi nadhani hili halileti tija yoyote Serikalini, naomba sana Wizara hii ya *Management* ya Utumishi, iingilie kati ili iruhusu kwa Maafisa Waandamizi wahudhurie warsha au semina ngapi kwa mwaka. Iweke idadi kabisa na ikifuatwa idadi hiyo, naamini watu watafanya kazi. Lakini bila utaratibu tunakuwa na wasiwasi kwamba, haya mambo naona yatakwenda *out of control. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko haya pia yasije yakawafanya Wakurugenzi ama Makatibu Wakuu, wakasimu madaraka yao kwa vyombo au mikutano hii mbalimbali. Kuna dalili nyingi sana zinazoonekana kwamba, wengi wa Maafisa Waandamizi siku hizi wanaogopa sana kutoa maamuzi mbalimbali. Maamuzi yanatolewa baada ya kuwa na mkutano wa maafisa mbalimbali au jopo la Wakurugenzi, wawepo kwa pamoja wajadiliane, halafu ndiyo uamuzi utoke. Kwa kweli, jambo hili inabidi liangaliwe vizuri ili tuweze kuendelea kuwa na maamuzi mazuri, yenye busara yanayotoka kwa viongozi wetu tuliowaweka kwenye madaraka yale. Kuogopa kutoa maamuzi kunaifanya Serikali iwe inalegalega katika kufanya mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninataka kulizungumzia ni kuhusu watumishi wanaofanya kazi katika eneo moja, kwa mfano, Hospitali Teule au zile *voluntary agencies.* Hapo utakuta kuna watumishi walioletwa wanafanya kazi lakini wako chini ya Serikali Kuu. Halafu wapo watumishi wengine wanaolipwa mathalani na lile Shirika husika, mfano wamisionari na kadhalika, utakuta tofauti ya mishahara inakuwa kubwa.

Wakati mwingine wale wanaolipwa moja kwa moja na Serikali, mishahara yao ni mizuri kuliko wale wanaolipwa na *mission.* Sehemu nyingine inatokea kwamba, wale wanaolipwa na mashirika haya wanakuwa na mishahara mikubwa na mizuri zaidi ya wale wanaolipwa na Serikali. Sasa ukiangalia mfumo wa namna hii, unajenga matatizo na migogoro mingi isiyo na sababu. Kwa hiyo, katika haya Mabaraza tutakayokuwa tunayaunda chini ya Sheria hii, kwa kweli ipo haja ya kuangalia unawezaje kuainisha hali ya mishahara na hali ya utumishi katika eneo lile bila kujali kwamba huyu ameajiriwa na *mission* au ameajiriwa na Serikali Kuu. Mimi naona kwamba, hapo ipo haki kabisa kwamba, hawa watumishi walio chini ya shirika fulani au chini ya utaratibu wa kazi fulani, wawe wanaangaliwa na maslahi yao yawe yanaangaliwa na yawe yanafanana kwa kila hali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilitaka kuzungumzia katika Muswada huu kwa mara ya kwanza suala ambalo mimi naipongeza Serikali ni kwamba, watumishi wamewekewa kipengele cha kuweza kuwa na migomo. Hili ni jambo la kimapinduzi kabisa. Haki ya kufanya mgomo ni haki ya wafanyakazi, lakini zamani haikuwepo. Ninachoomba tuwe na tahadhari kwa sababu kitu haki hakikuwepo sasa tusije tukaanza kuwa na milipuko ya migomo mingi katika sehemu zetu za kazi. Tukitumia vizuri sheria hii, hatakuwa na sababu ya mikwaruzo ambayo itasababisha migomo. Lakini kama tukitumia vibaya, kwa kweli haki ya wafanyakazi itakuwepo ili wagome na migomo kama haitumiwi vizuri inaweza kubomoa amani, utulivu uliopo kazini na hivyo kutoleta ufanisi wowote. Mimi naomba hapa itatakiwa juhudi ya ziada kuelimisha wafanyakazi na

wananchi juu ya maana ya mgomo ili kwa kupitisha sheria hii, tusije tukagubikwa na migomo mingi isiyo na sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nilitaka kuzungumzia kile kipengele cha 23, ambacho naona kama kinaleta matatizo. Kipengele cha 23 kinachohusu *role* ya Rais katika Muswada huu na kama ilivyokuwa imesemwa hapa kwamba, Rais anaweza kutoa *award* na wengi wanaona kwa nini atoe Rais? Mimi nataka kusema kwamba, namwona Rais, kama ni mtu mmoja, ambaye mambo yote karibu yako kwake. Kwa hiyo, tusimfunge, tumruhusu kutoa *award* inayotoka kwa Rais, kitu kikubwa na kizito. Kwa hiyo, kwa mfanyakazi ambaye atapata heshima hiyo, ningeomba kushawishi wenzangu kwamba, kwa kweli kipengele hiki kiendelee kama kilivyo katika *section* ya 23 kwa sababu inategemea kwa wakati huu inawezekana haja hii isiwepo, lakini kwa miaka mitano, kumi ijayo, inawezekana sheria hii itakuwa *valid* na kwamba, Rais wa nchi atoe kitu kikubwa kwa wafanyakazi waliofanya mambo makubwa. Sidhani kwamba, kukasimu kwa Waziri ni lazima sana. Mimi naona sheria kadri ilivyo, kwa kweli inaleta heshima nzuri kwamba, tumhusishe mwishoni Rais wetu kwa mambo yote mazito yanayohusu yeye kuyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba tena kuwapongeza Waziri, pamoja na Katibu Mkuu wake, kwa kuleta Muswada huu ambao mimi nauunga mkono moja kwa moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kupata nafasi hii, ili niweze kuchangia Muswada huu muhimu kwa Taifa letu la Tanzania. Naunga mkono Muswada huu kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Kabla sijachangia, nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi, kwa kazi kubwa ambayo ameisimamia katika Wizara hii. Taifa letu lilifanya marekebisho makubwa ya uchumi na kwa kweli kama Wizara ingeyumba, tunge- *fail* katika marekebisho haya kwa sababu asilimia 90 ya uchumi ulihusisha wafanyakazi wa maeneo tofauti. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mary Nagu, alisimama vizuri akaenda sambamba na Sera za Serikali na Dira ya Taifa. Kwa hiyo, ndiyo maana nikachukua juhudi ya kumpongeza kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Muswada huu ni muhimu sana na kwa kweli kuna faida kubwa sana kwa jamii ya Watanzania. Kwa hiyo, sina hofu nao hata kidogo, hasa kwa kuwa umepitia katika maeneo tofauti mpaka leo unawasilishwa hapa Bungeni. Lakini kidogo nitagusia baadhi ya maeneo ambayo nitataka kuyasisitiza tu kwa Wizara hii na kwa Serikali kwa ujumla ili kufanikisha malengo yale ambayo yalikusudiwa kwa dhati kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unasema madhumuni yake makubwa ni kuweka sheria, kanuni, miundo na mifumo ya uendeshaji wa shughuli za kazi. Kitu ambacho tunakijenga katika sheria, tusikiwekee tu sheria, lakini tuwe na utaratibu vile kuweza kukisimamia. Kama tutafanikisha hivyo, kwa kweli mafanikio makubwa ya Muswada huu yataweza kupatikana. Kwa hiyo, nimtake Mheshimiwa Waziri, pamoja na

kwamba, Muswada huu anawasilisha Bungeni, asiweke tu, lakini pia awe na uwezo wa kuusimamia ili kuondoa migogoro na matatizo mbalimbali katika maeneo yetu ya kazi katika Taifa letu hili Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Muswada huu unaelezea kwamba, unazingatia Katiba ya Nchi, matakwa na Mikataba ya Shirika la Kazi Dunia *(ILO),* ambayo nchi hii tumeridhia. Kitu ambacho tumeingiza katika Katiba, tunasema Katiba ndiyo sheria ya Msingi ya Taifa, kwa hiyo, kama kitu tumekiingiza kwenye Katiba, tuhakikishe kwamba, haki inayostahili kwa wananchi inapatikana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, suala la Katiba linawagusa wananchi na kitu kama unakiingiza katika Katiba, inabidi ukiangalie kisiwe na kasoro. Mfano hai, wananchi ukiwaambia kitu hiki kimo ndani ya Katiba ni kwamba, wanajua ni haki yao na ni sahihi katika kuisimamia na kuipigania. Mfano sahihi ni juzi tuliona Shirika la Ndege la Afrika Kusini, walipojaribu kutumia Wimbo wa Taifa wa Tanzania katika matangazo, wananchi wetu wali-*complain* na wakalalamika vibaya sana. Kwa hiyo, kitu ambacho kiko kwenye Katiba, tuangalie kama ni haki za kiasi gani wafanyakazi hawa wanastahili wazipate, kama ni masomo na mambo mengine na mazingira mazuri ya kazi. Kwa hiyo, ndiyo pale niliposisitiza sheria hii lazima iwe na usimamizi mzuri na wenye kuleta faida na mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikiendelea zaidi katika sehemu ya pili ya Muswada huu, inahusu haki na tija ya msingi ya jamii. Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri, katika Muswada wako umesema ajira kwa watoto na ajira za masharti ya shurti kulazimisha na ubaguzi katika ajira, katika misingi mbalimbali inakatazwa. Maeneo hayo matatu, naomba utakapokuja ku-*wind up,* hili suala la ajira kwa watoto muda mrefu sana tumekuwa tunalisema, je, sasa hivi pamoja na kwamba tumeleta Muswada huu, tumefanikiwa kiasi gani kulidhibiti? Kama tumeshindwa sababu yake ni nini? Je, hizi ajira za masharti ya kulazimishwa ni zipi na je tunazizuia vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine kubwa ni juu ya ubaguzi kazini. Sasa hivi asilimia kubwa ya hali ya uchumi wetu, sekta binafsi zinatawala kuajiri watu. Je, hii tofauti iliyopo baina ya wafanyakazi kutoka nje na wa ndani iko vipi? Je, kama iko tofauti kubwa tutawasaidia vipi wafanyakazi wetu wa Tanzania kama ulivyoleta Muswada? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, hili pia ujaribu kuliangalia kwa mafanikio makubwa. Kwa kweli, nilikupongeza kwa sababu tumerekebisha uchumi, tumekuta migogoro mingi sana kazini. Lakini ukafanikiwa kutatua matatizo hayo. Mfano hai ni migogoro ambayo watu waliostaafishwa kazi wanadai haki zao. Lakini siku hizi walioathirika ni wale watu, lakini Serikali haikuathirika kutokana na mfumo wake. Kwa hiyo, suala kama hili maeneo matatu tuyaangalia vizuri na unisaidie hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu pia ipo sehemu ambayo inaelezea mkataba wa mfanyakazi kuwa hawezi kufanya kazi zaidi ya siku 5 katika wiki. Lakini vile vile ikaelezea zaidi ya saa 45 katika wiki, lakini pia lingine nililoligundua ni kwamba, pia mfanyakazi hawezi kupata zaidi ya saa 10 ya *overtime* kwa wiki. Je, Mheshimiwa Waziri, kwa wale ambao itatokea wanafanya kazi zaidi ya maeneo hayo matatu, pengine atafanya kazi zaidi ya siku 6, Jumamosi na Jumapili atatakiwa aende

kazini, atafanya kazi zaidi ya saa 45 kwa wiki au *overtime* zaidi ya saa 10, je, hawa watu unawafikiria vipi?

Kwa sababu tunaamini baadhi ya masekretari katika Ofisi za Mawaziri au wakubwa wengine, wanafanya kazi zaidi ya saa za kawaida, kama alitakiwa amalize saa 9 au saa 11.00 lakini hufika mpaka saa 2.00 usiku, hawa wanafaidika vipi na Mikataba hii? Au tuchukulie kama yale maeneo aliyozungumza Mheshimiwa Jackson Makwetta kwamba, askari polisi akipelekwa *traffic* kwake inakuwa ni *priority*. Sasa kwa kuwa yeye ni Sekretari wa Waziri, kwa sababu anaogopa kuondolewa, anavumilia tu zile haki nyingine za msingi ambazo zimezidi ule muda wake wa kazi uliopangwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, hili jaribu kuliangalia ili haki iwe inapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nilizungumzie kwa kweli sasa hivi asilimia kubwa ya uchumi wa Taifa letu inategemea watumishi katika maeneo mbalimbali. Kunapokuwa na migogoro katika maeneo haya ya watumishi, tunaweza tukalifikisha Taifa mahali pa kuligawa. Kwa hiyo, ninataka Wizara hii ambayo kwa kweli ndiyo msingi wa Taifa letu, iangalie hili, kwa sababu kama wananchi watakuwa wanalalamika, wananchi wetu watataka kudai haki zaidi juu ya jasho lao, inaweza ikatuyumbisha na ikatuondoa katika ile *site* ambayo tumekusudia kwenda.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, kwa muda wote ambao tunalalamika, uchumi wa wananchi umeweza kusimama vizuri na wa Serikali. Kwa sababu vinginevyo matatizo wanayopata walimu ni makubwa. Mimi hivi karibuni nilikuwa katika benki moja ya *NMB* Dar es Salaam, niliwaonea huruma walimu ambao walikwenda kuchukua mishahara yao. Kwa bahati siku ya pili nilisoma gazeti nikakuta kwamba, baadhi ya walimu walipoteza fahamu pale. Wakaenda kwenye akauti zao hamna fedha zilizoingizwa baadaye wakatakiwa wakae foleni. Kwa hiyo, naiomba Serikali ikusaidie kwa haya na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa alipokuwa anaeleza madeni ya walimu wa Mkoa wa Mwanza ni mabilioni mengi sana ya fedha. Tuliangalie Taifa litafanya nini. Lakini sisi ni wanachama wa Shirika la Kazi la Duniani *(ILO)*, mashirika kama haya ya Kimataifa yanatusaidia vipi ili kumaliza matatizo mazito kama haya ya wafanyakazi wetu ambao kwa kweli ni mzigo mkubwa kwa Serikali? Hata kutuombea misaada kwa *IMF, World Bank* na mashirika mengine ya Kimataifa. Hatuwezi tu, jamii inategemea maisha ya hapa hakuna hata mfanyakazi mmoja ambaye hana zaidi ya watu 10 na kuendelea wanaomtegemea akiwemo yeye mwenyewe, atakuwa na mke na watoto, pia na familia nyingine inamtegemea, hata marafiki ambao wote watategemea mshahara huo. Kwa hiyo, tusiseme tu katika mafaili yetu, kwenye Mikataba yetu, tusiseme tu kwenye Miswada yetu, lakini pia tuwe na kazi kubwa ya usimamizi, wala Serikali isikae kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesimama hapa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na kumwonyesha kwamba, sina wasiwasi na *package* iliyomo katika Muswada huu, ime-*cover* kila sehemu wala sina wasiwasi, ajira za watoto, watumishi huajiriwa bila ya ridhaa yao na maeneo mengine. Kwa hiyo, cha msingi kwa sababu nimegusa hasa sehemu ya Katiba, naomba elimu hii ya Muswada ifikishwe kwa watumishi wote wa Serikali, isiishie tu humu kwenye Muswada au kwa wachache ambao wako Serikalini,

lakini wafanyakazi wa kawaida wa chini hawafahamu haki zao na taratibu nyingine ambazo zinaweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namalizia kwa kumpa pole sana ndugu yangu Mheshimiwa Bujiku Sakila. Nilikuwa nawasiliana naye katika simu kwa muda mrefu sana akiwa yupo Bugando Hospital na leo nimefurahi sana kumwona hapa. Wakati nikienda Wizarani nilikuwa nawasiliana na Waziri wake na alikuwa ananipa matumaini. Tunamtakia mafanikio mema na maisha mazuri, yenye kheri na baraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiye alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu. Saa 10.00 jioni tutakutana, watakaochangia wako kama watatu au wanne. Kwa hiyo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka Saa 10.00 jioni.

*(Saa 6.52 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie Muswada uliopo mbele yetu katika kazi za mchana nikiwa mchangiaji wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kueleza niliyonayo katika kuchangia, napenda niunge mkono Muswada huu mia kwa mia. *(Makofi)*

Kutokana na kuunga mkono Muswada huu, napenda basi nimpongeze Waziri na wataalam wake katika Wizara, kwa kuandaa Muswada huu na kuuwasilisha mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia Muswada huu, napenda niseme kwamba, Muswada huu naona umechelewa kulingana na uzuri au mahitaji yaliyotakiwa kuwa yamezingatiwa. Naweza kusema umechelewa kwa sababu utumishi wa umma ni wa muda mrefu tangu tulipopata uhuru karibu miaka 40. Kwa upande wa Serikali, Mashirika ya Umma yalikuwa na chombo angalau Mabaraza ya Wafanyakazi yaliyotokana na agizo la Rais kama Mheshimiwa Waziri alivyokariri hapa katika kipindi cha asubuhi. Agizo la Rais Na.1 la mwaka 1970 lilitoa mwongozo wa kuanzisha Mabaraza ya Wafanyakazi, kwa upande wa wafanyakazi waliokuwa katika Mashirika ya Umma. Lakini kwa upande wa Serikali hicho kitu hakikuwepo. Lakini napenda kuipongeza Serikali kwamba, katika kipindi hiki cha mageuzi ya uchumi, tayari Serikali kupitia Wizara yake, imeandaa Muswada huu ambao ndiyo tunaujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijielekeze katika Muswada kwa kuangalia sehemu zake kuu mbili. Kwanza, ni hii ya kuanzisha Baraza Kuu la Majadiliano ya Pamoja. Hili ni Baraza muhimu sana. Lakini napenda niseme kwamba, kwa kuwa shabaha yake ni kuwezesha utatuzi wa migogoro kama ilivyooneshwa pale, nadhani majukumu yake yaliyoelezwa katika Ibara ya Sita, naona kwamba msisitizo umewekwa

katika kutatua migogoro, lakini nadhani Baraza hili lingeweza kufanya kazi nyingine zaidi ya kusimamia tija.

Katika kifungu (b) imezungumziwa kwa kifupi tu kuhusu ufanisi, lakini nadhani kwa maoni yangu, Baraza hili lingechangia sana kama lingejiingiza katika suala la tija na hili ni tatizo tunalolipata katika utendaji wetu katika Idara mbalimbali za Serikali. Malalamiko tunayoyapata yanatokana na kutokuwa na tija na ufanisi. Sasa chombo kama hiki kingefanya kazi hiyo zaidi kwa kujielekeza katika kusimamia tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho, kazi zilizoainishwa pale, napenda niungane na Msemaji mmoja aliyetangulia mchana, alipozungumzia umuhimu wa mafunzo na hicho kipengele Mheshimiwa Halinga, aliekeleza mafunzo hayo kwamba yawe kwa Watumishi. Nakubaliana naye. Lakini ningependa kuongeza kwamba, mafunzo yanayotakiwa katika kifungu hiki yanapaswa yaelekezwe kwa wadau wote wanaohusika katika utekelezaji wa hii sheria. Wadau hao ni pamoja na wafanyakazi wenyewe. Lakini wapo wasimamizi wa kazi ambao ndiyo hao wapo katika Idara mbalimbali za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wengine ni wale wanaopata huduma zetu. Muswada umeeleza kwamba, kuna mkataba ambao unapaswa ufanywe kati ya watumishi na wanaopokea hizi huduma. Mikataba hii haiwezi kufikiwa kwa ufanisi kama elimu haijasisitizwa katika Muswada huu kwenda kwa hawa ambao wanapata huduma zetu ili wajue watumishi katika kuwahudumia wana mazingira gani, wanapaswa kufanya nini na wao wanapaswa kufanya nini kwa watumishi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wengine ni wale ambao wanatupa huduma nao, watu kama makandarasi. Hawa wanapopewa kazi au wanapo-*supply* vifaa, wanapaswa wajue mazingira ya kutupatia hivyo vifaa na hao wanapaswa hatua kwa hatua elimu iende kwao, wajue taratibu zetu na wajibu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wapo wafadhili wale ambao wanatusaidia katika kutufadhili kwa pesa za kuendesha mradi kama huu. Wale wanataka wajue kwamba, tunaendeleaje. Kwa hiyo, elimu inatakiwa. Tunapotoa taarifa kwao ya jinsi tulivyotekeleza, wanapojua matatizo yetu, hiyo ni elimu. Kwa hiyo, lazima Baraza hili lijielekeze katika suala la elimu. Pengine ni vyombo vya fedha, hawa vyombo vya fedha vinatazamiwa viingie katika suala la mikopo. Vyombo vya fedha vinapokea mishahara ya walimu na kadhalika na tumesikia matatizo yanayowapata walimu na watumishi wengine hasa walioko katika Vijiji. Je, elimu hii hivi vyombo vya fedha vitaipata wapi kama Baraza la namna hii halitajielekeza katika kuimarisha suala la elimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wengine ni haya mashirika yasiyo ya Kiserikali. Haya yanatoa huduma ndani ya jamii lakini je, suala la elimu ya kuyaunganisha haya yote liko namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili suala la elimu kwa kweli ni kazi ambayo kwa maoni yangu, lingetakiwa ionekane chini ya hicho kifungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda niligusie ni ibara ya 12. Hii ibara inasema, inapotokea kuna kutokukubaliana katika utendaji wa hili Baraza, basi Baraza hilo Mwenyekiti au Makamu wake anapeleka ripoti kwa Waziri. Imeoneshwa wazi wazi pale kwamba, ni lazima aisaini yeye au Makamu wake lakini ile nyongeza iliyooneshwa pale au wale waliowateua kufanya ile kazi, mimi naona kama tulivyokuwa tunazungumza katika Miswada iliyopita kwamba, kuongeza kipengele kama hicho ni kuifanya sheria ichezewe. Hawa wana jukumu na tumeoneshwa pale kwamba, huyu Mwenyekiti ni mteuliwa wa Rais na siyo mfanyakazi na wala hatoki kwenye vyama vya wafanyakazi. Sasa kama hivyo ndivyo, watawapa kazi hii watu gani katika lile Baraza? Hawawezi kuwapa wawakilishi wa wafanyakazi, vinginevyo watawapa wa Serikali. Lakini hawa tumesema wanapaswa wawe ni watu tofauti, sasa unapowapa nafasi ya kuwakaimu watu wengine kuandika na kusaini hiyo ripoti, nadhani siyo kitu kizuri. Ni vema katika kuhakikisha sheria hii ina uzito, inapotokea suala la mgogoro ambao umeshindikana kutatuliwa pale, hao ndiyo wampelekee taarifa Mwenyekiti na Makamu wake na imesemekana ni wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilidhani linapaswa liangaliwe ni lile la ibara ya 15. Tunaposema suala linapelekwa kwenye Mahakama, sasa kama limepelekwa kwenye Mahakama sitarajii kwamba, Mahakama itamwandikia Waziri ripoti. Mahakama ninavyotarajia itapitisha maamuzi. Sasa ni katika kuliona hivyo kwamba, Mahakama inapitisha maamuzi na maamuzi hayo kisheria yanazingatia sheria, yanapaswa yaheshimiwe. Kwa hiyo, sitarajii kwamba, Waziri ataandikiwa ripoti na Mahakama ya Kazi kwa sababu hicho ni chombo cha maamuzi yanayozingatia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara ya 27 ambayo inahusu Baraza Kuu la Wafanyakazi, hapa naona kuna kipengele kimoja muhimu sana ambacho hakikuainishwa, kazi mojawapo ambayo inapaswa ifanywe. Hili Baraza la Wafanyakazi, linapaswa lijadili malengo ya mipango na malengo ya maeneo yao ya kazi. Kwa sababu ni mipango hii ambayo inawawezesha kupanga maslahi ya wafanyakazi. Sasa kama chombo hiki hakikusimamia hayo, Baraza la Wafanyakazi halijadili malengo hata namna ya kufikiria kuwapandisha watu vyeo na kadhalika inakosekana. Ubunifu pia ambao unatakiwa utokane miongoni mwa wafanyakazi hauwezi kuonekana kama Baraza la Wafanyakazi halina utaratibu wa kujadili malengo na mipango ya maendeleo. Kwa hiyo, nadhani hapa ni suala ambalo lingepaswa kuangaliwa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lipo suala la kumhusisha Rais katika kutoa maamuzi. Mimi nadhani kwa sababu tumejiundia chombo cha sheria na kuna Mahakama ya Kazi, hicho chombo ni lazima kifanye kazi kwa sababu ni chombo cha Rais cha Utekelezaji. Haitazamiwi tena kwamba, Rais ndiye apelekewe hizo kazi. Tukumbuke pia Mashirika ya Umma nayo yana taratibu zao pamoja na kwamba, yale yamekuwa yakitumia lile agizo la Rais la mwaka 1970, hakuna sheria iliyoundwa, lakini itakapokuwa imeundwa, kwa sababu bado Mashirika yapo, itakapokuwa imeundwa, hayo Mashirika nayo yakilazimika kubadilisha sheria ili Rais atoe maamuzi, tutakuwa tunampa

mzigo ambao ni zaidi ya shughuli ambazo inapaswa zifanywe. Vyombo vyake nadhani ni vyema vikafanya kazi na ni vyombo ambavyo ni madhubuti, napenda iwe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tena kwa kumshukuru Mheshimiwa Dr. Mary Nagu wa Wizara hii kwa kutuletea Muswada huu mzuri mbele yetu, namshukuru sana. Ahsante sana.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii uliyonipa na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu, Muswada wa *The Public Service Negotiating Machine.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, kwanza nitumie nafasi hii kutoa rambirambi kwa wananchi wengi waliopoteza maisha yao zaidi ya 30 kwenye ajali ya *bus* iliyotokea Arusha - Moshi. Inasikitisha sana kwa sababu jana hiyo hiyo imetokea tena ajali nyingine mbele kidogo ya hapo sehemu ya Bomang'ombe ya lori la wafanyakazi wa Idara ya Maji na likaua watu wengine wanne na wengine wako Hospitalini! Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kutoa rambirambi kwa niaba ya Jimbo la Moshi Vijijini na kwa niaba yangu mwenyewe. Mungu azilaze roho yao mahali pema peponi. Amina.

**WABUNGE FULANI:** Roho zao.
**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Roho zao. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina machache kuhusiana na Muswada uliopo mbele yetu. Migogoro mingi inayotokana na wafanyakazi kazini inasababishwa na sheria kukosa meno. Sheria zinakosa meno, wafanyakazi wengine wanaoajiriwa wote wanakuwa na sharubu kama kambale mamba, kwa hiyo kila mmoja ni bwana mkubwa. Sasa inapotokea hivyo, akija mwingine anasema mimi bwana mkubwa, mwingine anasema bwana mkubwa, sasa amri zinatoka sehemu mbalimbali na matokeo yake inakuwa ni ukorofi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukorofi mwingine ni maslahi. Nizungumzie ugomvi ambao ulipelekea mpaka walimu wakaunda Chama cha Walimu. Kwa sababu hapakuwa na sababu watumishi wa Serikali kama walimu waunde Chama chao cha Walimu. Ni baada ya kuona kwamba, hawatendewi haki na wamedharauliwa na ni utumishi huo huo ambao unapaswa kuangalia mambo kama haya ili migogoro isiwepo. Utakuta mwalimu aliyeajiriwa Shule ya Binafsi, analipwa mshahara kuanzia shilingi laki mbili mpaka tatu. Lakini mwalimu anayeitumikia Serikali na ana vyeti vyake amesoma mpaka Chuo Kikuu, unakuta analipwa Sh.80,000/= au Sh.90,000/=, hakuna nyumba, nauli, wala chochote. Sasa unategemea huo mgogoro utaacha kuwepo? Huo mgogoro utakuwepo na Serikali inajua hilo.

Shule za watu binafsi kwa mfano, sasa hivi ziko nyingi zinashindana na za Serikali, lakini mishahara ya binafsi ni mikubwa kuliko mishahara ya Serikali. Tulikuwa tunatarajia kwamba, mishahara ya Serikali iwe mikubwa na ya binafsi ndiyo iwe midogo.

Sasa imekuwa kinyume. Kwa hiyo, nilitaka Waziri atueleze kwamba, sheria inasaidiaje hapo kuhusu maslahi ya wafanyakazi ambalo ni jambo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, najielekeza kwenye tuzo ambazo Rais anatoa. Tuzo hizi zinatakiwa kuangaliwa kwa makini. Nitatoa mifano. Kuna tuzo zilizowahi kutolewa kwa viongozi fulani wa *National Milling,* sitaki kuwataja majina na tuzo nyingine zilitolewa kwa *custom officer* aliyekuwa amekamata dhahabu. Lakini baadaye wakaja kuona kwamba, wametoa zile tuzo kwa makosa, kwa hiyo zile tuzo ikalazimu kufuta, lakini *already* Rais alishatoa tuzo kwa hawa watu! Sasa najielekeza huko kwa sababu kuna tuzo walipewa Mapolisi kule Zanzibar, kwa ajili ya kuua wale walioandamana huko. Nashukuru Muafaka umepita, lakini wakapewa tuzo siku ya pili yake bila tafakari! Tulikuwa tunashauri kwamba, mambo ya tuzo ni mambo mazito. Rais anakupa tuzo mtumishi bora, mtumishi mzuri, inatakiwa umakini zaidi. Inatakiwa Mabaraza haya ya Wafanyakazi yafanye tathmini ya huyu mtu anayetakiwa kupewa tuzo halafu ile tathmini wapeleke kwa Waziri halafu Waziri apeleke kwa Rais. Kwa hiyo, Rais anapokuja kuamua anaamua kitu ambacho kinakubalika na watu wote, wala hawezi akakosea tena. Kwa hiyo, ningeshauri mambo ya tuzo yaanzie chini halafu ndiyo Rais apewe taarifa na watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde kuna watu wanaongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu mikataba ya kazini, nayo ni mojawapo ambayo inaleta migogoro. Sasa hivi huu ubinafsishaji, wanafukuza wafanyakazi, wanaajiri kwa mkataba wa kibarua. Halafu na wala wa *permanent* wanaajiri watu wao. Yaani utakuta wengi sana ni wa Kenya, *South Africa* ndiyo *permanent.* Sisi Watanzania wenye mali zetu tunaajiriwa kama vibarua ili siku ya kufukuzwa tusiwe na haki. Sasa mambo kama hayo, mikataba ya namna hii, kwa sababu mtu anasaini mkataba aiwa na njaa, hawezi kukataa kwa sababu anaona watu wote wanakubali, hawezi kukataa. Lakini siku ya siku wanajiunda tena wanasema hebu tugome hili jambo, tuligomee haiwezekani, wanagoma. Ningeomba sheria hii iangalie chanzo cha migogoro inatoka wapi? Hivi ni vyanzo vya migogoro, watumishi hawapati haki zao wananyanyaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili la wizi katika Serikali wa fedha za umma zinapotea, hawajaliangalia, kumbe pesa hizi zinaibiwa kutokana na matatizo ya Serikali yenyewe. Serikali imeacha mwanya, watu wanachukua pesa. Nitalitolea maelezo.

Utakuta *Accountant General*, yeye ni msimamizi wa fedha yote. Lakini unakuta tena kuna *Auditor General* na yeye anasimamia watu wake kila mtu na nyanja yake. Lakini hana uwezo wa kumkabili aliyeiba fedha, hana madaraka. Hana hata madaraka ya kumfukuza, hana hata madaraka ya kumsimamisha kazi. Lakini kikazi ni msimamizi wake. Kwa hiyo, kuna mifano mingi kabisa ambayo wafanyakazi wameiba hela, badala ya kufukuzwa au kukemewa na mabosi wao, kwa sababu wanawajibika kwenye utumishi wanajua mtu atakayetukemea si Afisa Utumishi bwana, wala siyo huyu ambaye ananisimamia. Kwa hiyo, labda na yeye anahamishwa tu. Lakini kwa yule *Accountant General,* labda asingependa ahamishwe, angependa afukuzwe kwa sababu ndiye

anayejua *in and out* ya yule mtu. Lakini Wizara inasema hapana, asiwajibike kwa *Accountant General* ila awajibike kwa Afisa Utumishi. Lakini ile *profession* yake ambayo ndiyo inampa kibarua pale, eti bosi wake haruhusiwi kumwadabisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya mambo matatu niliyoyasema, kwa kweli na Mheshimiwa Lukuvi, ambaye nimeona ananiingilia ninapozungumza ataona kwamba hoja hizi ni za msingi kabisa. Huwezi kuwa *Accountant General,* ambaye huwezi kuwakabili watu wako. Fedha yote umekabidhiwa, lakini kumkabili anayekuibia fedha huna uwezo, *Auditor* hana uwezo, anapendekeza tu! Sasa haya mambo yarekebishwe ili migogoro na nidhamu iweze kuwepo kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushahidi, unakuta mwajiriwa ananyanyaswa. Anaponyanyaswa anakwenda kwenye Mabaraza ya Kazi. Anapofika kwenye Mabaraza ya Kazi labda wanampa haki, wanamwambia urudishwe kazini kwa sababu umeonewa. Anakwenda na barua yake kazini anaambiwa tuna-*appeal* kwa Waziri. Wana-*appeal* kwa Waziri, Waziri anaangalia *merits* zake, anaandika kwamba, huyu mtu arudishwe kazini, lakini mtu huyo huyo tena haheshimu hata saini ya Waziri, anasema nitakwenda Mahakamani. "Mimi siheshimu hii saini ya Waziri." Sasa Serikali gani? Haya mambo yapo na nina Ushahidi nayo. Mtu anathubutu kusema sijui habari ya Waziri, mimi nitakwenda Mahakamani. Amekataa yale Mabaraza, amekataa ya Waziri, anamtesa yule, sasa migogoro itaachaje kuwepo?

Kwa hiyo, haya mambo tuyaangalie. Kama tumekuwa na madaraka, kama mimi ningekuwa Waziri, mtu wa namna hiyo saa hiyo hiyo nasema akae ndani kwanza siku nne. Namfunga. Halafu namwambia sasa nenda katekeleze adhabu yako kule kwa nini unamdharau Waziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hayo mambo yote nasema kwamba, ni mambo yanayoharibu sifa ya utumishi, ambayo kwa kweli wakitengeneza masuala haya vizuri, ninaamini kwamba, migogoro itapungua na vile vile wafanyakazi watakuwa na kazi zao na hata Waziri atakuwa ame-*relax* hatapata kesi nyingi ambazo nilikwenda siku moja Ofisini kwa Waziri nikakuta mafaili yamejaa, hata Mahakamani hayako mengi namna hiyo. Kwa hiyo, itapunguza kesi ambazo ziko kwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Haya nashukuru. Waheshimiwa Wabunge, tujielekeze kwenye hoja zaidi. Mheshimiwa Profesa Mbilinyi.

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niseme machache tu kuhusu hoja iliyopo mbele yetu. Awali ya yote, nawapa pongezi nyingi kwa kufanya kazi nzuri. *Paper* ya hoja ni fupi lakini ina kila kitu ndani. Pamoja na mapungufu ya hapa na pale, lakini wanayotaka kusema wameyasema kwa ufasaha. Kwa hiyo, nawapa hongera kwa hilo. *(Makofi)*

La pili, hoja hii inahusu makundi mawili, mwajiri na mwajiriwa. Kwa hiyo, tutaweza kuongea hapa muda mrefu, lakini kitu kikubwa ni kuwa lazima kuwe na imani, kila mmoja awe na imani na mwenziwe. Anayetaka kuajiri awe na imani na anayetaka kumwajiri na yule anayetaka kuajiriwa naye awe na imani na chombo kile kinachotaka kumwajiri. Kwa hiyo, ukiwa na hiyo, inatakiwa kuwa kama inawezekana, pamoja na hiyo hoja ya leo kuna haja ya kuwa na mazungumzo kati ya mwajiri na waajiriwa *continuously,* yaani siyo lazima uwe mgomo tu, hapana.

Wawe na vipindi wanakutana kuona kama kuna *improvement* gani wanaweza kufanya katika *terms and conditions of service* kusudi wasiende kwenye mgogoro wa kwenda kwenye Mahakama, kwenye usuluhishi kwa kuwa tunasema kila mmoja anaomba kazi *individually,* lakini baadaye wale wote wanakuwa ni watumishi wa Serikali. Sasa kama vyombo vipo, labda wawe wanaongea *continuously* kuhusu *terms and conditions* za wale wafanyakazi. Kwa hivi sasa sina uhakika mishahara tunayopata kwa ngazi mbalimbali kama inatutosha kwa wiki ngapi katika mwezi. Nadhani wengi wanaopata kiasi cha Sh. 80,000/=, Sh.60,000/=, labda itatosha kwa wiki mbili au wiki tatu. Baada ya hapo sijui wafanye nini. Kwa hiyo, hicho ndicho kitu ambacho inatakiwa mwajiri, Serikali na mwajiriwa, *civil servants,* wawe na chombo cha kuongea au utaratibu unaweza ukawekwa katika hoja hiyo hiyo, kwa hiyo wataweza kukutana na kuzungumza mara nyingi.

Pili, nilitaka kuzungumzia juu ya maslahi au *terms and conditions of service* za *civil servants*. Nadhani *comprehensive review* ya hizo zilifanywa na Mr. Adu, kutoka Ghana kule. Mtaalam mmoja alikuja *in the 1960s*, nadhani baada ya Mkoloni kuondoka tu tulimwalika huyu. Huyu ndiye alifanya *comprehensive review* ya *civil service* yote, pamoja na *conditions of employment.*

Tangu wakati huo nadhani tumefanya tu vipande vipande, *half pieces* hapa na pale. Marehemu Mzee Mulokozi, alifanya moja, Mheshimiwa Shellukindo naye alifanya, halafu wengine imekuwa *Ad-hoc,* kama mishahara ya Makatibu Wakuu imefanywa bila *review* yoyote, wakaahidiwa wenyewe, sijui waliipitisha wapi? Lakini wao wamejitengenezea mambo yao yakawa safi. Lakini sio utaratibu hasa unaotakiwa uwe wa Kiserikali na watumishi wa Serikali. Nadhani kuna haja ya kuwa na *review* nyingine ya *terms and conditions of service* kama aliyofanya Mzee Adu mwaka ule wa sitini na kitu, kama hili tukiweza kufanya labda tutaona *gaps* kuwa ni nyingi sana. Moja ya *gap* kubwa kabisa ni wakati ule tukilipwa kwa *pounds*.

Kwa hiyo, unaambiwa unapewa *three hundred and thirty pounds per year,* ilikuwa ndogo sana. Lakini mahitaji yako yote yanakwisha, nguo na vitu vingine, kila kitu kwa mia tatu tu na thelathini na wakubwa kabisa wakipata 760 *pounds per annum,* sio kwa mwezi kwa mwaka. Lakini leo *pound* ile wakati ule ilikuwa shilingi 20 siku hizi nadhani *pound* imekuwa sijui Sh. 1,800/= na ngapi na ambayo uzito wake na bei ya *tray* ya mayai ni tofauti. Kwa hiyo, haya yote yangeweza kufanyiwa uchambuzi na watu wakawa na *real salary,* ambayo ina-*reflect* hali halisi ya uchumi wa nchi katika muda fulani. Nadhani hiyo ingekuwa kitu kikubwa kama tutashindwa kulipa lakini ijulikane

kuwa kwa kweli mtu mzima na familia yake si vizuri anahitaji kitu kiasi hiki. Serikali haiwezi lakini itampa kiasi kadhaa.

Halafu ya tatu, nilifikiria kuwa, tulifanya *exercise* hiyo mwaka 1996, ambayo ilikusanya malupulupu yote, *allowances,* kufanya *salary* iwe nzuri na pia *retirement benefit* iwe nzuri zaidi. Sasa tangu wakati ule nadhani hatujafanya tena. Sasa naona kuwa kama *allowances* hizi zinaanza kurudi tena kidogo hapa na pale na kadhalika. Hii inaonyesha kuwa kuna haja ya kufanya hiyo *review.*

Halafu ya mwisho kabisa, nilidhani inanitisha ni kuwa ile *Civil Service Reform* awali kabisa tukasema kuwa tusiajiri tena, tulikubaliana na wahisani kuwa tusiajiri. Kulipigwa *stop* kuajiri, halafu baadaye ikabadilika kuwa *warning* kutoka Utumishi, kwa Mheshimiwa Dr. Nagu, itoe kibali kuajiri watu. Sasa hiyo nayo pia imeleta *distortion* kubwa sana katika uchumi hasa katika ajira. Huwezi kuwa una Universities, High Schools, *Technical Schools* na *Colleges* na kila mwaka unazalisha wasomi, halafu useme kuwa hawa wasomi wasiajiriwe, wakae tu kijiweni! Tusingeona uchumi kama huo popote. *(Makofi)*

Sasa tuna vijana wa *High School* wanatembea tu mpaka viatu vinakwisha. Vijana toka *University* nao wanaanza kuwa wengi hawana kazi na *Civil Service* yetu haipanuki, ingawa inapanuka kwa *Institutions* lakini watu hawaajiriwi. Nadhani kuna haja ya kusema mahali kuwa sisi tutaajiri angalau *sixty or seventy percent* ya wale wanaomaliza mwaka ule ili angalau tusiwe tunapoteza hela ku-*train* watu na baada ya kuwa-*train* wanakaa tu mahali au wanatembea tu kutafuta kazi. Kwa hiyo, tunaweza kulifikiria hilo katika *reform* kuwa tuwe na ajira, tuwe na Sera ya Ajira ikitilia maanani *limits* zile za fedha ambazo zilikuwa ni matatizo kwa wakati ule.

Kwa hiyo, nilidhani kuwa nichangie hayo machache, mengi wameshasema wenzangu na mimi nimekuwa wa mwisho mwisho, nilisema kuwa sitoi mchango, yote hiyo ni katika kuboresha hiyo hoja, kuboresha Muswada ili uwe mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema naunga mkono hoja ya Waziri, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, mia kwa mia na ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nichangie angalau machache. Kwanza, niipongeze Kamati inayohusika kwa jinsi ambavyo imejitahidi kutetea kifungu Namba 6, kifungu kidogo cha 6 cha Sheria Na.8 ya mwaka 2002, ambacho kilifutwa kwamba Halmashauri isiwe na mamlaka ya kutoa ajira na badala yake alipewa Mkurugenzi kutoa ajira hiyo.

Naishukuru Kamati kwa kutetea kifungu hicho. Lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa sababu kimsingi amekubaliana na hoja hiyo na kwamba, inaelekea sheria hiyo itabidi irudishwe tena Bungeni ili Halmashauri wenyewe ndiyo wapewe uwezo wa kuajiri badala ya *DED.* Mimi nakushukuru Mheshimiwa Waziri, lakini nilikuwa nakuomba ujitahidi kuleta mabadiliko hayo mapema takriban mwanzoni

mwa mwezi wa kwanza ili sheria hiyo iweze kufanya kazi kwa mamlaka ya umma zaidi. Naomba nikupongeze sana kwa hilo Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Jambo lingine ni kwamba, unaposema Serikali, mara nyingi kumekuwa na utata wa kuelewa ni nani Serikali, maana Kiserikali wote ni watumishi. Ukija kwa upande wa waajiri, kwa maana ya Serikali, wapo waajiriwa ambao wana mamlaka ya utawala na *management* lakini wapo watumishi wa kawaida ambao wanaisaidia *management,* pamoja na utawala wenyewe. Sasa unasema nani ni Serikali, ni wale wenye kutoa maamuzi ya juu au nani na wafanyakazi ni nani? Lakini unakuta wote ni wafanyakazi na wote ni Serikali.

Tatizo linalojitokeza hapa ni ile kada yenye kutoa maamuzi kujiona wao ni wa juu zaidi na kwa hiyo, wanafikia mahali wanaanza kuwanyanyasa watumishi wa kawaida. Hata watumishi wa kawaida ambao kwa ujumla ndiyo wengi na ndiyo watenda kazi, wanapojaribu kujijitea, hawa wenye kutoa maamuzi, wanakuwa wagumu. Pale ndipo migogoro inapoanza na bahati mbaya sana, hawa wenye kutoa mamlaka hutoa vitisho, kwa hiyo Serikali inaonekana ndiyo inayotoa vitisho. Lakini Serikali ni nani basi? Serikali ni wote. Maana kama wewe ni mtumishi wa umma, yule mwenye kutoa maamuzi ya mamlaka kwenye *management* na utawala na hawa watumishi wa kawaida wote chombo hiki ni chombo chetu. Kwa hiyo, kuletwa kwa sheria hii naona ni vizuri, kwa sababu kunakuwa na chombo kinachowaunganisha wote wawili sasa waweze kujadili badala ya mmoja huyu kuonekana yeye ni mlalamikaji tu na mwingine ni sugu tu. Matokeo yake migogoro inatokea kazini, kugoma kunakuwepo na watu wengine wanaweza kupoteza haki.

Katika kuunda chombo hiki, kubwa ninaloliona ni vizuri mwajiri ajitahidi kutimiza wajibu wake kikamilifu na pia mwajiriwa naye ajaribu kutimiza wajibu wake kikamilifu na hapa ndipo tunapojenga uzalendo kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla. Lakini kama mwajiri atashindwa kutimiza wajibu wake na mwajiriwa atashindwa kutumiza wajibu wake, tatizo kubwa hapa linatokea. Naweza nikatoa mfano wa Mwalimu, kama mfano. Mwalimu usipomtekelezea haki zake na kwa sababu yeye atasema mimi naiogopa Serikali, mimi ni mnyonge, anaweza akaweka mgomo baridi wa kutowafundisha watoto, anakwenda shuleni lakini hawafundishi watoto ipasavyo. Matokeo yake elimu inashuka chini kabisa na kwa hiyo kiuchumi na kijamii, inakuwa mnalijenga Taifa ambalo halina uzalendo. Kwa hiyo, ndipo ninaposema ni vizuri mwajiri kwa maana ya Serikali, kwa maana ya wale wanaosimamia utawala na *management* na watumishi wa kawaida, wawe ni kitu kimoja, watimize wajibu wao wote kwa pamoja.

Nikija kwa upande wa kuunda vyama huru, mahali pengi watumishi wamelalamika au kutetea kwamba, wakifika hata 20 pengine wawe na vyama vyao huru. Ushauri mwingine ukatolewa angalau 30, wengine wakang'ang'ania 20. Mimi naona busara inakosa kutumika zaidi kwa sababu kukiwa na utitiri wa vyama inawezekana pia haki isipatikane. Vitakuwepo vyama na mnaviita ni huru, lakini vimegawanyika vyama hivi, chama hiki na mambo yake na kile na mambo yake. Haya siyo ya umoja tena. Kwa hiyo, inapofikia mahali ambapo mnataka mkubaliane katika jambo fulani, inawezekana

pia hata huyo anayeitwa Serikali akapata tatizo. Maana inawezekana hata wao wakaanza kugombana, hawa wanakubaliana hawa hawakubaliani.

Kwa hiyo, utitiri ingawa tunaita ni uhuru wa vyama, bado utitiri huo wa vyama vyenyewe, unaweza ukawasababishia watumishi hawa wasipate haki zao. Kwa hiyo, nasema ni vizuri busara ikatumika kwa watumishi wahusika, mahali walipo, wasiwe na utitiri wa vyama. Ukitazama hata vyama vya siasa vikiwa vyama vingi vyenye utitiri, kunakuwa ni kero. Kunakuwa ni tatizo. Vingine vinagombana, vingine vikitaka kuungana vingine havitaki. Vingine dakika ya mwisho vinagongana. Kwa hiyo, ni tatizo. Katika nchi nyingi imetokea hivyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, watumishi hawa watumie busara, wasiwe na vyama utitiri ndugu zangu. Wakiwa na vyama utitiri watakwama na wanisikie mahali popote walipo maana yake na kuna sheria nyingine zinakuja, wao wanang'ang'ania utitiri wa vyama, wanakuwa huru, watakuwa na uhuru usiokuwa huru. Maana watagombana, hawatapatana na bado huyu wanayetaka kum-*attack* ili awasaidie, ili awape haki yao, hataweza kuwapa haki yao kwa sababu inawezekana kabisa huyu mkubwa mnayemtaka, ataamua kununua baadhi ya vyama vidogo vidogo, akawa nao na wakawasumbua, haki yenu haipo. Kwa hiyo, Sheria juu ya Sheria ikawa haipo. Mimi nilikuwa nashauri hawa wafanyakazi wasing'ang'anie kuwa na utitiri wa vyama, wawe na vyama vichache vyenye watu wengi, ili wawe na nguvu ya pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la *Bunge Service Commission* tunayo hapa. Mimi nilikuwa naomba tu wapate elimu, hawa *Bunge Service Commission* wenyewe watakuwa wapi? Je, wanajitegemea kwa maana kwamba, yaani wanaweza kuruhusiwa kugoma? Eee! Tumekuja hapa Bungeni, tunataka kufanya shughuli za Bunge, hatuwatendei haki, tunang'ang'ania haki zetu tu kama Wabunge na wao wapo. Je, wao chombo chao hicho kinakwendakwendaje, kiko katika mfumo huu au hawapo na wao haki zao zinaweza zikawa vipi wakitaka kugoma ili mambo yetu yakwame? Mimi nilikuwa naomba kulifahamu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, si kawaida yangu, leo nimeishiwa maneno, kwa sababu ya Muswada wenyewe ni mzuri, naomba kuunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuendesha kikao hiki cha Bunge lako Tukufu, kwa namna ambayo imeniwezesha kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma. Aidha, ninapenda kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa shukrani za pekee kwa Waheshimiwa Wabunge wote, waliochangia kwa kusema na kwa maandishi kuhusu Muswada huu. Napenda vile vile kurudia shukrani zangu za dhati kwa Kamati iliyoupitia Muswada huu na kutoa taarifa yake hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa watumishi wa umma kama kiungo katika kukuza uchumi wa nchi hii, ni suala ambalo liko wazi na lisilohitaji mjadala. Vile vile inafahamika wazi kwamba, ni kundi maalum lililoshikamana. Kwa hiyo, siyo kundi la kuchezea. Hivyo, ni rahisi kutoa ujumbe kwao na ukaeleweka kwa urahisi kuliko katika kundi lingine lolote au hata usieleweke. Ninapenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba, kazi yetu kubwa baada ya Bunge kupitisha Muswada huu itakuwa kuwaelimisha wafanyakazi wote kuhusu wajibu na haki zao na namna ya kuzipata.

Vile vile Serikali kwa upande wake, itawajibika kuhakikisha kuwa inatengeneza mazingira mazuri kuwawezesha wafanyakazi kufanya kazi zao kwa utulivu. Muswada huu basi umewasilishwa katika Bunge lako Tukufu kwa lengo la kuboresha zaidi utoaji wa huduma kwa wananchi kwa kuzingatia dhana niliyoitaja hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kutoa shukrani kwa watumishi wa umma, wakiwemo Walimu, kwa uvumilivu waliokuwa nao katika kipindi chote ambacho hawakuwa na fursa kuweza kujadili maslahi yao kupitia mfumo uliokuwepo. *(Makofi)*

Ni imani yangu kuwa sasa watakuwa wamepata fursa hiyo kupitia Muswada huu bila vikwazo vyovyote. Pia ni matumaini yangu kwamba, hawatatumia vibaya fursa hii. Naomba nisisitize kwamba, kuongezeka kwa maslahi ya watumishi, kunategemea sana Pato la Taifa. Kwa hiyo, bila tija kuongezeka ni vigumu kuongeza mishahara na maslahi mengine ya watumishi. Kwani kufanya hivyo, kunaweza kusababisha athari katika uchumi wa Taifa. Athari hizo ni pamoja na mfumko wa bei na kuwepo kwa uwezo mdogo wa kupanua ajira na vile vile uhaba na uduni wa vifaa vya kutendea kazi.

Aidha, Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi pale ambapo tija haiongezeki, ukiongeza mishahara na maslahi utazaa mfumko wa bei ambao utatufanya sisi tushindwe kupanga mipango yetu. Lakini baadhi ya watumishi wenyewe watajipunguzia ajira au kwa sababu kuongeza mishahara kabla mapato hayajaongezeka maana yake ni kupunguza ajira kwa mmoja au kwa wengi zaidi. Kama hivyo viwili havitatokea, basi watakuwemo kazini lakini hakutakuwa na vitendea kazi. Kwa watumishi wa Serikali lazima wafahamu kuwa wao ndio chimbuko la maslahi yao kuwa bora kwa kufanya kazi kwa tija na kwa ufanisi. Nguvu zetu zitaelekezwa kuwaelimisha watumishi wa umma kuelewa hali hiyo ili tuwe na majadiliano yanayolenga hali halisi ya maendeleo ya uchumi na jamii katika nchi yetu. Kwa upande wa waajiri tutakuwa tunakumbushana kila wakati kuhakikisha kwamba, haki inatendeka bila ya hivyo kutakuwa na migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata fursa ya kujielimisha juu ya Muswada huu, kuungana na Serikali katika kuwaelimisha watumishi wa umma kuhusu sheria hii mpya inayotegemewa kutungwa kutokana na Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa napenda kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, waliochangia Muswada huu, lakini kabla sijafanya hivyo, naomba nitambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia Muswada wa Sheria ya

Majadiliano ya Pamoja au *The Public Service Negotiating Machinery Act* ya mwaka 2003. Waliochangia kwa kauli na wale waliochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa kwanza ni Mheshimiwa George M. Lubeleje, Makamu Mwenyekiti wa Kamati iliyoangalia Muswada huu na Mbunge wa Mpwapwa, Mheshimiwa Edson M. Halinga, Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mbunge wa Geita, Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, Mbunge wa Karatu, Mheshimiwa Getrude I. Mongella, Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Abu T. Kiwanga, Mbunge wa Kilombero, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi, Mbunge wa Kyerwa, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mbunge wa Masasi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mbunge wa Chake Chake, Mheshimiwa Edward N. Ndeka, Mbunge wa Kigoma Kusini, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini na Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mbunge wa Nkasi. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi ni wafuatao: Mheshimiwa Musa A. Lupatu, Mbunge wa Korogwe Magharibi, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, Mheshimiwa Eliachim J. Simpasa, Mwenyekiti wa Kikao chetu na Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Profesa Simon M.Mbilinyi, Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Profesa Juma A. Kapuya, Mbunge wa Urambo Magharibi na Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, naomba sasa niweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kama walivyochangia katika Bunge lako Tukufu. Hoja ya kwanza ilikuwa inahusu tafsiri ya neno *Court* na hili limechangiwa na Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kupitia kwa Makamu Mwenyekiti na Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, Mbunge wa Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Industrial Court*, tulivyokuwa tunajadiliana katika Kamati yetu, mtaalam kutoka kwa *Attorney General* alikuwa ameliweka hili sawa lakini Wajumbe wa Kamati wakaomba kwamba, kwa vile Muswada ule mwingine wa *Labour Regulations* ulikuwa haujaletwa Bungeni, tuendelee na *Industrial Court* lakini tumeongezea na *Court* nyingine itakayohusika na masuala ya kazi na kwa hiyo mchango wenu umezingatiwa na tutahakikisha kwamba hilo linakuwepo katika *amendment.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ni kutajwa kwa *Service Schemes.* Hili lilipiganiwa sana na *Trade Union,* pamoja na Kamati ya Bunge na Wabunge wengine humu Bungeni. Waliochangia hoja hii ni pamoja na Mheshimiwa Mrope, Mheshimiwa Kiwelu na Mheshimiwa Mjaka. Napenda nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Grace Kiwelu, kwa taarifa yake aliyoitoa hapa Bungeni, kama mwakilishi wa upande wa Upinzani kuhusu masuala ya utumishi wa umma na kwa kuchangia na kusisitiza umuhimu wa kutajwa *Service Schemes.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii imezingatiwa na kama walivyochangia wengi, basi *Service Schemes* hizi zote zitakuwa kwenye hii Sheria Mpya ili kusiwe na kisingizio chochote baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tatu, ni kurekebisha kifungu cha 4(3) ili kuongeza maneno, *"The most representative Trade Union."* Waliochangia hoja hii ni pamoja na Kamati yetu inayohusika, pamoja na Kamati pia kuna Mheshimiwa Rwilomba, Mheshimiwa Mkanga, Mheshimiwa Mutungirehi, Mheshimiwa Mongella na Mheshimiwa Nyami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafurahi kusema kwamba, hoja hii itazingatiwa katika Jedwali la marekebisho kwa sababu pengine wataalam wa *Attorney General* walikuwa na kazi nyingi, kama haionekani hivyo katika jedwali, mimi natoa ahadi hii itakuwa kwenye *Hansard,* hakutakuwa na utata wowote hivyo itajumuishwa katika sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya nne ni kuongeza kifungu kidogo cha nne kuhusu Wajumbe wa Baraza kuwa na uwezo wa kufanya maamuzi. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ililiona hili. Mheshimiwa Rwilomba naye alitaka hilo lizingatiwe. Mheshimiwa Getrude Mongella, Mheshimiwa Mkanga, Mheshimiwa Mutungirehi na Mheshimiwa Ruth Msafiri, nao walichangia. Naomba niseme kwamba, hoja hii itazingatiwa katika jedwali la marekebisho. *(Makofi)*

Kuhusu kifungu cha 7(2), kuhusu vikao vya Baraza kufanyika mara mbili kwa mwaka ambapo Kamati ya Utawala na Kamati ya Katiba na Sheria ilitaka hilo toka wakati Kamati ikiuangalia Muswada huu. Naomba niseme vile vile kwamba, hoja hii imezingatiwa katika Jedwali la marekebisho. *(Makofi)*

Kifungu kingine ambacho kilijadiliwa na Waheshimiwa Wabunge, pamoja na Kamati ni kifungu cha 17(6), Waziri kutangaza makubaliano ya Baraza kwenye Gazeti la Serikali. Hoja imezingatiwa katika Jedwali la marekebisho. *(Makofi)*

Hoja ya 7 ni kuwa Sheria kuzingatia jinsia. Hili halina mjadala. Kuhusu tafsiri ya Sheria, Sura ya kwanza haijafanyiwa marekebisho kuhusu matumizi ya baadhi ya maneno ambayo imejitokeza kuwa suala zima la jinsia katika matumizi yake halizingatiwi. Nasema kwamba, kama ilivyokuwa katika Sheria kwa kweli mara nyingi hata unaposema *Chairman* ilikuwa inamaanisha jinsia zote mbili. Lakini nafikiri kwa sababu sheria hii ndiyo inaandikwa sasa hivi haitakuwa jambo gumu kulizingatia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wengi au Wabunge wengi waliongelea umuhimu wa haki ya kuelimishwa watumishi na wadau wote. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge, wanisaidie kwa hili lakini sisi kwa upande wetu kupitia vyombo mbalimbali vya habari tutazingatia hilo. Kuhusu elimu ya haki na wajibu wa wafanyakazi na waajiri, hili lilichangiwa sana na Mheshimiwa Halinga, Mheshimiwa Getrude Mongella,

Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Mrope, Mheshimiwa Chilolo, Mheshimiwa Stephen Kazi na Mheshimiwa Profesa Mbilinyi.

Serikali inatambua umuhimu wa watumishi wa umma katika kukuza uchumi, hivyo elimu itatolewa kwa wafanyakazi wote na waajiri kuhusu Muswada huu. Ingawa ni kawaida kwa Serikali kuwaelimisha wananchi wote kwa ujumla kuhusu Muswada wowote ambao unapitia hapa Bungeni lakini ni zaidi kwa sababu tunaogopa migogoro. Tutatumia muda wetu mwingi katika kuwaelimisha wote wanaohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kifungu cha 11, kuhusu kuwepo majadiliano baina ya Bodi ya Kima cha Chini na Baraza la Majadiliano ya Pamoja, hili lilitolewa na Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa. Kwa kuwa Serikali ni moja, tutakuwa na mawasiliano na Bodi ya Kima cha Chini kuhusu kima cha chini cha mshahara. Kwa kawaida waajiri wote ni lazima au ni budi kuzingatia kima cha chini kinachokubaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu haki ya kugoma kwa watumishi wa huduma nyeti nchini, hoja hii ilichangiwa na Mheshimiwa Grace Kiwelu, vile vile ilichangiwa na Mheshimiwa Prof. Simon Mbilinyi, pamoja na Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya. Watumishi wote wa umma wamepewa haki ya kugoma ili mradi wafuate taratibu zilizoainishwa katika Muswada. Lakini vile vile jambo ambalo ni nyeti leo pengine linaweza lisiwe nyeti kesho au *situation* ambayo itakuwepo huwezi ukai-*determine* kutoka leo. Kwa vile tuko katika majadiliano na mimi nimezingatia mengi ya upande ule, ni matumaini yangu kwamba, wadau wangu watakubaliana na mimi kwamba, hili libaki lilivyo kwa sababu hatuwezi kujua jambo ambalo ni nyeti kwa sasa hivi na hili ni suala la majadiliano kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupunguza semina na makongamano, nataka kusema ya kwamba, kwa kiasi kikubwa hata Mheshimiwa Rais mwenyewe ameona ya kwamba hizi semina zimechosha na kwa hiyo jambo linapotoka kwa Mheshimiwa Rais ni kama agizo. Kwa vile leo limetoka kwenye Bunge lako Tukufu, Serikali itatoa maelekezo ya kusisitiza watendaji na watumishi wa umma kupunguza semina na warsha, makongamano na majina mengine yote yanayotumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi katika Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma, tulikwishaanza kulifanyia kazi na kwa sababu jambo hili limekuwa kero kweli. Ni kero kweli kwa sababu kwa kawaida anapoondoka mtumishi wa umma kwenye Ofisi, Ofisi inakuwa haijaondoka lakini unaweza ukakuta wale wote wenye maamuzi wameondoka kwenda kwenye makongamano, hili ni kosa. Mtumishi wa Serikali wa ngazi yoyote anapoondoka, inabidi ahakikishe ya kwamba, Ofisi yake inaendelea kufanya kazi maadam semina, makongamano na majina mengine yote tutakayoyatoa, yamewanyima haki wananchi kupata huduma ya watumishi wa umma, hili tutalivalia njuga na tunalifanyia kazi, tutalitolea maamuzi. Ni mategemeo yangu kwamba, waajiri wote na watumishi wa umma wote watatuelewa pindi tutakapotoa tamko kuhusu hili. Hata hivyo, kuna Waraka wa Rais kuhusu semina, tutasisitiza utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu marekebisho ya Sheria Na. 8 ya mwaka 2002 ambalo limetoka kwa Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa na Mheshimiwa Ponsiano Nyami. Pamoja na marekebisho yatakayowasilishwa na Serikali Bungeni, napenda kusisitiza ya kwamba, Sheria inatambua kuwa mwajiri wa watumishi wa Serikali za Mitaa ni Halmashauri husika na ndio *spirit* ya Sheria yenyewe. Sheria ya Utumishi wa Umma, *spirit* yake ilikuwa ni kupeleka mamlaka na uwezo wa maamuzi na usimamizi kwenye mamlaka husika ikiwemo Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, nilisema awali na pia narudia tena kusema ya kwamba, hili tutalishughulikia na kwa wakati muafaka, marekebisho yataletwa kwa namna ambayo nina hakika ninyi ndiyo mtakaopitisha kwa sababu katika kurekebisha Sheria haiwezi ikapitia mahali pengine isipokuwa katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu Na. 23 kuhusu Mheshimiwa Rais kutoa tuzo, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali na Mheshimiwa Ruth Msafiri, wamelisemea. Mheshimiwa Rais, anatoa tuzo pale tu ambapo hakukuwa na makubaliano hadi ikafikia hatua ya kupeleka shauri Mahakamani. Nilielezea katika maelezo yangu ya asubuhi kwamba, jambo likishapelekwa Mahakamani na Mheshimiwa Waziri mhusika, si rahisi tena kurudi kwa Mheshimiwa Waziri huyo huyo na ndiyo maana inakuwa ni vema ikarudi kwa Mheshimiwa Rais. Hayumkiniki suala ambalo limeamuliwa na Mahakama kurejeshwa kwa mmoja wa pande ambazo zinahusika na mgogoro kutolea maamuzi. Hii ndiyo mantiki ambayo inalazimu kupeleka suala hili kwa Mheshimiwa Rais, kwa maamuzi ya mwisho. Lakini vile vile Mheshimiwa Rais, ndiye mwenye maamuzi ya matumizi ya mapato ya Taifa au mapato ya Serikali.

Nimeeleza katika maelezo yangu asubuhi kwamba, mishahara ya Serikali sasa hivi ni zaidi ya asilimia 35 ya Bajeti ya Serikali na kwa hiyo utaona ya kwamba, mishahara ya watumishi inachukua sehemu kubwa sana ya Bajeti ya Serikali. Mishahara inapochukua sehemu kubwa ya Bajeti ya Serikali, maana yake kwa maeneo mengine ni kwamba, itaathiri kwa vyovyote kwa mfano, ujenzi wa barabara hata manunuzi ya dawa na mambo mengine muhimu ndani ya nchi. Kwa hiyo, kutokana na unyeti na kwamba Mheshimiwa Rais, ndiye mwenye mamlaka ya matumizi ya Bajeti ya Serikali, ningependa kuomba wadau wakubali kwamba, tuzo la mwisho lazima litolewe na Mheshimiwa Rais. Kwa vile tumekubaliana kwenye mengine, sioni kama hili litakuwa sababu ya sisi kutokubaliana leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujumuishwa watumishi wa mashirika ya umma, hili limetolewa na Mheshimiwa Musa Lupatu, kwenye mchango wake wa maandishi. Suala hili litafanyiwa kazi ili kuweza kuwajumuisha watumishi wa mashirika ya umma katika vyombo vya majadiliano. Ninyi wote mnakumbuka ya kwamba, watumishi wa mashirika ya umma walikuwa chini ya *SCOPO*, sasa hivi *SCOPO* haipo na haipo kwa sababu mashirika ya umma yamepungua lakini bado tuna mashirika machache. Sasa hivi Msajili wa Hazina ndiye anayeshughulikia masuala ya mashirika ya umma, lakini yale ya utumishi pengine yanaweza yakapunguwa na kwa hiyo kutokana na sababu hii, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma, itajaribu kuona ni namna gani itaunganisha masuala ya watumishi wa mashirika ya umma hasa kwa masuala yanayohusiana na utumishi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wachangiaji ambao waliongezeka mchana huu, ni Mheshimiwa Ndeka na mwingine ni Mheshimiwa Thomas Ngawaiya. Mheshimiwa Ndeka ametueleza mambo muhimu sana, ambayo wachangiaji wengine wameyagusia lakini kuna moja ambalo halijagusiwa na wachangiaji wengine, nalo ni kuhusu Mabaraza kuhusika na malengo ya kazi ili kuzingatia suala la tija. Hilo tutalizingatia, tumelichukua na tunamshukuru sana kwa huo mchango wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, naye alikuwa ameongelea mambo yanayohusu tuzo na tasfiri ya tuzo. Tuna tasfiri za tuzo mbalimbali lakini naomba tuwe na uhakika na tasfiri ambayo inakubalika. Tuzo kufuatana na Sheria ni uamuzi wa mamlaka husika kuhusu maslahi ya wafanyakazi unaotokana na makubaliano ya majadiliano au uamuzi unaotolewa wa mamlaka ya kazi na hasa pale kazi inapofanyika ipasavyo au vizuri. Tuzo kama alivyoongelea Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, ni zawadi na siyo maslahi na kwa hiyo lazima tutofautishe kati ya maslahi na tuzo. Maslahi ni sawa sawa na mshahara lakini tuzo ni pale kazi inapofanyika na ikaonekana ni nzuri na kwa hiyo kunahitajika kutolewa tuzo, lakini kwa maana nyingine ni maamuzi yale ambayo yanatokana na makubaliano ya majadiliano na ambayo ndiyo yatakuwa *registered* kwenye Gazeti la Serikali. Kwa hiyo, naomba tukumbuke kwamba, tuzo kama tuzo si nishani ambayo inatolewa holela holela, itatokana na majadiliano na makubaliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. Simon Mbilinyi, naye aliongelea kuhusu umuhimu wa mazungumzo kuwa yanaendelea kila siku kama njia ya kuepukana na migogoro. Mheshimiwa Prof. Simon Mbilinyi, vile vile alitukumbusha umuhimu wa kufanya tathmini ya *minimum wage* au *living wage*. Kuna tofauti kati ya *minimum wage* na *living wage*. *Minimum wage* inatokana na uwezo wa mwajiri kuweza kulipa kima cha chini lakini *living wage* ni ule mshahara ambao unatosheleza mahitaji ya msingi ya mtumishi. Kwa hiyo, inawezekana kama uwezo wa Serikali ni mdogo, *minimum wage* isiwe sawa na *living wage,* lakini nia ya Serikali na madhumuni makubwa ya Serikali ni *minimum wage* ilingane na *living wage* ili watumishi wa Serikali wasiwe watu wenye matatizo ya kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, narudia tena, suala zima la tija na ufanisi maana yake mapato yanatokana kwa kiasi kikubwa na tija na ufanyaji kazi. Utumishi wa Serikali ni msingi wa mambo mengine yote hata wafanyabiashara hawawezi wakafanya biashara kwa ufanisi bila Serikali kuwa na ufanisi na pia hata wakulima hawawezi kulima kwa ufanisi kama Serikali haifanyi shughuli zake kwa ufanisi. Mkulima atapoteza muda hospitalini badala ya kwenda kulima shambani kwake kama madaktari hawafanyi kazi kwa ufanisi na pia mfanyabiashara atapoteza biashara ya mwaka kama Serikali itamnyima leseni. Kwa hiyo, nataka muone unyeti na msingi wa utumishi wa Serikali katika uchumi wa Serikali. Kwa hiyo, napenda kusema ya kwamba, tukitaka *minimum wage* ifikie *living wage,* hatuna njia nyingine isipokuwa kufanya kazi kwa bidii na kuzingatia masuala ya tija. Itakuwa siyo jambo la busara kwa Serikali yetu kulipia mishahara hela za *grant,* hela tunayopewa kutoka nje, itakuwa si jambo la busara kwa sababu mtu anapaswa kulipwa kutokana na jasho lake, sasa unapomlipa mtu kutokana na hela za misaada maana yake ni kwamba, unamlipa zaidi ya jasho alilotoka na hivyo

haitakuwa busara na pengine tutakuwa tumeweka uhuru wetu kwa namna ambayo haitatuhakikishia kuendelea nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. Simon Mbilinyi, naye alisema ya kwamba, kuna umuhimu wa kupanua ajira. Napenda kurudia tena kwamba, pale ambapo tunaongeza mishahara bila kuzingatia tija, maana yake ni kuongeza *inflation* na kama siyo kuongeza *inflation* maana yake ni kupunguza ajira na kama siyo kupunguza ajira maana yake ni kutokuwa na uwezo wa kufanya kazi kama mazingira ya kazi si mazuri. Kwa hiyo, nakubaliana naye kwamba, kuna umuhimu wa kuongeza ajira lakini napenda kusema ya kwamba, watumishi wa umma na waajiri lazima watambue ya kwamba, kuna njia moja pekee ya kuongeza ajira na ni kufanya kazi kwa bidii na kuzingatia masuala ya tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nimalizie kwa kusema kwamba, utumishi wa umma ni utumishi ambao unapaswa kuigwa na sehemu nyingine za uchumi. Hata waajiri wa sekta binafsi wanaiangalia Serikali mshahara wake wa kima cha chini ni kiasi gani na kwa hiyo, Serikali lazima ione ya kwamba, inatenda haki kwa watumishi wake ili sekta binafsi nayo itende haki. Lakini utumishi wa umma ni kichocheo cha tija na ongezeko la mapato ndani ya Taifa. Kwa hiyo, napenda kutoa wito kwa watumishi wote kwamba, kama Serikali ilivyoona umuhimu wa kuwashirikisha katika maamuzi yanayohusu maslahi yao, basi na wao waone umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii kusudi tusiangalie upande wa haki peke yake, inabidi tuangalie na upande wa wajibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, sasa napenda kurudia tena kutoa shukrani zangu za dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kuunda Chombo cha Majadiliano ya Utatuzi wa Migogoro ya Kikazi katika Sekta ya Utumishi wa Umma wa Mwaka 2003 *(The Public Service (Negotiating Machinery) Bill, 2003)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Nimesimama kuomba tufanye marekebisho tena, marekebisho juu ya marekebisho kwenye tasfiri ya neno *"Court"*. Sasa hivi kwenye marekebisho yaliyosambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge, tasfiri ya Mahakama hiyo

inasema: *"Court means Industrial Court established under the Industrial Court Act, 1967 or any other Court which may be established for the purpose of determining or settling differences between employees and the employers"*.

Sasa kwa kutambua mchango uliotolewa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, kwa yale yanayotarajiwa kuja baadaye, tumeona ni vizuri tufanye marekebisho hapo kwa kusema kwamba, baada ya neno 67 tuendelee kusema: *"or any successor court thereto"*, tunaweka *semicolon*. Ahsante sana. *(Makofi)*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3
Kifungu cha 4

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)*

Kifungu cha 5
Kifungu cha 6

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)*

Kifungu cha 10

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 11

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)*

Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 16
Kifungu cha 17

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)*

Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 29

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa naelezea masuala ya kugoma kwa wafanyakazi kama haki yao pale wanapoona hawajatekelezewa matakwa yao, niliulizia kuhusu watumishi wa Bunge kwamba, wao wanaingia wapi katika eneo hilo? Ile *Bunge Service Commission,* wao wanaingia kwenye Sheria ipi? Nilichokuwa nataka ni ufafanuzi na kama Sheria hii inaweza ikawatambua au kuna Sheria nyingine ambayo wao wanahusika nayo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Ponsiano Nyami, kwa kunikumbusha suala ambalo nilisahau kulielezea. Kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, watumishi wa Bunge wako chini ya *Bunge Commission* na kwa hiyo hawaingii kwenye Sheria hii pamoja na kwamba, wao ni watumishi wa umma. Hii inatokana na zile *pillars* tatu za *state*. Kwa hiyo, katika *Commission* inawezekana kabisa wakaweza kuiga huu mfano wa kwetu lakini kwa sasa hivi hawamo, kwa mujibu wa Sheria ambayo ipo na ambayo inatokana na Sheria ya *Public Service*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 30

Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kuunda Chombo cha Majadiliano ya Utatuzi wa Migogoro ya Kikazi katika Sekta ya Utumishi wa Umma wa Mwaka 2003 *(The Public Service (Negotiating Machinery) Bill, 2003)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, baada ya Bunge Zima kukaa kama Kamati na kupitia kifungu kwa kifungu Muswada wa Sheria ya Kuunda Chombo cha Majadiliano ya pamoja katika Utumishi wa Umma wa mwaka 2003 *(The Public Service (Negotiating Machinery) Bill, 2003),* pamoja na marekebisho yake sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Shughuli zilizopangwa kwa siku ya leo zimekwisha. Kwa hiyo, naahirisha Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 11.25 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa Tarehe 7 Novemba, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*